GEORGE S. CLASON



TAJIRI WA BABELI


GEORGE S. CLASON
TAJIRI
WA
BABELI

Contents

Foreword

I. HARDCOPY& SOFTCOPY

MTU ALIYETAMANI DHAHABU

TAJIRI WA BABELI

TIBA SABA DHIDI YA POCHI TUPU

KUTANA NA MUNGU WA BAHATI

SHERIA TANO ZA DHAHABU

MKOPESHA PESA WA BABELI

KUTA ZA BABELI

MUUZA NGAMIA WA BABELI

MABAMBA YA VIGAE KUTOKA BABELI

MTU MWENYE BAHATI KULIKO WOTE KATIKA BABELI

Foreword

Maendeleo ya nchi yetu yanategemea maendeleo ya mtu mmoja mmoja.

Kitabu hiki kinahusu mafanikio ya kila mmoja wetu. Mafanikio ni malengo tunayotimiza kutokana na uwezo na jitihada zetu. Na maandalizi mazuri ni jambo la muhimu ili kufikia mafanikio.

Matendo yetu yanategemea fikra zetu. Nazo fikra zetu zinategemea uelewa wetu. Kitabu hiki ni muongozo katika kuelekea uelewa wa kifedha.

Lengo kuu la kitabu hiki ni kuwapa mwanga wale wenye nia ya kupata mafanikio ya kifedha. Mwanga juu ya kupata pesa, kuitunza na kutumia ziada kuzalisha zaidi.

Kitabu hiki kitaturudisha katika jiji la Babeli(Babiloni). Jiji ambalo Kanuni za pesa zinazotumika duniani leo zilianzia kutumika.

Babiloni lilikuwa jiji tajiri kuliko yote katika zama zake kwa sababu raia wake walikuwa ni matajiri. Walitambua thamani ya pesa. Walitumia kanuni bora katika kupata pesa, kutunza na kuwekeza. Pia walijihakikishia kitu ambacho sote tunatamani sana.....kipato kwaajili ya wakati ujao.

George. S. Clason.

MTU ALIYETAMANI DHAHABU

Bansir alikuwa ni mtengenezaji wa magari ya kukokotwa na farasi huko Babiloni. Alikuwa ni mtu ambaye hakuridhika na hali ya maisha yake. Siku hii alikuwa amekaa juu ya ukuta mfupi unaozunguka nyumba yake. Aliangalia kwa huzuni kajumba kake na eneo analofanyia kazi ambapo kulikuwa na gari la farasi ambalo halijaisha kutengenezwa.

Mara kwa mara mke wake alionekana mlangoni. Kwa jinsi alivyokuwa akimuangalia, ilimkumbusha kuwa unga ulikuwa unakaribia kuisha hivyo anatakiwa kufanya kazi gari lile liishe. Agongelee, akate, apige msasa, apige rangi, aweke matairi na kupamba, kisha alipeleke kwa mteja wake ili apate pesa.

Hata hivyo mwili wake mnene na uliojengeka uliendelea kukaa kizembe juu ya ukuta. Akili yake nzito ilikuwa inahangaika kutatua tatizo ambalo hakuweza kupata jibu lake.

Joto na jua kali la kwenye bonde la mto Efrati lilikuwa likimpiga bila huruma. Matone ya jasho kama shanga yalimtoka kwenye paji la uso. Yalimtiririka mpaka kwenye kifua chake chenye vinyweleo vingi bila yeye mwenyewe kujua wala kutilia maanani.

Mbali na nyumba yake kulikuwa na jumba kubwa la Mfalme lililokuwa limezungukwa na ukuta. Pembeni yake kulikuwa na jengo refu lililopakwa rangi; hekalu la Bel(Bwana, Marduki). Katikati ya majengo makubwa na ya kifahari namna hiyo, kulikuwa na kajumba kake na vijumba vingine vichafu zaidi.

Babiloni ulikuwa ni mji wa namna hiyo, mchanganyiko wa ufahari na uchafu. Utajiri mkubwa na umaskini wa kutupwa. Vilichanganyika na kujazana pamoja bila mpango ndani ya ukuta wa jiji.

Nyuma yake (Japo hakugeuka kuangalia) kulikuwa na kelele za magari ya kukokotwa na farasi ya watu matajiri, yakipita sambamba na wafanyabiashara waliovaa makubazi na ombaomba waliokuwa peku.

Matajiri walilazimika kuegesha magari yao pembeni kupisha msafara mrefu wa watumwa waliobeba maji kwaajili ya kazi za mfalme. Kila mmoja wao alibeba mfuko mzito wa maji uliokuwa umetengenezwa kwa ngozi ya mbuzi. Walikuwa wanayapeleka kwenye bustani zinazoelea za Babiloni.

Bansir alikuwa amezama kwenye mawazo kuhusu shida zake wala hakukazia akili vurugu za mji. Alishtushwa na mlio wa kinubi ambao haukuwa mgeni kwake. Aligeuka na kukutana na uso unaotabasamu wa rafiki yake kipenzi; Kobbi, mwanamuziki.

“Baraka za Miungu ziwe nawe rafiki yangu,” alisalimia Kobbi. “Inaonekana Miungu ni wema sana kwako hadi huna

haja ya kufanya kazi! Nafurahia bahati yako maana na mimi naweza kufaidika nayo. Bila shaka mifuko yako imetuna, vinginevyo ungekuwa unapiga kazi saa hizi. Nikopeshe shekeli mbili, nitakulipa jioni baada ya karamu ya matajiri."

"Yaani hata kama ningekuwa na shekeli mbili nisingekukopesha," akajibu Bansir kwa unyonge. "Nisingekopesha mtu yeyote, hata wewe nisingekukopesha. Hizo ndizo zingekuwa kila kitu kwangu na mtu hawezi kukopesha kila kitu alichonacho, hata kwa rafiki yake kipenzi."

"Unasema!" Akashangaa Kobbi. "Inamaana hauna hata shekeli moja mfukoni lakini umekaa juu ya ukuta kama sanamu! Kwanini usimalizie hilo gari? Sasa utapataje mahitaji yako? Siyo kwa mtindo huo rafiki yangu. Nguvu zako za siku zote ziko wapi? Kuna kitu kimekukwaza, Miungu imekuletea matatizo?"

"Itakuwa ni mateso toka kwa Miungu," alikubali Bansir. "Ilianza kama ndoto, ndoto isiyo na maana. Ndani ya ndoto nilikuwa ni mtu wa maana. Kwenye mkanda wangu wa kiunoni ilining'inia pochi nzuri iliyojaa pesa. Kulikuwa na pesa nyingi kiasi kwamba ningeweza kugawia ombaomba bila kujali kuishiwa; nilikuwa na dhahabu zilizonifanya nijihisi salama hata kwa siku za usoni na wala sikuogopa kutumia pesa. Nilikuwa ni mtu niliyeridhika sana. Usingenijua kama ni mtu mwenye bidii ya kazi wala mke wangu usingemtambua. Uso wake haukuwa na makunyanzi na uling'ara kwa furaha,

alikuwa mwanamwali tena, kama alivyokuwa mwanzo nilipomuoa.”

“Ndoto tamu kweli,” akasema Kobbi. “Lakini kwanini ndoto tamu hivyo ikufanye ukae juu ya ukuta kama sanamu?”

“Hilo ndilo swali! Nilipoamka na kukumbuka jinsi mifuko yangu ilivyo mitupu, hisia za uasi na kutojali zikaniingia. Ngoja tuongelee hilo suala pamoja. Kama mabaharia wasemavyo; mimi na wewe tupo ndani ya mtumbwi mmoja. Wakati tukiwa wavulana tulijifunza pamoja kwa kuhani. Tulipokuwa vijana tulifurahia maisha pamoja. Na katika utu uzima tumekuwa marafiki wa karibu. Tumekuwa watu wa kuridhika. Tumeridhika kufanya kazi kwa masaa mengi na tunatumia mapato yetu kwa uhuru. Tumepata pesa nyingi kwa miaka yote tuliyofanya kazi lakini furaha ya utajiri tunaipata ndotoni tu. Bah! Tunatofauti gani na kondoo wasioelewa kitu? Tunaishi kwenye mji tajiri zaidi duniani. Wasafiri wanasema hakuna mji unaofanana nao kwa utajiri lakini sisi hatuna kitu. Baada ya kufanya kazi ngumu kwa nusu ya maisha yangu, mimi, wewe na rafiki zetu wengine, hatuna kitu.’

“Naweza kuazima shekeli mbili na nitakulipa jioni? Nilijibuje? Nilisema kuwa hii hapa? Hapana, nilikubali kuwa mifuko yangu haina kitu kama yako tu.

“Shida yetu nini? Kwanini hatuwezi kuwa na fedha na dhahabu zaidi ya zinazotosha nguo na chakula tu?

“Fikiria kuhusu wana wetu” aliendelea Bansir. “Je, hawafuati hatua zetu? Si kwamba wao, familia zao, na familia

za watoto wao wataishi katikati ya dhahabu na utajiri kama sisi lakini wataridhika na kunywa maziwa mgando ya mbuzi na uji tu?"

"Katika maisha yote ya urafiki wetu sijawahi ona ukiongea kama hivi Bansir," alishangaa Kobbi.

"Miaka yote hiyo sijawahi pata mawazo kama haya," akajibu Bansir . "Toka asubuhi hadi giza linapoingia nimekuwa nikitengeneza magari bora sana. Nilitegemea siku moja Miungu itaona kazi yangu nzuri na kunitunuku mafanikio. Hawajawahi fanya hivyo na mwishowe nimegundua hawatakuja kufanya hivyo. Natamani kumiliki ardhi na ng'ombe. Kuwa na nguo nzuri na pesa mfukoni.

Niko tayari kufanya kazi kwa nguvu na akili zangu zote ili kupata vitu hivyo. Natamani kazi yangu inilipe ninavyostahili. Kwani tuna mkosi gani? Nikuulize tena! Kwanini hatuna vitu vizuri?"

"Unafikiri najua jibu?" Alijibu Kobbi. "Mimi ni kama wewe tu. Mapato kutokana na kinubi changu yanaisha haraka sana. Muda wote inanibidi niumize akili ili familia yangu isijepatwa na njaa. Pia moyoni mwangu natamani kupata kinubi kikubwa zaidi ili niweze kupiga muziki hasa. Kinubi kama hicho kinaweza kutoa muziki bora ambao hata Mfalme hajawahi kuusikia. Na si mfalme tu, hata Miungu watashangazwa na muziki wake mzuri.

Lakini nawezaje kupata kinubi bora ikiwa sote ni maskini kama watumwa wa mfalme tu? Sikiliza kengele! Hao wanakuja." Akaonyesha kwenye msafara mrefu wa watumwa

waliotoka mtoni. Waliokuwa wamebeba maji huku wakiwa nusu uchi, jasho likiwatiririka huku wakitembea kwa taabu kutoka mtoni. Walitembea watano watano huku wamebeba mifuko mizito ya ngozi ya mbuzi ikiwa imejaa maji.

“Anayewaongoza ana afya nzuri,” akasema Kobbi huku akionyeshea kwa mtu aliyevaa kengele akiongoza mbele ya msafara, yeye alikuwa hana mzigo wowote. “Bila shaka ni mtu wa maana huko kwao, si unamuona!” Akaendelea kusema Kobbi.

“Watu wengi tu kwenye huo msafara wamejengeka vizuri,” alisema Bansir. “Wako kama sisi tu. Warefu, weupe kutoka kaskazini, weusi kutoka kusini na wa kahawia kutoka nchi za jirani. Wote wanatembea kutoka mtoni hadi bustanini, kwenda na kurudi. Hawategemei furaha yoyote. Usiku kitanda cha nyasi kinawasubiri na chakula chao ni makande. Waonee huruma Kobbi!”

“Unawahurumia lakini mimi sioni tofauti yao na yetu japo tunajiita watu huru,” akasema Kobbi.

“Hilo ni kweli Kobbi, ukweli mchungu. Hatujapenda kuishi kama watumwa miaka na miaka. Kufanya kazi kwa bidii bila kufika popote,” akasema Bansir kwa unyonge.

“Unaonaje na sisi tujue jinsi wenzetu wanavyopata mafanikio? Unaonaje na sisi tuwaige?” Akauliza Kobbi.

“Pengine kuna siri tunaweza kujifunza tukiuliza wale waliofanikiwa,” akaongezea Bansir kwa matumani.

“Huwezi amini! Leo hii hii nimekutana na rafiki yetu wa zamani Arkad,” akasema Kobbi. “Alikuwa amepanda gari

lake la dhahabu. Nilipomuona nikajisemea moyoni, 'hawezi kuniangalia mtu wa chini hivi, hana tofauti na matajiri wengine.' Nikashangaa ananipungia mkono. Watu wote walishuhudia tajiri mkubwa akimsalimia Kobbi mpiga kinubi kwa uchangamfu!"

"Inasemekana ndiye tajiri kuliko wote hapa Babiloni," akasema Bansir kwa kustaajabu.

"Ni tajiri hadi inasemekana mfalme huomba msaada wa kifedha kwake," akasema Kobbi...

"Tajiri sana," Bansir akamkatiza. "Ninaogopa siku nikikutana naye kwenye giza naweza kumpora".

"Acha ujinga!" Kobbi akamzodoa. "Mtu hatembei na utajiri wake mfukoni. Mifuko huwa mitupu haraka iwapo hakuna namna ya kuijaza tena. Arkad ana kipato ambacho kinafanya mifuko yake itune muda wote, haijalishi ana matumizi ya kiasi gani."

"Kipato! Hicho ndiyo kitu muhimu." akasema Bansir kwa furaha. "Natamani kuwa na kipato ambacho kitakuwa kinaingia hata nikisafiri nchi za mbali au nikikaa juu ukutani kama sanamu. Arkad atakuwa anajua jinsi ya kuwa tajiri. Unafikiri anaweza kunielewesha mtu mwenye akili nzito kama mimi?"

"Nafikiri inawezekana, mbona aliweza kumfundisha mtoto wake Nomasir," akajibu Kobbi "Nilisika watu wakisema kuwa kijana wake alienda Ninawi, na bila msaada wa baba yake, amekuwa mmoja ya watu matajiri huko Ninawi."

“Kobbi umenipa wazo,” akasema Bansir huku macho yake yaking’aa kama mtu aliyegundua jambo. “Haitupunguzii kitu kupata ushauri kwa rafiki, na Arkad ni rafiki mzuri. Tusijali kuwa mifuko yetu ni mitupu kama kiota cha mwaka jana cha kipanga. Twende tusiogope. Tumechoka kuwa maskini katikati ya utajiri mwingi. Kama tumedhamiria kuwa watu wa maana na twende kwa Arkad tumuulize cha kufanya ili na sisi tuwe na kipato cha kueleweka.”

“Umeongea kweli tupu Bansir. Umenifungua akili. Umenifanya nielewe kuwa sababu ya kutokuwa na utajiri ni sababu hatujautafuta. Umefanya kazi kwa bidii kutengeneza magari bora, kwa hilo umefanikiwa. Mimi nimefanya bidii kuwa mpiga kinubi hodari na nimefanikiwa katika hili. Kwa kila jambo tulilotia bidii na kutumia akili zetu zote tulifanikiwa. Miungu ilitubariki.

Sasa tumeona mwanga, kama mwanga wa jua linalochomoza. Inatubidi kujifunza zaidi ili kufanikiwa zaidi. Tukiwa na maarifa tunaweza kupata njia bora za kutimiza matamanio yetu.”

“Twende zetu kwa Arkad leo hii hii,” akasema Bansir. “Pia tuwapitie rafiki zetu wengine ambao hali zao ni kama sisi wajiunge nasi kupata maarifa ya Arkad.”

“Hilo ni jambo zuri Bansir! Kuwaza kuhusu rafiki zako. Kama ulivyosema, twende tuwapitie na twende kwa Arkad leo hii hii.”

TAJIRI WA BABELI

Hapo zamani kwenye mji wa Babiloni aliishi mtu mmoja tajiri sana aliyeitwa Arkad. Utajiri wake ulisifika hadi nchi za mbali sana. Pia alisifika kwa utoaji wake. Alikuwa na roho ya utoaji, hakuwa na choyo kwa familia yake na kwa watu baki pia. Wala hakuwa mbahili kwenye matumizi. Pamoja na hayo, kila mwaka utajiri wake uliongezeka kwa kasi kuliko alivyoutumia.

"Siku moja rafiki zake wa utotoni walimjia na kusema, "Arkad wewe umebarikiwa kuliko sisi. Umekuwa mtu tajiri kuzidi wote katika Babiloni wakati sisi ni watu wa kubangaiza tu. Unaweza vaa nguo bora kabisa, na kula chakula kizuri wakati sisi tunavalisha familia zetu kile kinachopatikana, na tunakula kile tunachoweza pata."

"Zamani tulikuwa sawa, tulisoma wote chini ya mkufunzi mmoja, na tulicheza michezo pamoja. Na si katika masomo wala michezo ambako ulikuwa bora kutuzidi. Na kwa miaka mingi baada ya hapo ulikuwa raia wa kawaida kama sisi tu. Na si kwamba unafanya kazi kwa bidii kuliko sisi au ni muaminifu kutuzidi. Sasa kwanini bahati ikuchague wewe tu kufurahia vitu vizuri vya maisha na kutuacha sisi ihali kila kitu tunafanana?"

Hapo Arkad akapinga na kusema, “Kama hamjafanikiwa kupata zaidi ya mahitaji ya kuwafanya muishi tu toka tulipokuwa vijana, ni kwasababu mmeshindwa kujifunza sheria zinazoongoza ujengaji wa utajiri, au mmeshindwa kuzitambua.

“Bahati! Bahati ni Mungu katili ambaye hawezi kumletea mtu mafanikio ya kudumu. Kinyume chake huleta maangamizi kwa karibu kila mtu anayempatia dhahabu. Anafanya wawe watumiaji wabaya ambao baada ya muda mfupi hubaki bila kitu bali matamanio wasiyoweza timiza. Wengine huwafanya wawe mabahili wanaoogopa kutumia utajiri walionao. Wakijua hawana uwezo wa kupata tena iwapo watatumia. Hawa hupatwa na uoga juu ya majambazi na huishia kuishi maisha ya usiri, kujitenga na wasiwasi mwingi.

“Wapo pia ambao huchukua dhahabu waliyofanikiwa kuipata kwa bahati na kuifanya iongezeke. Hawa huwa na furaha na kuridhika. Lakini wa aina hii ni wachache sana. Mi sijawahi ona bali nawasikia tu. Hebu fikirieni kuhusu watu waliopata utajiri kwa kurithi na muone kama ninalosema lina ukweli.”

Rafiki zake walikiri kuwa; watu waliowafahamu wamepata utajiri kwa kurithi, maneno yake ni kweli. Wakamuomba awaeleze ni jinsi gani ameweza kuwa na mafanikio makubwa kiasi kile.

Arkad akaendelea kusema, “Katika ujana wangu niliangalia na kuona vitu vingi vizuri vinavyoweza kuleta

furaha na kuridhika. Nikagundua kuwa, utajiri hufanya vyote hivyo vipatikane. Utajiri ni nguvu, hufanya vitu vingi viwezekane.

“Mtu anaweza kupamba nyumba yake kwa vitu vya gharama. Kusafiri bahari za mbali na kula vyakula adimu kutoka nchi za mbali. Anaweza kununua mapambo kutoka kwa sonara wa dhahabu au kwa mchonga mawe ya vito. Mwingine anaweza hata kujenga mahekalu makubwa kwaajili ya Miungu.

“ Mtu anaweza kufanya hivi na vingine vingi vya kuridhisha nafsi yake.

“ Nilipogundua hili, nikaamua kuwa nitahakikisha na mimi napata sehemu ya vitu vizuri maishani. Sitakuwa kati ya wale wanaosimama pembeni na kuangalia kwa kutamani wengine wakifurahia maisha. Sitaridhika na kuvaa midabwada. Sitaridhika na vitu vya kimaskini. Nitajitahidi niwe mshiriki wa karamu ya vitu vizuri.

“Kama mnavyofahamu, mimi ni mtoto wa mfanyabiashara wa kawaida tu. Familia yetu ilikuwa kubwa sana kwa hiyo sikuwa na matumaini ya urithi. Pia kama mlivyosema, sikuwa na akili sana wala vipaji vyovyote kuwazidi. Niligundua kuwa ili kufikia malengo yangu nilihitaji kujifunza na kutumia muda vizuri.

“Kuhusu muda, watu wote tuna muda wa kutosha. Hata nyinyi mlikuwa na muda wa kutosha kuwafanya kuwa matajiri, lakini mmesema wenyewe kuwa hamna kitu zaidi ya familia zenu. Ndiyo kitu pekee mnachojivunia.

“Kuhusu kujifunza, je, mwalimu wetu hakutufunza kuwa kujifunza kupo kwa aina mbili? Aina ya kwanza ni juu ya vitu tunavyofundishwa na kufahamu. Aina ya pili ni mafunzo yanayotufundisha jinsi ya kutafiti na kuelewa vitu tusivyoelewa.

“Kwa hiyo nikaamua kujifunza jinsi ya kuwa tajiri na kufanyia kazi niliyojifunza kikamilifu. Hamuoni kuwa ni busara kufurahia maisha ingali bado tupo hai kabla ya kuingia kwenye giza la kifo?

“Nilipata kazi kama muandishi kwenye jumba la kumbukumbu. Nilifanya kazi masaa mengi nikiandika kwenye mabamba ya vigae. Wiki baada ya wiki na miezi baada ya miezi nilifanya kazi. Hata hivyo sikuwa na chochote cha kuonyesha kwa kazi yangu hiyo ngumu.

“Pesa yangu yote iliishia kwenye chakula, nguo, sadaka na vitu vingine vidogovidogo. Lakini sikukata tamaa kuhusu lengo langu.

“Siku moja, Aligamishi, tajiri mkopesha pesa, alikuja kwa msimamizi wa mji na kuomba apate nakala ya sheria ya tisa. Alisema kuwa anataka kazi yake ikamilike ndani ya siku mbili. Niliambiwa nikifanikiwa kufanya kazi hiyo kwa siku mbili nitapewa zawadi ya sarafu mbili za shaba.

“Nilifanya kazi kwa bidii lakini sheria ya tisa ilikuwa ndefu sana. Aligamishi aliporudi na kukuta kazi yake haijaisha alikasirika sana. Kama ningekuwa mtumwa wake hakika angenipiga. Lakini kwa kujua kuwa msimamizi wa mji asingemruhusu anipige, sikuogopa, nikamwambia,

“‘Aligamishi wewe ni tajiri sana. Niambie jinsi ya kuwa tajiri nami nitafanya kazi yako usiku kucha, asubuhi itakuwa tayari.’

“Akatabasamu na kusema, ‘We mjanja sana, basi na iwe hivyo’

" ‘Usiku kucha nilikesha nikiandika, japo mgongo uliuma na harufu ya utambi iliniumiza kichwa hadi macho yakawa hayaoni vizuri. Alipofika asubuhi kazi yake ikawa tayari.”

“Hapo nikamwambia, ‘Niambie ulichoniahidi’

“Kijana wangu umefanya sehemu yako kwa ukamili,’ aliniambia kwa upole. ‘Sasa ngoja nami nitimize sehemu yangu. Nitakwaambia ujuzi huo kwasababu nimezeeka na ulimi wa wazee hupenda kuongea. Vijana wanapoomba ushauri kutoka kwa wazee, hupata hekima ya miaka mingi. Lakini mara nyingi vijana hufikiri kuwa hekima ya wazee imepitwa na wakati, hilo linafanya wakose kufaidika.

“Kumbuka hili jambo, jua lililowaka wakati wa baba yangu ndilo hilo hilo litakalokuwa linawaka mjukuu wangu wa mwisho atakapokufa.

“Mawazo ya ujana,’ akaendelea kusema. ‘Ni kama mwanga mkali wa kimondo kinachopita angani kwa kasi. Lakini hekima ya wazee ni kama nyota inayoangaza siku zote kiasi kwamba mabaharia huitegemea kuwaongoza.

" ‘Nisikilize kwa makini nitayokueleza na uelewe, vinginevyo kazi yako ya usiku kucha itakuwa ni kazi bure.’ Hapo aliniangalia kwa makini kwa macho yake yaliyokuwa yamefunikwa na makunyanzi, kwa sauti ya chini lakini

thabiti, akaniambia. ‘Niliipata njia ya utajiri nilipoamua kwamba *sehemu ya kumi ya kipato changu ni yangu*. Na wewe unatakiwa ufanye namna hiyo.’

“Hapo akaendelea kuniangalia kwa macho ambayo nilihisi kama yananichoma,lakini hakuongea zaidi.

" ‘Ni hilo tu?’ Nilimuuliza.

" ‘Hilo lilitosha kubadilisha moyo wa mchunga kondoo, kuwa moyo wa mkopesha pesa,’ alinijibu.

“Lakini mbona kila ninachopata ni changu mwenyewe?’ nikahoji.”

“Unajidanganya,’ akasema. ‘Je humlipi mshona nguo? Humlipi mtengeneza makubazi? Haulipii vitu unavyokula? Unaweza kuishi Babiloni bila kutumia pesa? Una nini cha kuonyesha kutokana na kipato chako cha mwezi uliopita? Vipi mwaka uliopita? Unalipa watu wote, kasoro wewe mwenyewe. Usiye na akili! Unafanyia wengine kazi. Ni sawa tu na kuwa mtumwa na kufanya kazi kwa yule anayekupa chakula na mavazi. Iwapo ungetunza sehemu ya kumi ya pato lako lote, ungekuwa na kiasi gani ndani ya miaka kumi?’

“Hesabu bado zilikuwa zinachaji kichwani mwangu, ‘Itakuwa sawa na pato langu la mwaka mmoja’, nikajibu.

" ‘Kwa kiasi fulani upo sahihi’ alisema. ‘Kila kipande cha dhahabu ulichojilipa ni mtumwa wa kukufanyia kazi. Kila senti unayopata ni mtoto anayetakiwa kukuzalishia. Ili kuwa tajiri, kile unachotunza kinatakiwa kikuzalishie, na watoto wake wakuzalishie pia. Hilo ndilo linaweza kukufanya ufikie matamanio yako ya kuwa na mali.

" ‘Unaweza dhani nakudanganya na umekesha bure, lakini ninachokupa kina thamani mara elfu ya kazi uliyofanya. Unatakiwa tu kuwa na akili ya kuelewa.’

‘' ‘Lazima ujilipe sehemu fulani ya pato lako. Haitakiwi kuwa chini ya sehemu ya kumi ya pato lako lote, hata kama pato lako ni dogo kiasi gani. Lakini inaweza kuwa zaidi ya hapo kulingana na uwezo wako. Lazima ujilipe kwanza na panga matumizi yako vizuri, usinunue nguo na viatu kwa pesa nyingi hadi ukakosa pesa ya kutoa misaada na sadaka.

" ‘Utajiri ni kama mti, unakua kutoka kwenye mbegu ndogo sana. Pesa kidogo unayoanza kutunza ndiyo mbegu ya mti wa utajiri wako. Unavyopanda mapema ndivyo na mti utakua mapema. Na kadri unavyotunza mti wako kwa kuumwagilia kwa kutunza pesa, ndivyo utakavyokaa na kufurahia kivuli chake mapema,’

“Baada ya kusema hayo, alichukua mabamba yake na kuondoka.”

“Nilifikiria kwa makini kile alichokuwa ameniambia na nikaona kinapatana na akili, nikaazimia kukifanyia kazi. Kila mara nilipolipwa, nilichukua sehemu ya kumi ya pato na kuitunza. Jambo la ajabu ni kwamba sikupata shida yoyote ya mahitaji yangu. Tofauti ilikuwa ndogo sana na baadaye nikazoea. Akiba yangu ilipoanza kukua nikaanza kupata kishawishi cha kuitumia. Nilitamani kununua vitu vizuri vilivyoletwa na meli na ngamia kutoka kwa wafoenike lakini nikajizuia.

“Baada ya miezi kumi na miwili Aligamishi akarudi tena. Akaniuliza, ‘kijana, ulifanikiwa kujilipa sehemu ya kumi ya pato lako kwa mwaka uliopita?’

“Ndiyo mkuu, niliweza,” nilijibu kwa kujivuna.

‘' ‘Vema sana,’ akajibu Aligamishi akiwa kafurahi, ‘Umefanyia nini?’

‘' ‘Nimempatia Azmur, mfyatua matofali. Aliniambia atafanya safari kwenda nchi za mbali, na akifika Tiro ataninunulia vito adimu kutoka kwa wafoenike. Akirudi tutauza kwa bei kubwa na kugawana faida,’

‘' ‘Kila mpumbavu anatakiwa kujifunza,’ alifoka Aligamishi, ‘Kwanini umemuamini mfyatua matofali kwa jambo linalohusu vito? Unaweza kwenda kwa muoka mikate kuuliza kuhusu mambo ya nyota? Hapana! Utaenda kwa mnajimu iwapo una akili. Akiba yako imeshapotea, umeng’oa mti wako wa utajiri. Lakini unaweza panda upya. Jaribu tena, na wakati mwingine ukitaka habari za vito nenda kwa sonara. Ukitaka kujua kuhusu kondoo, nenda kwa mfuga kondoo.

“ ‘Ushauri mara nyingi ni kitu ambacho hutolewa bure, lakini kuwa makini na hakikisha unachukua ule unaofaa tu. Anayechukua ushauri kuhusu akiba yake kutoka kwa mtu ambaye hana uzoefu, ataipoteza kwanza, ndipo atajua kuwa haufanyi kazi.’ Baada ya kusema hayo akaondoka.

“Kama alivyokuwa amesema Aligamishi, wafoenike walimtapeli Azmur. Walimuuzia vioo vilivyoonekana kama vito. Lakini kama Algamish alivyonihimiza, nikaanza kutunza

tena kila sehemu ya kumi ya pato langu. Kwa vile nilikuwa nimeshazoea, haikuwa kazi ngumu.

“Baada ya miezi kumi na miwili Algamishi alirudi tena, alinitafuta na kuniuliza, ‘Umefikia wapi toka tulipoonana?’

‘' ‘Nimejilipa kwa uaminifu’, nilijibu. ‘Akiba yangu nimempatia Aggar mtengeneza ngao, alienda kununua shaba na kila baada ya miezi minne ananilipa.

‘' ‘Vyema sana. Na hiyo pesa anayokulipa umeifanyia nini?’

‘' ‘Nimefanya karamu kubwa ikiwa na asali, divai na keki zenye viungo. Pia nimenunua kanzu ya rangi nyekundu-angavu na nina mpango wa kununua punda wa kutembelea.’

“Aliposikia hivyo Aligamishi alicheka, kisha akasema, ‘Unakula watoto wa akiba yako. Sasa unategemea watakufanyiaje kazi? Na watawezaje kuwa na watoto ambao watatakiwa kukufanyia kazi?

“ ‘Tengeneza kwanza jeshi la watumwa wa dhahabu na utafurahia karamu nyingi bila wasiwasi? ‘

“Baada ya kusema hayo aliondoka tena.

“Sikumuona tena kwa miaka miwili. Aliporudi alikuwa amezeeka sana, akaniambia, ‘Arkad, umefanikiwa kupata utajiri ulioutaka?’ “Sijafanikiwa lengo bado lakini nilicho nacho kinazalisha na kilichozalishwa nacho kinazalisha,” nilijibu.

‘' ‘Bado unachukua ushauri kutoka kwa wafyatua matofali?’

'' 'Labda kuhusu matofali, hapo wanatoa ushauri mzuri sana,' nilijibu.

'' 'Umejifunza somo hili vizuri sana Arkad. Kwanza ulijifunza kuishi chini ya kipato chako. Kisha ukajifunza kupata ushauri kwa wale wenye uzoefu, na mwisho umejifunza kufanya fedha ikufanyie kazi.

'' 'Umejifunza jinsi ya kupata pesa, jinsi ya kuitunza na jinsi ya kuitumia. Sasa upo tayari kwa majukumu makubwa zaidi. Mimi sasa nimekuwa mzee na wana wangu wanafikiria kutumia pesa tu, hawawazi namna ya kujiongezea kipato. Miradi yangu ni mingi na nina wasiwasi sitaweza kuisimamia vizuri. Kama utaweza kwenda Nippur na kusimamia miradi yangu, nitakufanya kuwa mshirika wangu na utakuwa na hisa kwenye mali zangu.'

"Kwa hiyo nikaenda Nippur na kusimamia mali zake, alikuwa na mali nyingi sana. Kwa sababu nilikuwa ni mtu mwenye malengo na sasa nilikuwa nimejifunza zile sheria tatu za jinsi ya kusimamia utajiri niliweza kukuza sana mali zake.

"Nilitajirika sana. Algamish alipokufa nilibaki na hisa zangu kwenye mali ile kama alivyoandaa kwenye mkataba." Hayo ndiyo aliyozungumza Arkad.

"Alipomaliza kuongea mmoja wa rafiki zake akasema, "Ulikuwa na bahati sana kwa Aligamishi kukufanya kuwa mrithi wake."

"Nilikuwa na bahati kwa sababu nilikuwa na matamanio ya kufanikiwa hata kabla hatujaonana naye. Je, sikuonyesha

uwezo wangu kwa kutunza sehemu ya kumi ya pato langu kwa miaka minne? Unawezaje kumuita mvuvi ambaye kwa miaka mingi amesoma tabia za samaki na anajua majira mazuri ya kushusha nyavu ana bahati?

"Bahati ni Mungu katili ambaye ambaye hapotezi muda na wale ambao hawako tayari."

"Ila Arkad una moyo mgumu sana. Maana baada ya kupoteza akiba yako ya mwaka wa kwanza bado hukukata tamaa. Upekee wako upo hapo," alisema rafiki yake mwingine.

"Moyo mgumu!" Alisema Arkad akishangaa. Upuuzi! Unafikiri moyo mgumu unaweza kumpa mtu nguvu za kunyanyua mzigo ambao ngamia hawezi, au kukokota kitu ambacho ng'ombe wa kukokota hawezi hata kukitikisa? Si moyo mgumu bali nia ya kufanya jambo ulilolipanga mpaka likamilike. Kama nimejiwekea lengo, hata liwe gumu kiasi gani nitahakikisha nalikamilisha. Vinginevyo nawezaje kujiamini kutimiza mambo muhimu?

"Nikijiambia, 'kwa siku miamoja nikipita kwenye daraja la kuelekea mjini, nitaokota jiwe dogo barabarani na kulitupa kwenye maji, nitafanya hivyo. Iwapo siku ya saba ikifika na nikasahau kutupia jiwe nitajiambia, 'haina shida kesho nitatupia mawili?' Si ni kitu kile kile? Hapana! Nitarudi na kutupia jiwe mtoni. Wala ikifika siku ya ishirini siwezi sema, 'Arkad, hili ni jambo la kijinga, inakusaidia nini kurusha jiwe mtoni kila siku? Tupia yote kwa wakati mmoja na uwe umemalizana na hili jambo. Hapana! Sitasema wala kufanya

hivyo. Nikijiwekea lengo lazima nilikamilishe. Kwa sababu hiyo, nipo makini sana kutoanzisha vitu vigumu na visivyowezekana kwa sababu sipendi kujitesa."

Hapo rafiki yake mwingine akasema. "Kama unayosema ni kweli, na kwa jinsi ulivyoeleza inaonekana ni kweli. Sasa ikiwa ni rahisi namna hiyo, na kila mtu akifanya hayo, kutakuwa na utajiri wa kutosha wote?"

"Utajiri hukua pale watu wanapofanya kazi," akajibu Arkad. "Iwapo tajiri amejenga jumba kubwa, pesa alizotumia zinapotea? Hapana, mfyatua matofali anapata kidogo na vibarua nao wanapata kidogo. Wasanifu nao hupata kidogo, na kila mtu aliyefanya kazi kwenye ujenzi wa nyumba hiyo hupata kidogo. Lakini je, nyumba iliyojengwa haiwi na thamani sawa na dhahabu iliyotumika? Na ardhi ambamo imejengwa haipandi thamani kwa sababu sana ina nyumba? Na ardhi inayopakana nayo haiongezeki thamani kwa sababu inapakana na jumba kubwa? Utajiri hukua kimaajabu sana. Hakuna anayeweza kutabiri mwisho wake. Je, wafoenike hawajajenga majiji makubwa kwenye pwani za jangwani kutokana na utajiri unaoletwa na meli zao za biashara?

"Kwa hiyo unatupa ushauri gani juu ya cha kufanya ili nasi tuwe matajiri? Maana miaka inaenda na uzee unaingia lakini hatuna tulichowekeza." Alisema rafiki mwingine tena.

"Nawashauri kuchukua ushauri wa Aligamishi na kujiambia, 'sehemu fulani ya pato langu ni yangu.' Sema hivyo asubuhi unapoamka, sema mchana, sema na usiku.

Sema kila saa ya siku. Jiambie hivyo hadi maneno hayo yatokee kama herufi za moto angani.

“Jaza wazo hili ndani yako na tunza kiasi unachoona kinafaa ila isiwe chini ya moja ya kumi ya pato lako. Ikiwa kuna ulazima, badili matumizi yako ili kufanikisha hili. Baada ya muda utaanza kuhisi hisia za utajiri. Akiba inayokua itakuletea furaha, furaha ya kumiliki kitu chako mwenyewe. Kadri hazina yako inavyokua ndivyo utakavyochochewa kuweka zaidi. Utapata furaha maishani na nguvu ya kutafuta zaidi itakuingia. Je, kadri unavyopata zaidi si na kiasi unachotunza kitaongezeka?

“Baada ya hapo jifunze jinsi ya kufanya akiba yako ikutumikie. Ifanye mtumwa wako. Wafanye watoto wake na watoto wa watoto wake wakutumikie.

“Hakikisha una kipato kwaajili ya siku zijazo. Waangalie wazee na kumbuka kuwa siku zijazo nawe utakuwa mzee. Hivyo wekeza kwa tahadhari ili hazina yako isipotee. Biashara zenye kudai zina faida kubwa ni mtego na udanganyifu. Ni nyimbo zinazoimbwa ili kumvuta mtu asiye makini kwenye hasara na majuto.

“Hakikisha familia yako haitateseka iwapo Miungu wakikuita. Unaweza fanya hivyo kirahisi kwa kutunza pesa kidogokidogo mara kwa mara. Mtu mwenye fikra za mbele hasubiri kupata kiasi kikubwa ndiyo akitunze au akiwekeze kwa wakati ujao.

“Jadiliana na watu wenye hekima. Tafuta ushauri kutoka kwa wale wanaofanya kazi zihusuzo pesa kila siku. Hao

watakusaidia kuepuka makosa kama niliyofanya mimi kwa kumpa pesa zangu Azmur, mfyatua matofali. Faida ndogo penye usalama ni bora kuliko faida kubwa lakini penye hatari ya kupoteza mali zako.

“Furahia maisha ungali bado upo duniani. Usijibane kupita kiasi ili kutunza pesa, na usijaribu kutunza kiasi kikubwa kuliko uwezo wako. Kama sehemu ya kumi ndiyo unayoweza kutunza bila kupata taabu basi ridhika na kutunza kiwango hicho tu. Ishi kulingana na kipato chako ila usiwe bahili na kuogopa kufanya matumizi. Maisha ni matamu na yana vitu vingi vya kufurahia.”

Rafiki zake wakamshukuru na kwenda zao. Wengine walikuwa kimya kwa sababu haikuwaingia akilini na hawakuweza kuelewa. Wengine walidhihaki kwa kusema , “Mtu tajiri hivyo alitakiwa kugawana utajiri wake na rafiki zake wasio na kitu.” Lakini wengine walikuwa wamepata mwanga mpya. Walielewa kuwa, Aligamishi alirudi kwa Arkad mara nyingi sababu alikuwa anataka kumuona mtu akitoka gizani hadi kwenye mwanga. Mtu huyo alipopata mwanga fursa zilimsubiria, hakuna anayeweza kutumia fursa hizo mpaka afanye bidii kupata uelewa kwanza.

Hawa ndiyo ambao baadaye walikuwa wakimtembelea Arkad kila mwaka. Aliwashauri na kuwapa maarifa yake bure kama ambavyo watu wenye maarifa na busara nyingi hufanya. Pia aliwasaidia kuwekeza akiba zao ili wapate faida nzuri bila ya kuingia katika hatari ya kupoteza pesa zao wala kuingia kwenye uwekezaji usioleta faida. Maisha ya watu hawa

yalibadilika siku ile walipogundua ukweli uliotoka kwa Aligamishi kwenda kwa Arkad. Kutoka kwa Arkad hadi kwao.

Sehemu fulani ya pato unalopata ni yako.

TIBA SABA DHIDI YA POCHI TUPU

Ufahari wa Babiloni umesifika kwa vizazi vingi sana. Sifa zake za kuwa jiji tajiri kuliko yote na utajiri wake usio na kipimo zimesimuliwa vizazi na vizazi. Hata hivyo, jiji hili halikuibuka tu na kuwa tajiri. Utajiri wa Babiloni ulitokana na maarifa ya watu wake. Kwanza kabisa walijifunza jinsi ya kupata utajiri.

Mfalme Sargon wa Babiloni aliporudi baada ya kuwashinda Waelami, alikuta jiji lipo kwenye hali mbaya sana. Mshauri wa mfalme alimuelezea hali hiyo, alisema:

"Kwa miaka mingi kumekuwa na ukuaji wa uchumi na watu wamekuwa matajiri sababu ya wewe kujenga mifereji ya umwagiliaji na mahekalu makubwa ya Miungu. Sasa baada ya miradi hiyo kukamilika watu hawana kazi za kuwaingizia kipato.

"Wafanyakazi wamekaa tu. Wafanyabiashara hawana wateja. Wakulima hawana wa kumuuzia mazao yao, na raia hawana pesa za kutosha kununua chakula."

"Lakini pesa zote tulizotumia kwenye miradi ya serikali zimekwenda wapi?" Akahoji mfalme.

"Nina wasiwasi zimeishia mikononi mwa matajiri wachache. Zimepita mikononi mwa watu haraka kama vile

maziwa ya mbuzi yanavyopita kwenye chujio. Sasa mzunguko wa pesa umekuwa chini na watu wetu hawana cha kuonyesha kutokana na mapato yao."

Mfalme alifikiria kwa muda kidogo na kisha akasema. "Imekuwaje watu wachache wameweza kumiliki pesa nyingi kiasi hicho?"

"Kwa sababu wanajua jinsi ya kupata pesa," akajibu yule mshauri.

"Mtu anayejua jinsi ya kufanikiwa hawezi kulaumiwa akifanikiwa, na wala si haki kuchukua mali ya mtu aliyeipata kihalali na kuwapa wazembe."

"Lakini kwanini iko hivi?" Akahoji mfalme. "Kwanini watu wote hawajifunzi mbinu za kufanikiwa ili na wao wawe matajiri na kufanikiwa?"

"Mtukufu mfalme, hilo linawezekana, lakini ni nani atawafundisha? Hawawezi kuwa makuhani, hawajui chochote kuhusu mbinu za kutengeneza pesa."

"Sasa kwenye mji wetu ni nani anafahamu namna ya kuwa tajiri?" Akauliza mfalme.

"Hilo linajijibu lenyewe mtukufu mfalme, ni nani aliye tajiri kuliko wote hapa Babiloni?"

"Umenena vema mshauri wangu, ni Arkad. Ndiye mtu tajiri kuliko wote. Kesho mlete nionane naye."

Kesho ilipofika Arkad alifika mbele ya mfalme. "Arkad ni kweli kuwa wewe ndiye tajiri kuliko wote hapa Babiloni?"

"Na mimi nimesikia hivyo mtukufu mfalme na sijaona mtu wa kubisha."

“Umewezaje kuwa tajiri namna hiyo?”

“Kwa kutumia vizuri fursa zilizopo wazi kwa watu wote kwenye mji wetu huu.”

“Kwa hiyo hapo mwanzo hukuwa na utajiri wowote?”

“Sikuwa na chochote, sikuwa na kingine zaidi ya nia ya kuwa tajiri.”

“Sikiliza Arkad” akasema mfalme. “Mji wetu hauna furaha. Sababu kuu ni kuwa watu wachache ndiyo wanajua namna ya kuwa na utajiri na hawa wameuhodhi. Walio wengi hawana ujuzi wa kutunza pesa wanazopata. Ni nia yangu kufanya Babiloni kuwa mji tajiri zaidi duniani, unatakiwa kuwa mji wa matajiri. Kwa hiyo tunatakiwa kuwafundisha watu namna ya kupata utajiri. Hebu niambie Arkad, kuna siri ya namna ya kuwa tajiri? Watu wanaweza kufundishwa siri hiyo?”

“Inawezekana mtukufu mfalme. Kile mtu mmoja anachokijua inawezekana kufundishwa kwa wengine.”

“Arkad umeongea vitu nilivyotaka kusikia. Je unaweza kufanya hiyo kazi? Unaweza kufundisha hiyo elimu kwa wakufunzi, ambao nao watafundisha wengine mpaka kuwe na walimu wa kutosha kumfundisha kila raia wangu maarifa hayo?”

“Arkad akainama kwa heshima na kusema, “Mimi ni mtumishi wako, nitafanya kama ulivyoagiza. Maarifa yote niliyonayo nitayafundisha kwa ajili ya usitawi wa raia wenzangu na utukufu wa mfalme wangu. Ninaomba mshauri wako aniandalie darasa la watu mia moja, nami

nitawafundisha tiba saba zilizofanya niwe na pochi iliyotuna, pochi ambayo ilikuwa tupu kuliko zote katika Babiloni.”

Baada ya siku arobaini, na kama mfalme alivyoagiza, wale wateule mia moja walikuwa wamekusanyika kwenye ukumbi mkubwa ulio ndani ya Hekalu la Elimu. Walikuwa wamekaa kwenye nusu duara wakipendeza kwa mavazi yao ya rangi mbalimbali. Arkad likaa pembeni ya kiti kidogo ambacho juu yake chetezo cha kuabudia kilikuwa kikitoa moshi wenye harufu nzuri sana.

“Tazama mtu tajiri zaidi katika Babiloni,” alinong’ona mwanafunzi mmoja huku akimgusa mwenzake Arkad alipokuwa anasimama. “Ni mtu kama sisi tu!”

“Nikiwa kama mtumishi mtiifu wa mfalme wetu,” alianza kuongea Arkad. “Ninasimama mbele yenu kufanya kazi yake. Kwa sababu zamani nilikuwa kijana aliyetamani kuwa tajiri, na kwa sababu nilipata maarifa yaliyoniwezesha kuupata, ameniagiza niwafundishe maarifa niliyonayo.

“Utajiri wangu ulianzia chini sana. Sikuwa na cha ziada, nilikuwa kama nyinyi au raia wengine wa Babiloni.

“Sehemu kuu ya kutunza hazina yangu ilikuwa ni pochi yangu. Nilichukia jinsi ilivyokuwa tupu bila kazi yoyote. Nilitamani ijae na itune, ikilia kwa sauti za dhahabu zilizogongana ndani yake. hivyo nikatafuta tiba zote dhidi ya pochi tupu, nikapata tiba saba.

“Kwa nyinyi mliokusanyika hapa mbele yangu. Nitawafundisha tiba hizo saba na, hizo zinatakiwa kujulikana

na watu wote wanaotaka utajiri. Kila siku, kwa siku saba nitawafundisha moja ya tiba hizo.

"Msikilize kwa makini yale nitakayowafundisha. Mjadiliane kati yenu. Jifunzeni mambo haya kikamilifu ili hata kwenu yaweze kuweka mbegu ya utajiri kwenye pochi zenu. Mwanzo kila mmoja wenu atatakiwa kuanza kujenga utajiri wake. Mkiweza kufanikiwa hilo ndipo mtaweza kufundisha wengine.

"Nitawafundisha jinsi ya kutunisha pochi zenu kwa njia rahisi. Hii ndiyo ngazi ya kwanza kuelekea hekalu la utajiri. Hakuna mtu anaweza kupanda ngazi kama hawezi kuweka mguu wake kwenye ngazi ya kwanza.

"Sasa na tuone tiba ya kwanza."

TIBA YA KWANZA

Anza kutunisha pochi yako.

Arkad alianza kwa kuongea na mtu aliyekaa mstari wa pili, aliyeonekana yuko makini sana. "Rafiki yangu, unafanya kazi gani?"

"Mimi ni muandishi wa kumbukumbu kwenye mabamba ya vigae." Alijibu mtu yule.

"Hata mimi kazi hiyo ndiyo iliyonipatia pesa zangu za kwanza. Una fursa kama yangu ya kujenga utajiri."

Kisha akaongea na mtu aliyekuwa na uso mwekundumwekundu, aliyekuwa amekaa siti ya nyuma.

"Ndugu tuambie, unapataje mkate wako wa kila siku?"

“Mimi nauza nyama. Nanunua mbuzi toka kwa wafugaji, nawachinja na kuuza nyama. Ngozi huwa nawauzia watengeneza viatu.”

“Sababu na wewe una kazi na kipato, nawe pia una fursa ya kufanikiwa kama mimi.”

Arkad aliuliza kazi ya kila mmoja wao. Alipomaliza alisema:

“Mnaweza kuona kuwa, kuna kazi nyingi za kufanya ili kujipatia kipato. Kila njia ya kujipatia kipato ni kijito cha dhahabu ambacho kinaingia kwenye pochi. Kwahiyo, kwenye kila pochi ya mmoja wenu kuna kijito cha pesa kinachotiririka. Wengine kwa wingi na wengine kwa uchache kulingana na uwezo wa kila mtu, si ndivyo ilivyo? Hapo walikubaliana naye kuwa asemayo ni kweli.

Hivyo Arkad akaendelea “Iwapo kila mmoja wenu atakuwa na nia ya kuwa tajiri, je, si busara kutumia chanzo cha utajiri ambacho tayari anacho?”

Hili nalo wakakubaliana naye.

Hapo Arkad akamgeukia mtu mmoja mnyenyekevu aliyejitambulisha kuwa anafanya biashara ya mayai. “Mfano ukichukua kikapu kimoja na kuweka humo mayai kumi kila siku asubuhi na kila jioni ukatoa mayai tisa, nini kitatokea?”

“Baada ya muda kikapu kitajaa kupita kiasi.” Akajibu muuza mayai.

“Kwa nini?”

“Kwa sababu kila siku naweka yai moja zaidi ya ninayotoa.”

Arkad aliligeukia darasa huku akitabasamu. “Kuna mtu hapa ana pochi tupu?”

Kwanza wanafunzi walionyeshwa kushangazwa, kisha wakacheka na mwishowe wakapunga pochi zao hewani kwa pamoja.

“Sawa!” Akaendelea Arkad.”Sasa nitawaambia tiba ya kwanza ya pochi tupu. Fanyeni kama nilivyo mshauri muuza mayai. Kila ukiweka sarafu kumi kwenye pochi basi chukua tisa tu kwa matumizi yako. Pochi yako itaanza kutuna mara moja. Uzito wa pochi yako utakuwa mzuri mikononi mwako, utakuburudisha moyoni.

“Usidharau kitu nisemacho kwa sababu kinaonekana ni rahisi. Mara zote ukweli huwa rahisi. Niliwaambia kuwa nitawaeleza niliwezaje kuwa tajiri, hivyo ndivyo nilivyoanza. Mimi mwenyewe nilikuwa na pochi tupu na niliichukia kwa sababu haikuwa na kitu chochote cha maana. Lakini nilivyoanza kuweka kumi na kutoa tisa, ilianza kutuna. Nanyi itakuwa hivyohivyo.

“Sasa niwaambie kitu cha ajabu kilichonitokea na mpaka sasa sikielewi. Nilipoacha kutumia zaidi ya tisa ya kumi ya pato langu niliishi kama zamani tu, sikupungukiwa chochote. Pia cha kushangaza zaidi, nikaanza kupata pesa kirahisi kuliko mwanzo. Bila shaka ni sheria za Miungu kumpa pesa kirahisi yule anayetunza sehemu ya pato lake. Yule mwenye mifuko mitupu pesa humuepuka.

“Ni kitu gani unatamani sana? Kutimiza matamanio ya kila siku. Vito, nguo nzuri, chakula kingi, vitu ambavyo

vinakuja na kupita. Au vitu vya kudumu, dhahabu, ardhi, mifugo na uwekezaji wenye kuingiza pesa? Pesa unayotoa kwenye pochi yako huleta hivyo vitu vya kwanza. Pesa unayoiacha kwenye pochi huleta hivyo vitu vya pili.

"Hii ndiyo tiba niliyoigundua: *'kwa kila sarafu kumi nilizoweka kwenye pochi, nilitumia tisa tu'* jadilianeni kuhusu hili, kama kuna mtu anaona halina ukweli basi kesho tukionana tena aniambie."

TIBA YA PILI

Pangilia matumizi yako.

"Wengine kati yenu wameuliza: mtu anawezaje kutunza moja ya kumi ya pato lake wakati pato lote analopata halitoshi kwaajili ya matumizi yake ya lazima?" Hivyo ndivyo Arkad alianza kuongea kwenye siku ya pili.

"Jana ni wangapi kati yenu walikuwa na pochi tupu?"

"Wote," darasa lilijibu.

"Lakini si kwamba wote mnapata kipato sawa. Wengine hupata zaidi na wengine wana familia kubwa. Lakini wote pochi zenu zilikuwa tupu. Sasa nitawaambia jambo la kushangaza kuhusu watu. Ni hivi; kile ambacho tunaita 'matumizi ya lazima' mara zote hukua kulingana na kipato chetu kinavyokua, isipokuwa tu tukijizuia.

"Usichanganye matumizi ya lazima na matamanio. Wote hapa na familia zenu mna matamanio mengi kuliko mnayoweza kutimiza. Kwa hiyo, mnaendelea kuyatimiza

kadri kipato chenu kinavyoongezeka. Lakini bado mengi yanabaki bila kutimizwa.

“Watu wote wamelemewa na matamanio mengi kuliko wanayoweza kuyatimiza. Mnafikiri sababu ya utajiri wangu basi naweza kutimiza matamanio yangu yote? Si kweli. Kuna kikomo cha nguvu zangu. Kikomo cha umbali ninaoweza kusafiri. Kikomo cha ninachoweza kula na kikomo cha mambo ninayoweza kufurahia.

“Kama ambavyo magugu hukua sehemu ambazo mkulima kaacha nafasi kwa mizizi yake kushika, ndivyo matamanio hukua kwa mtu anayetamani kuyatimiza. Matamanio yenu ni mengi lakini mnayoweza kuyatimiza ni machache.

“Chunguzeni kwa makini namna mnavyoishi. Mtakuta mna matumizi mengi yasiyo ya lazima, matumizi ambayo mnaweza kuyapunguza au kuyaacha kabisa. Acha kaulimbiu yenu iwe kupata asilimia mia moja ya thamani mnapofanya matumizi.

“Kila mmoja aandike vitu alivyopanga kutumia pesa. Kisha chagua yale matumizi ya muhimu, yale tu yanayowezekana kwa kutumia tisa ya kumi ya pato lako. Tupilia mbali mengine yote na yaone ni kama matamanio ambayo hayana umuhimu wa kuyatimiza.

“Panga matumizi yako. Usiguse ile moja ya kumi ya kutunishia pochi yako. Kutunza pesa liwe ndiyo tamanio lako kuu. Panga bajeti yako kwa uangalifu mkubwa. Acha ikusaidie katika kutunisha pochi yako.

Hapo mwanafunzi mmoja aliyekuwa na vazi la rangi nyekundu na dhahabu, akasimama na kusema, “Mimi ni mtu huru. Nafikiri kuwa nina haki ya kufurahia vitu vizuri maishani. Naona kama kupanga matumizi na kuishi kwa bajeti inayonipangia kiasi cha kutumia na kwa matumizi gani ni utumwa. Naona hilo litaharibu furaha yangu maishani na kunifanya niishi kama punda mbeba mizigo tu.”

Arkad akamjibu, “Rafiki, ni nani atapanga bajeti yako?”

“Nitapanga mimi mwenyewe,” akajibu yule bwana.

“Kama ni hivyo, unafikiri punda mbeba mizigo akiambiwa apange pajeti ya mizigo yake atabeba vito, mazuria na dhahabu? Hapana, ataweka nyasi, nafaka na mfuko wa maji kwaajili ya safari ya jangwani.

“Lengo la bajeti ni kutunisha pochi yako. Inakusaidia kupata mahitaji yako ya muhimu na kutimiza matamanio mengine iwapo inawezekana. Inakusaidia kutofautisha mahitaji ya muhimu na matamanio tu. Kama mwanga ndani ya pango lenye giza totoro. Bajeti inakusaidia kuona tobo kwenye pochi yako. Inakusaidia pia kuliziba na kupanga vizuri matumizi kwa mambo ya msingi na starehe.

“Hii ndiyo tiba ya pili kwa pochi iliyo tupu. *Panga matumizi yako hadi uwe na pesa ya matumizi ya lazima , na pesa ya starehe bila kutumia zaidi ya tisa ya kumi ya pato lako.”*

TIBA YA TATU

Fanya dhahabu zako ziongezeke.

“Tazama pochi yako imeanza kutuna! Umekuwa na nidhamu ya kutunza moja ya kumi ya pato lako. Umepanga matumizi yako vizuri na umelinda akiba yako. Hatua inayofuata tutajifunza namna ya kufanya hazina yako kufanya kazi na kukua zaidi. Pesa kwenye pochi ni kitu cha kuridhisha lakini haizalishi kitu chochote. Pesa tuliyopata kwa kutunza ni mwanzo tu. Mapato itakayozalishandiyo yatayojenga utajiri wetu. " Hivyo ndivyo alivyoanza Arkad kwenye siku ya tatu.

“Jinsi gani tunaweza fanya pesa zetu zifanye kazi? Uwekezaji wangu wa kwanza haukuwa mzuri. Nilipoteza pesa zote. Nitasimulia hilo baadaye. Uwekezaji wangu wa kwanza ulioleta faida ulikuwa ni mkopo niliompa Aggar, mtengeneza ngao. Alikuwa akinunua shaba kwaajili ya kutengeneza ngao, lakini alikuwa hana mtaji wa kutosha hivyo alikuwa akikopa kwa wenye pesa. Alikuwa ni mtu muaminifu, alilipa mikopo yake na riba vizuri mara tu alipouza ngao.

“Kila mara nilipomkopesha, nilimkopesha na ile riba aliyonilipa. Kwa hiyo mtaji wangu uliongezeka na mapato yangu yakaongezeka pia. Lilikuwa jambo la kuburudisha sana kuona pesa zile zikiingia kwenye pochi yangu.

“Nisikilizeni kwa makini.’

‘‘Utajiri wa mtu haupo kwenye fedha zilizopo kwenye pochi yake, bali kwenye kijito cha dhahabu kinachotiririka kwenda kwenye pochi yake na kuitunisha. Kipato kinachoingia hata akisafiri au asipofanya kazi.

“Nimeweza kupata pesa nyingi sana hadi kufikia kuitwa mtu tajiri zaidi. Mkopo wangu kwa Aggar ulikuwa ni somo

langu la kwanza juu ya uwekezaji wenye faida. Kutokana na uzoefu nilioupata hapa nikatanua uwekezaji wangu kadri mtaji ulivyokuwa ukiongezeka. Nilianza na kidogo, lakini baada ya muda kikawa kikubwa. Utajiri ulimiminika kwenye pochi yangu.

"Tazama! Kutoka kwenye mapato yangu kidogo nilipata umati wa watumwa ambao walifanya kazi ya kuzalisha zaidi. Watoto wao walinitumikia na watoto wa watoto wao nao walinitumikia. Jumla ya pato walilozalisha ilikuwa kubwa sana.

"Dhahabu hukua kwa kasi iwapo inazalisha, kama tu mtakavyoona kwenye mfano ufuatao.

"Kulikuwa na mkulima ambaye mtoto wake wa kwanza alipozaliwa, alichukua vipande kumi vya fedha na kwenda kwa mkopesha pesa. Akamwambia aweke ile pesa kwa riba mpaka mtoto wake atakapotimiza miaka ishirini. Mkopesha pesa akakubali, na wakakubaliana kuwa riba itakuwa moja ya nne ya ile pesa kila baada ya miaka minne. Mkulima akasema, kwa sababu ile pesa ni kwaajili ya kijana wake basi hata ile riba iongezwe kwenye mtaji.

"Kijana wake alipofikisha miaka ishirini, mkulima akaenda tena kwa mkopesha pesa kuuliza kuhusu fedha alizoweka. Mkopeshaji akamwambia kuwa kwa sababu pesa ilikuwa ikiongezeka kwa riba inayobadilika kulingana na muda, vile vipande kumi vya fedha sasa vimekuwa thelathini na moja na nusu.

“Mkulima akafurahi sana, na kwa sababu kwa wakati huo kijana wake hakuhitaji fedha zile akaziacha kwa mkopeshaji. Mtoto wake alipofika miaka hamsini, wakati huo mkulima yule tayari akiwa ameshafariki, mkopeshaji akamlipa mtoto wake vipande mia moja na sitini na saba vya fedha.

“Kwa miaka hamsini, uwekezaji ulikuwa umekua karibia mara kumi na saba.

“Hii ndiyo tiba ya tatu ya pochi tupu: *Fanya fedha yako ifanye kazi na ijizalishe kama mnyama wa kufugwa. Ilete kipato ambacho kitatiririka kwenye pochi yako daima.*

TIBA YA NNE

Linda hazina yako isipotee.

“Bahati mbaya hupendelea sehemu inayong’ara. Dhahabu ndani ya pochi inatakiwa kulindwa kwa nguvu zote, vinginevyo itapotea. Kwa hiyo ni busara kuanza na kiasi kidogo, tukiweza kumudu kukiendesha na kukilinda ndipo Miungu itatuamini na kutupatia kikubwa zaidi.” Alisema hayo Arkad katika siku ya nne.

“Kila mtu mwenye pesa hushawishika na fursa za kuwekeza kwenye uwekezaji unaodaiwa kuwa na faida kubwa sana. Mara nyingi hushawishiwa na ndugu na marafiki ambao tayari wamo humo.

“Kanuni ya kwanza ya uwekezaji ni usalama wa mtaji wako. Je, ni busara kufuatilia faida kubwa huku ukihatarisha mtaji wako? Hapana, adhabu ya kutochukua tahadhari ni

hasara. Chunguza kwa makini kabla haujatumia hazina yako. Hakikisha hata mambo yakienda kombo bado mtaji wako utakuwa salama. Usidanganyike na ndoto za kuwa tajiri haraka.

“Kabla hujamkopesha mtu hakikisha kama anaweza kulipa na ana sifa hiyo. Usije ukatoa kama zawadi mali uliyoitafuta kwa jasho.

“Kabla hujawekeza kwenye mradi wowote hakikisha unajua mapungufu na hatari za huo mradi.

“Uwekezaji wangu wa kwanza ulikuwa wa hovyo sana. Pesa niliyotunza kwa mwaka mzima nilimpatia Azmur mfyatua matofali. Alisafiri nchi za mbali hadi jiji la Tiro, aliahidi kununua vito kwa Wafoenike. Ilikuwa tuviuze na kugawana faida. Wafoenike walimtapeli na kumuuzia vioo. Hazina yangu ilipotea. Leo, uzoefu wangu unaniambia ubaya wa kumuamini mfyatua matofali kwenye masuala ya vito.

“Kutokana na uzoefu wangu, nimejifunza kuwa: usiamini uelewa wako kupita kiasi na ukaishia kuwekeza hazina yako kwenye mradi mbaya. Ni bora kupata ushauri wa wenye uzoefu wa kuwekeza kwa faida. Kawaida ushauri kama huo hutolewa bure kwa wanaouliza, na una thamani sawa tu na kiwango unachotaka kuwekeza sababu unakiokoa kiwango hicho kisipotee.

“Hii ndiyo tiba ya nne ya pochi tupu. Hii ni ya muhimu sababu inalinda pochi iliyotuna isiwe tupu tena. *Linda hazina yako kwa kuwekeza kwenye miradi ambayomtaji wako utakuwa salama. Wekeza kwenye Miradi ambayo inaleta faida siku zote.*

Omba ushauri kwa wenye uelewa, na tumia ushauri wa watu wenye uzoefu wa kuwekeza kwa faida. Acha maarifa yao yalinde hazina yako dhidi ya uwekezaji mbaya."

TIBA YA TANO

Fanya makazi yako kuwa uwekezaji wenye faida.

"Iwapo mtu anatumia tisa ya kumi ya pato lake kwa mahitaji ya msingi na kufurahia maisha, na iwapo sehemu ya hii fedha anaweza kufanya uwekezaji wenye kuleta faida bila kuathiri maisha yake, hazina yake itakuwa kwa kasi sana." Hivyo ndivyo alivyoanza kuongea Arkad kwenye siku ya tano.

"Watu wengi hapa Babiloni hutunza familia zao kwenye nyumba za mbavu za mbwa na zilizo sehemu mbaya kabisa. Nyumba zisizofaa watu kuishi. Huko wanawalipa wenye nyumba kodi kubwa kwa nyumba ambazo hata nafasi ya kupanda maua ya kufurahisha moyo hakuna. Watoto wao hawana hata sehemu ya kucheza bali hucheza kwenye vichochoro vichafu.

"Hakuna familia inayoweza kufurahia maisha bila ya watoto kuwa na sehemu safi ya kucheza, na eneo ambalo mke anaweza kupanda si tu maua, bali pia mbogamboga kwa ajili ya familia yake.

"Inafurahisha mtu kula matunda kutoka kwenye mti wake, na zabibu za bustani yake, kumiliki makazi yake na

kujivunia sehemu yake. Hilo litamfanya ajiamini na aweze kutimiza malengo yake mengine kwa moyo mmoja.

“Hivyo, napendekeza kila mtu amiliki nyumba kwaajili yake na familia yake.

“Kumiliki nyumba si jambo lisilowezekana kwa wale walio na nia. Je, mfalme wetu hajatanua kuta za Babeli ili kuwe na eneo kubwa, na sasa mtu anaweza kununua kiwanja kwa bei nafuu?

“Pia niwaeleze kitu kingine, wakopesha pesa hutafuta watu wanaokopa kwaajili ya kununua ardhi na ujenzi wa nyumba. Watakukopesha haraka ili umlipe mfyatua tofali na mjenzi, utahitaji tu kuonyesha kiasi kidogo ulichotenga kwaajili ya kazi hiyo.

“Ukishajenga nyumba unaweza kumlipa mkopeshaji kama ulivyokuwa unamlipa mwenye nyumba. Kila unaporejesha unakuwa unapunguza deni, na baada ya miaka michache unakuwa umemaliza.

“Hapo utafurahi kuwa na nyumba yako mwenyewe, na hutadaiwa na mtu zaidi ya kodi ya mfalme tu.

“Pia mkeo akienda mtoni kufua anaweza kurudi na maji ya kumwagilia bustani. Baraka nyingi huja kwa mtu anayemiliki nyumba yake mwenyewe. Pia hili hupunguza sana gharama za maisha. Pesa nyingi hubaki kwaajili ya kustarehe na kutimiza matamanio mengine. Hii ndiyo tiba ya tano ya pochi iliyo tupu.

Miliki nyumba yako mwenyewe.

TIBA YA SITA

Jihakikishie kipato cha wakati ujao.

“Maisha ya kila mmoja huanzia utotoni hadi uzeeni. Hii ni njia ya maisha na mtu hawezi kuiepa isipokuwa Miungu imemuita mapema. Hivyo ninasema kuwa; ni muhimu kwa mtu kufanya maandalizi ili wakati ujao awe na kipato. Kipindi ambacho hatakuwa kijana tena. Pia anatakiwa kuweka maandalizi kwaajili ya familia yake ili isihangaike ikitokea Miungu imemuita mapema. Kwa hiyo nasema kuwa ni jambo la muhimu kwa mtu kufanya maandalizi ili aje kuwa na kipato uzeeni, nyakati ambazo hatakuwa kijana tena. Na pia kufanya maandalizi kwaajili ya familia yake iwapo atafariki. Somo hili linafundisha kuhakikisha pochi yako imetuna hata wakati ambapo huwezi kufanya kazi ya kuingiza kipato. Hivyo ndivyo alivyoanza kusema Arkad katika siku ya sita.

“Mtu ambaye anajua kanuni za utajiri, na akaweza kujipatia utajiri ni muhimu akafikiria kuhusu wakati ujao. Anatakiwa kuwekeza kwenye miradi ambayo ni salama na inadumu kwa miaka mingi. Lakini mapato kutokana na miradi hiyo yanatakiwa kupatikana kirahisi mara yatakapohitajika.

“Kuna njia nyingi ambazo mtu anaweza kuhakikisha kuwa wakati ujao atakuwa salama. Anaweza kuwa na sehemu ya siri na kufukia hazina yake hapo. Lakini hata afiche namna gani lazima siku moja wezi wataipata. Kwa hiyo sishauri kufanya hivyo.

“Mtu anaweza kununua nyumba au ardhi kwaajili ya wakati ujao. Kama amechagua vizuri, na kuna uwezekano wa kupanda thamani huko mbeleni, hivi ni vitu vyenye thamani ya kudumu. Mapato yake au mapato kutokana na kuviuza yanaweza kufaa kwa ajili ya wakati ujao.

“Pia anaweza kukopesha pesa zake huku akiziongeza mara kwa mara. Riba inayoongezwa kwenye pesa hiyo itafanya pesa yake ikue haraka sana. Binafsi namfahamu mtengenezaji wa makubazi mmoja anayeitwa Ansam. Ansam aliniambia kuwa kila wiki huweka vipande viwili vya fedha kwa mkopesha pesa. Amekuwa anafanya hivyo kwa muda wa miaka minne sasa. Hivi karibuni ameenda kuona akiba yake na imemfurahisha sana. Pesa yake, ukichanganya na riba ya moja ya nne kwa kila miaka mine, imefikia jumla ya vipande elfu moja na arobaini vya fedha.

“Kwa ujuzi wangu wa masuala ya fedha nilimhamasisha kuendelea kuweka kwa kumuonyesha kuwa; akiendelea hivyo kwa miaka kumi na miwili mingine atakuwa anamdai mkopesha pesa vipande elfu nne vya fedha. Kiasi kitakachomtosha maisha yake yote.

“Kiasi kidogo hivyo kikiwekezwa kwa ukawaida huwa kikubwa sana. Hakuna mtu ambaye hawezi kuweka akiba

kwaajili ya uzee wake, au kwaajili ya wakati ujao wa familia yake. Hilo halijalishi biashara yake ni kubwa kiasi gani au ana miradi gani.

"Nategemea siku moja watu wenye akili watabuni bima ya kifo. Watu wengi waweke pesa kidogokidogo, na kisha mmoja wao anapokufa basi familia yake wapewe kiasi fulani. Hili naona kama litakuwa jambo zuri na napendekeza lifanyike. Lakini hili kwa sasa ni gumu kufanyika kwa sababu ni jambo linalofanyika baada ya ya maisha ya mtu, au nje ya ushirika wowote wa kibiashara. Ili ufanye kazi unatakiwa kuwa imara kama kiti cha ufalme. Lakini siku moja nafikiri hilo litawezekana na kuleta baraka kwa watu wengi. Hata pesa ndogo iliyowekezwa itafanya familia ya marehemu kulipwa pesa ya kutosha.

"Lakini kwa sababu tunaishi katika siku hizi, basi tunatakiwa kutumia njia zilizopo. Kwa hiyo basi; nashauri watu wote kutumia njia zilizothibitika kuwa ni bora ili kujiandaa kwa ajili ya miaka ya uzeeni. Mtu asiye na kitu na hawezi kufanya kazi au familia iliyoondokewa na kichwa cha familia na kuachwa bila kitu ni janga kubwa sana.

Hii ndiyo tiba ya sita; *Hakikisha una kipato kwajili ya uzee wako, na kwaajili ya ulinzi wa familia yako.*

TIBA YA SABA

Ongeza pato lako.

“Leo nitazungumza moja ya tibamuhimu kabisa ya pochi iliyo tupu. Sitazungumza kuhusu fedha bali nitazungumza kuhusu nyinyi. Nitaongea kuhusu nyinyi mliokaa hapa mbele yangu mkiwa na mavazi ya kuvutia. Nitazungumza juu ya vitu ambavyo vipo katika akili na maisha ya watu na kukwamisha mafanikio yao.” Hivyo ndivyo alivyoanza kuongea Arkad kwenye siku ya saba.

“Siku si nyingi zilizopita alikuja kwangu kijana mmoja akiomba mkopo. Nilipomuuliza anataka kwaajili ya nini, akasema kuwa pato lake halitoshi kulipia mahitaji yake. Hilo lilifanya wakopesha pesa wasiweze kumkopesha kwa kuwa hakuwa na kipato cha ziada cha kumuwezesha kulipa mkopo.

“Nilimwambia, ‘unachotakiwa kufanya, ni kuongeza kipato. Umefanya jambo gani ili kujiongezea kipato?’

“‘Nimefanya kila njia,’ alijibu. ‘Mara sita kwa muda wa miezi miwili nimemfuata muajiri wangu na kuomba nyongeza ya mshahara bila mafanikio. Siwezi kwenda zaidi. Hakuna mtu anaweza kwenda zaidi ya hapo.’

“Tunaweza kucheka na kumuona ni mzembe, lakini alionyesha jambo muhimu linalohitajika ili kujiongezea kipato. Ndani yake alikuwa na nia ya kujiongezea kipato. Nia yenye nguvu.

“Nia inaanza kisha mafanikio hufuata. Nia yako inatakiwa kuwa yenye nguvu na yenye lengo. Nia ya jumla ni dhaifu na ni kama matamanio tu ya kupoteza wakati. Kutamani tu kuwa tajiri hakutakufikisha popote. Ila kutamani kupata vipande

vitano vya dhahabu ni kitu kinachoeleweka na kinaweza fanyiwa kazi hadi kikatimizwa.

“Hapo unaweza kutafuta njia ya kupata vipande kumi, kisha ishirini na baadaye vipande elfu moja. Kuja kutazama, umeshakuwa tajiri! Baada ya kujifunza kutimiza malengo madogo unakuwa umepata uzoefu wa kukuwezesha kutimiza malengo makubwa. Hivi ndivyo utajiri unavyopatikana. Kwanza kwa kuweza kumudu kiasi kidogo na baadaye kiasi kikubwa kadri unavyoongeza uwezo.

“Lengo linatakiwa kuwa rahisi na linaloeleweka. Inakuwa haina maana ya kuwa na malengo iwapo ni mengi, hayaeleweki na yapo juu ya uwezo wa mtu kuyatimiza.”

“Kadri mtu anavyotimiza malengo yake ndivyo uwezo wake wa kuongeza kipato unavyoongezeka. Kipindi kile nilipokuwa muandishi, niligundua kwamba wafanyakazi wengine walifanya zaidi na kupata zaidi. Hilo lilifanya niweke lengo la kutozidiwa na yeyote. Haikuchukua muda nikajua siri ya kufanikiwa kwao. Kuipenda kazi, kufanya kazi kwa umakini na kuwa mvumilivu. Baada ya muda ni watu wachache tu ndiyo walioweza kuandika mabamba mengi kuliko mimi. Bila kuchelewa, ujuzi wangu ulianza kunipa faida haraka. Wala hakukuwa na ulazima wa kwenda kwa bosi wangu mara sita ili anitambue.

“Kadri tunavyoongeza maarifa ndivyo tutakavyoongeza kipato chetu. Mtu anayejitahidi kuijua kazi yake vizuri atapata mafanikio zaidi. Kama ni fundi sanaa basi anatakiwa kujua mbinu za mafundi bora kabisa wa sanaa. Kama ni

mwanasheria au ni mganga, basi anatakiwa kuomba ushauri na kubadilishana ujuzi na watu walio kwenye nyanja yake. Kama ni mfanyabiashara, inampasa kuendelea kutafuta bidhaa bora ambazo zina bei ya chini.

"Maisha ya mwanadamu hubadilika na kuwa bora sababu ya watu wenye udadisi na wenye kutafuta ujuzi kwa faida ya wote. Nawahimiza watu wote kuwa mstari wa mbele wa maendeleo, na si kukaa kizembe na kuachwa nyuma. Pia mtu anayejiheshimu anatakiwa kufanya mambo kama haya yafuatayo:

"Anatakiwa kulipa madeni yake haraka iwezekanavyo, hatakiwi kununua kitu asichoweza kumudu. Anatakiwa kujali familia yake, hilo litafanya imheshimu na imuongelee vyema.

"Anatakiwa kuacha wosia kwa maandishi ili siku akifa mali yake igawanywe kwa utaratibu.

"Anatakiwa kuwa na huruma kwa wagonjwa, wasiojiweza na wale waliopatwa na majanga. Awasaidie kulingana na uwezo wake. Anatakiwa kuwa mkarimu kwa wapendwa wake.

"Kwa hiyo, tiba ya saba na ya mwisho ya kutibu pochi iliyo tupu ni kuwa mtu bora. Kujifunza na kujizoeza kupata maarifa zaidi, kupata ujuzi zaidi na kujiendesha kwa heshima. Hapo unaweza kujiamini na utaweza kutimiza malengo yako.

"Hizi ndizo tiba saba za pochi tupu. Kutokana na maisha yangu marefu yenye mafanikio, nawahimiza watu wote wanaotamani utajiri kuwa.

“Kuna dhahabu nyingi ndani ya Babiloni kuliko mnavyodhania. Nyingi za kutosha kila mtu.

“Nendeni mfanyie kazi mambo niliyowaambia nanyi mtafanikiwa kuwa matajiri.

“Nendeni mkafundishe ukweli huu kwa raia wote wa mfalme ili nao washiriki utajiri wa jiji letu kuu.”

KUTANA NA MUNGU WA BAHATI

Kama mtu ana bahati, huwezi jua inapoishia. Mtupe ndani ya mto Efrati naye atatoka ameshika lulu.

–Methali ya wababiloni

Kila mtu anatamani kuwa na bahati njema. Katika Babiloni tamaa hiyo ina nguvu leo kama tu ilivyokuwa miaka elfu moja iliyopita. Wote tuna matumaini ya kutembelewa na Mungu wa bahati njema. Je, kuna njia ya kumvuta atutembelee? Siyo tu atuone bali atupatie bahati pia.

Je, kuna njia ya kufanya mtu awe na bahati?

Hili ndilo watu wa kale wa Babiloni walitaka kujua. Na ndilo jambo waliloamua kulichunguza. Walikuwa ni watu wenye hekima na wenye kufikiri kwa makini. Kitendo cha mji wao kuwa tajiri kuliko yote ni ushahidi wa hilo.

Zamani hizo hawakuwa na shule wala vyuo, lakini walikuwa na sehemu ya kujifunzia na walipata elimu yenye kufaa sana. Katika majengo makubwa ya Babiloni kulikuwa na moja lililolingana kwa umuhimu na ikulu ya mfalme, bustani zilizoning'inia na mahekalu ya Miungu. Lakini si rahisi kulikuta jingo hilo limetajwa kwenye vitabu vya

historia, na mara nyingi halitajwi kabisa. Pamoja na hilo, jengo hili lilikuwa na ushawishi mkubwa sana wakati ule. Jengo hili ni Hekalu la Elimu. Humo maarifa ya kale yalifundishwa na walimu wa kujitolea, na mambo yahusuyo jamii yalijadiliwa kwa uwazi. Ndani ya jengo hili watu wote walikuwa sawa. Mtumwa wa hali ya chini aliweza kubishana vikali na mwana mfalme.

Mmoja wa watu waliopenda kutembelea Hekalu la Elimu alikuwa ni mtu mmoja tajiri sana aliyeitwa Arkad. Ilisemwa ndiye mtu tajiri zaidi katika Babeli. Alipendelea kuingia kwenye ukumbi mmoja, humu kundi kubwa la watu lilikusanyika kila jioni. Wengine wazee na wengine vijana lakini wengi walikuwa watu wa umri wa kati. Walikusanyika wakijadiliana na kubishana kuhusu mambo yaliyowahusu. Hebu tufanye kama tunawasikia tuone kama wanajua mbinu za kuvuta bahati.

Jioni ya leo jua lilikuwa kama mpira mwekundu, likimulika kwa shida kupitia vumbi la jangwani lililojaa angani. Huu ndiyo muda ambao Arkad alikuwa anaingia ukumbini. Tayari watu wanne walikuwa wameshafika. Walikuwa wamekaa kwenye mazuria madogo sakafuni. Wengine wengi walikuwa wakiwasili.

“Tutajadili nini usiku wa leo?” Aliuliza Arkad.

Baada ya kimya kifupi, mtu mmoja mrefu ambaye alikuwa ni mshona nguo akasema huku akisimama kama ilivyo desturi.

“Nina jambo ambalo ningependa lijadiliwe ila nasita kulisema, lisije onekana ni la kijinga mbele yenu.”

Baada ya kutiwa moyo na Arkad na wale wengine kulisema, akasema: “Leo nilikuwa na bahati, niliokota pochi iliyokuwa na vipande vya dhahabu ndani. Napenda niendelee kuwa na bahati. Nadhani kila mtu anatamani hivyo, kwa hiyo napendekeza leo tujadili jinsi ya kuvuta bahati. Pengine tunaweza kujua mbinu za kuivuta.”

“Hiyo ni mada nzuri sana,” akasema Arkad. “Inafaa kujadiliwa. Kwa watu wengine bahati ni kama ajali tu. Inatokea bila sababu wala lengo lolote. Wengine wanaamini mletaji wa bahati njema ni Mungu wetu mwenye vitu tele, Ashtar. Inasemwa kuwa tamaa yake ni kuwatunza wale wamfurahishao. Tujadili suala hili rafiki zangu. Mnasemaje, tuchunguze iwapo kuna njia ya kuweza kuvuta bahati?”

“Ndiyo! Ndiyo! Tuchunguze! Lilijibu lile kundi kwa shauku.

Arkad akaendelea. “Kuanza mjadala wetu, kwanza tusikie kutoka kwa wale ambao wamewahi kukutana na kitu kilichomkuta mshona nguo. Kupata au kupokea kitu cha thamani bila ya kutumia jitihada zozote.”

Kulikuwa na ukimya, kila mmoja akitegea labda kuna mtu atasema lakini hakuna aliyesema.

“Hakuna hata mmoja?” Akasema Arkad. “Basi bahati ni kitu adimu sana. Nani atoe muongozo wa jinsi ya kuanza uchunguzi wetu?”

“Ngoja nianze,” akaongea kijana fulani aliyekuwa kavalia nadhifu huku akisimama. “Mtu anapoongelea kuhusu bahati si moja kwa moja anakuwa anazungumza kuhusiana na kucheza kamari? Si huko ndiko tunapata watu wakijitahidi kumfurahisha Mungu wa bahati wakitegemea atawabariki kwa ushindi?”

Alipotaka kukaa akasikia sauti ikisema, “Usikae, endelea kutueleza. Je, wewe umewahi barikiwa na Mungu wa bahati wakati wa kucheza kamari? Je aligeuza kete na kufanya upande wenye rangi nyekundu kuwa juu na kujaza mifuko yako na kumpa hasara mchezesha kamari? Au aliruhusu rangi ya bluu kuwa juu na kufanya mchezeshaji kuchukua fedha yako uliyoitolea jasho?”

Yule kijana akacheka kama wengine walivyocheka kisha akajibu.

“Naomba nikiri kuwa ilionekana Mungu wa bahati hata hajui kama nipo pale. Vipi kuhusu nyinyi? Mmewahi mkuta akiwasubiri na akigeuza kete

Ili mshinde? Tuna shauku ya kujifunza.”

“Mwanzo mzuri,” hatimaye akasema Arkad. “Hapa huwa tunakutana kuangalia pande zote za mada. Kutoacha kuongelea kamari itakuwa ni kudharau kitu ambacho watu wanakifanya kila siku. Kupenda kutumia fedha kidogo kwa matumaini ya kupata kiasi kikubwa.”

“Hilo limenikumbusha mashindano ya farasi, tena jana tu nilikuwa huko,” akasema mtu mmoja kutoka kwa wasikilizaji.

“Ikiwa Mungu wa bahati hutembelea sehemu za kamari, bila shaka atakuwa anatembelea na mashindano farasi. Kwanza farasi na magari yao huvutia zaidi. Hebu tuambie Arkad, jana Mungu wa bahati alikunong’oneza kuweka pesa zako juu ya wale farasi wa kijivu kutoka Ninawi? Nilisimama nyuma yako na sikuamini masikio yangu niliposikia ukiweka pesa zako kwa wale farasi. Sote tunaelewa kuwa farasi kutoka Ashuru hawawezi kuwashinda farasi wetu mashindanoni.

“Je, ni Mungu alikuambia uweke fedha zako kwa wale farasi wa Ninawi, maana mwishoni kabisa farasi weusi walijikwaa na kuzuia farasi wetu kusonga na kufanya wale wa Ninawi washinde?”

Arkad akatabasamu baada ya kusikia maneno yale. “Tuna sababu gani ya kufikiria kuwa Miungu inatilia maanani watu wanaocheza kamari za farasi? Mi najua Ashtar ni Mungu wa upendo ambaye anafurahi kusaidia wale wenye uhitaji, na kuwabariki wanaostahili. Hapatikani kwenye meza za kamari wala kwenye mashindano ya farasi, sehemu ambazo watu hupoteza pesa nyingi kuliko wanazopata. Kinyume chake, yeye hupatikana sehemu ambazo watu wanafanya mambo ya maana na wanastahili baraka.

“Kwenye kilimo, kwenye biashara halali na kwenye kazi zote ambazo binadamu hufanya kujipatia kipato. Pengine siyo mara zote mtu atapata kwa sababu mara nyingine mipango yake inaweza kuwa mibaya, au nyakati nyingine hali hubadilika na kuwa mbaya. Lakini akimlilia atafanikiwa, hiyo ni kwa sababu uwezekano wa kufanikiwa huwa ni mkubwa.

“Lakini vipi mtu anapocheza kamari?Hali inakuwa ni kinyume chake. Uwezekano wa yeye kushinda ni mdogo kuliko ule wa mchezesha kamari. Mchezo unakuwa umepangwa kumpendelea mchezeshaji. Ni biashara ya mchezesha kamari kutengeneza faida kutoka kwa wachezaji. Ni wacheza kamari wachache hutambua jinsi mchezo unavyompendelea mchezeshaji, na jinsi ulivyo dhidi yao.

“Chukulia mfano wa wanaocheza kamari za mezani. Kila mara kete ikirushwa anasema ni upande upi utakuwa juu. Kama ni mwekundu basi mchezesha kamari atamlipa mara nne ya kiasi alichoweka. Lakini kama ni pande nyingine kati ya pande zake tano ikaja juu basi atapoteza pesa zake. Hesabu inaonyesha kuwa, kila kete inaporushwa kuna uwezekano wa mara tano wa kupoteza pesa zetu zaidi ya uwezekano wa kushinda.

“Lakini kwa sababu rangi nyekundu inalipa mara nne, basi tuna uwezekano wa kushinda mara nne. Kwa hiyo, kila siku mchezesha kamari anatarajia kuingiza moja ya tano ya pesa zote zilizochezwa.

“Je, mtu anaweza kutarajia kushinda mara nyingi ikiwa mchezo umepangwa ili apoteze mmoja katika kila michezo mitano?”

“Lakini watu huwa wanashinda pesa nyingi,” akasema msikilizaji mmoja.

“Ni kweli,” akasema Arkad. “Lakini bado najiuliza kuwa pesa zinazopatikana kwa namna hiyo zinaweza leta mafanikio ya kudumu? Nina rafiki wengi ambao ni matajiri

sana hapa Babiloni, lakini hamna hata mmoja wao aliyepata utajiri wake kupitia kamari. "

“Nyinyi mliokusanyika hapa mnajua watu wengi zaidi. Ningependa kujua ni watu wangapi wamepata mafanikio kupitia kamari? Kila mmoja aseme anaowajua.”

Baada ya kimya kirefu mtu mmoja mjanjamjanja akasema, ‘swali lako linahusisha wachezesha kamari?”

“Kama hamna mnayemfahamu, vipi kuhusu nyinyi, kuna mtu hapa huwa anashinda mara kwa mara kiasi kwamba anaweza kusema kuwa chanzo chake cha mapato ni kamari?”

Swali lake lilijibiwa kwa miguno na vicheko.

“Inaonekana hatuendi kutafuta bahati sehemu ambazo Mungu wa bahati hutembelea,” akaendelea Arkad.

“Hebu na tuone maeneo mengine. Bahati haipo kwenye kuokota pochi. Haipo kwenye meza za kamari wala kwenye mashindano ya farasi. Kwenye mashindano ya farasi nakiri kupoteza pesa nyingi kuliko nilizowahi shinda.

“Sasa tuangalie kazi na biashara zetu. Je, si kawaida kuwa tukifanya biashara, au kazi na kupata faida hatuoni kuwa ni bahati, bali huona kuwa ni matokea ya jitihada zetu? Nafikiri inawezekana hatuoni baraka za Ashtar. Inawezekana anatusaidia lakini hatuthamini baraka zake. Ninyi hili mnalionaje?”

Hapo alisimama mfanyabiashara mmoja mzee na kuweka vazi lake sawa, kisha akasema.”Kwa ruhusa yako mheshimiwa na rafiki yangu Arkad naomba kutoa mchango wangu. Kama umesema mafanikio yetu yanatokana na

jitihada zetu, vipi kuhusu mafanikio tuliyoshindwa kuyafikia? Yale ambayo iwapo tungeyafikia tungepata faida kubwa. Si ingekuwa ni mfano mzuri wa bahati iwapo tungeyafikia? Kwa sababu hatukuyafikia hatuwezi kusema ni baraka tulizostahili. Watu wengi hapa wametokewa na jambo kama hilo."

"Tuliangalie hilo kwa mtazamo ufuatao," akasema Arkad. "Nani kati yenu alikuwa karibu kabisa kupata bahati lakini ikamponyoka?"

Mikono mingi ilinyooshwa, na wa yule mfanyabiashara mzee ukiwemo. Arkad akamuonyeshea ishara kuwa aongee. "Kwa sababu wewe ndiye umetoa wazo, tungependa kusikia kutoka kwako."

"Nitafurahi kuwasimulia hilo," akasema Arkad.

"Nitawasimulia hadithi inayoonyesha ni jinsi gani bahati inaweza mkimbia mtu, na jinsi anavyoweza kuiacha iondoke bila kujua na kuishia kupata hasara, au majuto."

"Miaka mingi iliyopita nilipokuwa kijana. Nilipokuwa nimetoka tu kuanza kazi na kuoa, baba yangu alinifuata na kunisihi sana kuhusu kuanza kuwekeza. Mtoto wa mmoja wa rafiki zake alikuwa ameona eneo moja kame nje ya kuta za mji. Lilikuwa lipo sehemu ya muinuko kutoka kwenye mfereji wa umwagiliaji hivyo maji hayakuweza kufika.

"Kijana yule aliandaa mpango wa kununua lile eneo na alitarajia kujenga mashine ya kupandisha maji iliyoendeshwa kwa ng'ombe. Akikamilisha hilo, alipanga kuligawa kwenye

vishamba vidogovidogo na kuwauzia wakazi wa jiji kwaajili ya kulima bustani.

“Lakini kijana yule hakuwa na pesa za kutosha kufanya yote haya. Kama mimi tu, alikuwa ni kijana mwenye kipato cha kawaida. Baba yake alikuwa na familia kubwa na kipato cha kawaida, kama baba yangu tu. Kwa hiyo aliamua kutafuta watu ambao wako tayari kushirikiana naye kwenye huo mradi. Walitakiwa watu kumi na mbili wenye kipato. Kila mmoja alitakiwa kuchangia moja ya kumi ya kipato chake mpaka pale eneo litakapokuwa tayari kwa kuuzwa. Baada ya kuuza kila mmoja atapata faida kulingana na alichowekeza.

‘Kijana wangu,’ aliniambia baba yangu. ‘Ningependa uanze kuwekeza ungali bado kijana ili hapo baadaye uje kuwa mtu wa maana. Napenda kuona ukifaidika kwa kujifunza kutokana na makosa ya baba yako.’

' ‘Natamani sana kufanya hivyo baba yangu,’ nikajibu.

‘' ‘Vema, nashauri ufanye kile nilichopaswa kufanya nilipokuwa na umri kama wako. Kwenye pato lako hakikisha moja ya kumi unawekeza kwenye mradi. Kwa kipato utakachopata kutokana na uwekezaji huo, utakuwa tajiri mkubwa kabla hata ya kufika umri kama wangu.

‘' ‘Hayo ni maneno ya hekima sana baba yangu. Natamani sana kuwa tajiri lakini kipato changu kina matumizi mengi. Sitaweza kufanya kama ulivyoshauri ila mimi bado ni kijana, muda bado upo.

‘' ‘Hata mimi nilipokuwa na umri kama wako nilifikiri hivyo, lakini sasa miaka mingi imepita na sijafanya

chochote.’

‘ ‘Nyakati zimebadilika mzee wangu, nitajitahidi kuepuka makosa yako.’

‘' ‘Mwanangu, fursa ipo mbele yako. Inakupa nafasi ya kuweza kuwa tajiri. Nakuomba usikawie kuitumia. Kesho nenda kamuone kijana wa rafiki yangu na kubaliana naye kuwekeza asilimia kumi ya pato lako kwenye mradi. Nenda kesho bila kuchelewa. Fursa haimsubiri mtu yeyote. Siku zinasonga haraka, usichelewe.’

“Pamoja na ushauri mzuri wa baba yangu lakini sikuweza kuufuata. Kulikuwa na mavazi mazuri yaliyoletwa na wafanyabiashara kutoka mashariki. Zilikuwa nguo nzuri sana kwa hiyo nikanunua yangu na ya mke wangu.

“Ningetumia asilimia kumi ya pato langu kuwekeza kwenye ule mradi, ningekosa vitu hivi vizuri na vingine vingi. Nilichelewa kufanya maamuzi hadi muda ukapita. Najutia sana jambo hili.

“Mradi ule ulikuja kuleta faida kuliko tulivyofikiria. Hiyo ni hadithi yangu ya jinsi nilivyoacha bahati ipite.”

“Kwenye simulizi hii tumeona jinsi bahati inavyomfuata mtu ambaye anatumia fursa,” alisema mtu mmoja mweusimweusi kutoka maeneo ya jangwani. “Ili kujenga utajiri lazima kuwe na mwanzo. Mwanzo unaweza kuwa vipande vichache tu vya dhahabu au fedha, kile ambacho mtu anatoa toka kwenye pato lake na kuwekeza. Mimi mwenyewe ninamiliki mifugo mingi sana. Nilianza ufugaji nikiwa mvulana tu. Nilinunua ndama mmoja kwa kipande kimoja cha

fedha. Huo ndiyo ulikuwa mwanzo wa utajiri wangu na ninauthamini sana.

“Kuanza hatua za kwanza za kujenga utajiri ndiyo bahati yenyewe. Hatua hiyo ndiyo huwabadili watu kutoka wale wanaotegemea kipato kutokana na kazi zao kuwa wale wanaopata kipato kutokana na uwekezaji wao. Wengine kwa bahati nzuri huwekeza wangali bado vijana. Hawa huwaacha mbali wale wanaowekeza umri ukiwa umeenda, au wale wasiowekeza kabisa, kama baba wa huyu mfanyabiashara.

“Kama rafiki yetu mfanyabiashara angeanza kuwekeza angali kijana pale alipopata fursa, leo angebarikiwa kwa utajiri mkubwa hata zaidi. Kama rafiki yetu mshona nguo naye akichukua hatua muda huu, utakuwa mwanzo wa mafaniko makubwa sana.”

“Asanteni! Nami ningependa kusema.” Akasema mtu mmoja kutoka nchi ya mbali. “Mimi ni Msiria. Siongei vizuri lugha yenu. Napenda kumbatiza huyu mfanyabiashara jina. Pengine mtaona si vema lakini ningependa nimpe jina. Sijui kwa lugha yenu mnamuitaje huyu mtu, nikimuita kwa kisiria hamtaelewa. Naomba mniambie; mnamuitaje mtu ambaye kila mara anachelewa na kusita kufanya mambo ambayo yanaweza kuwa na faida kwake?”

“Mhairishaji,” ilijibu sauti moja.

“Huyo huyo,” alisema Msiria kwa furaha.

“Akiona fursa haitumii, anasema sasa nina mambo mengi, kwaheri tutaongea baadaye. Fursa hawezi kusubiri mtu goigoi hivyo. Anajua kuwa mtu anayetafuta bahati lazima

atachangamkia fursa. Mtu yeyote ambaye hatumii fursa haraka ni mhairishaji mkubwa kama huyu rafiki yetu mfanyabiashara.”

Mfanyabishara alisimama na kutoa ishara ya kuinamisha kichwa baada ya watu kulipuka kwa kicheko.” Heshima yangu kwa mgeni wetu Msiria ambaye hajasita kuongea ukweli’

“Sasa hebu tusikilize simulizi nyingine juu ya fursa iliyopotea. Nani ana simulizi nyingine?” Akauliza Arkad.

“Mimi nina kisa kimoja,” akasema mtu mmoja wa umri wa kati aliyekuwa amevaa vazi jekundu. “Mimi nafanya biashara ya wanyama, hasa hasa ngamia na farasi, na mara chache kondoo na mbuzi. Hadithi yangu itaonyesha jinsi ambavyo fursa hutokea bila kutegemewa. Pengine ndiyo maana niliacha ipite, mtajionea wenyewe.

“Siku moja jioni nilirudi jijini kutoka kwenye safari ya siku kumi ya kutafuta ngamia, safari ambayo sikupata ngamia wowote. Nilipofika Babiloni nilikasirika sana kukuta milango ya jiji imefungwa. Ikatubidi kulala nje ya jiji. Hatukuwa na maji wala chakula cha kutosha. Watumwa wangu walipokuwa wanatengeneza mahema kwaajili ya kulala, nilifuatwa na mfugaji mmoja mzee. Naye pia alikuwa amechelewa na kukuta milango ya jiji imefungwa.

" ‘Mheshimiwa,’ alianza kunisemesha. " ‘Kwa muonekano wako unaonekana kama ni mfanyabiashara. Kama ndivyo ningependa nikuuzie kondoo niliokuja nao, ni kondoo bora kabisa. Mke wangu yupo kitandani kwa kuumwa,

ninatakiwa kurudi nyumbani haraka. Nunua kondoo wangu ili mimi na watumwa wangu turudi bila kuchelewa.”

“Ilikuwa ni giza sana kiasi ambacho sikuweza kuona kondoo wake, lakini kutokana na milio yao nilitambua kuwa walikuwa wengi sana. Baada ya kuhangaika siku kumi na kukosa ngamia nilifurahi kufanya naye biashara. Kwa sababu ya kuwa na haraka alinitajia bei nzuri sana. Nikakubali nikitarajia asubuhi tutawaingiza kondoo jijini na kuwauza kwa faida kubwa.

“Tukakubaliana kisha nikawaita watumwa wangu walete taa ili tuwahesabu wale kondoo. Yule mfugaji alisema ana kondoo mia tisa. Nisiwachoshe na maelezo ya jinsi ilivyo vigumu kuhesabu kundi kubwa la kondoo wenye njaa na kiu gizani. Lilikuwa zoezi gumu sana. Nikamwambia yule mfugaji kuwa nitawahesabu asubuhi kukicha na nitamlipa wakati huo.

‘' ‘Tafadhali mheshimiwa,’ aliniomba. ‘Basi nilipe theluthi mbili ya pesa leo usiku ili niende zangu. Nitamuacha mtumwa wangu mwenye uelewa ili akusaidie kuhesabu ifikapo asubuhi. Yeye ni muaminifu na utampatia pesa iliyobaki.

“Nilikuwa mjeuri na nilikataa kulipa usiku ule. Asubuhi ilipofika, kabla sijaamka milango ya jiji ilifunguliwa na wanunuzi wanne walitoka wakitafuta kondoo. Walikuwa na mchecheto wa kununua, tena kwa bei kubwa sababu kulikuwa na uwezekano wa jiji kuzingirwa hivyo kulikuwa na uhaba wa chakula. Walinunua kondoo wale kwa bei mara tatu zaidi ya

ile niliyoambiwa jana usiku. Hivyo ndivyo nilivoruhusu bahati adimu iniponyoke."

"Hiki ni kisa cha tofauti sana," akasema Arkad. "Kinatufundisha nini?"

"Kinatufundisha kuchukua hatua haraka iwapo tumeona biashara ni nzuri na haina tatizo," alisema mtu mmoja wa makamo ambaye kazi yake ilikuwa ni kutengeneza matandiko ya wanyama. "Kama biashara inaonekana kuwa ni nzuri, je hatuhitaji kujilinda dhidi ya udhaifu wetu kama tu tunavyojilinda dhidi ya binadamu wengine? Binadamu ni viumbe tunaobadilikabadilika. Lakini niseme kuwa, mara nyingi tunabadilika tunapokuwa sahihi kuliko tunapokuwa tumekosea. Tukikosea tunakuwa wajeuri. Tukiwa sahihi, huanza kujizungusha hadi fursa inapotea. Kawaida maamuzi yangu ya kwanza huwa ndiyo bora zaidi. Lakini bado mara nyingi hujikuta nasita kukamilisha biashara ambayo imeonekana ni nzuri. Ili kujilinda na udhaifu huu mara nyingi mimi hukamilisha biashara zangu haraka. Hili hunisaidia kuepuka majuto ya kupoteza bahati.

"Asanteni sana! Ningependa kuongea tena," akasema Msiria akiwa amekwishasimama. "Hizi hadithi zinafanana. Katika zote fursa ilipotea kwa njia ileile. Kila mara fursa inawafuata wahairishaji ikiwa na mpango mzuri. Lakini mara zote wanasita, hawajiambii huu ndiyo muda muafaka nifanye haraka! Mtu unawezaje kufanikiwa kwa mwendo kama huo?"

"Maneno ya busara sana rafiki yangu," akasema mfanyabiashara ya mifugo. "Kwenye simulizi zote, bahati

ilipotea kwa sababu ya kusitasita na kuhairisha mambo. Tunatamani kuwa matajiri, lakini mara zote fursa zinapotokea roho ya kuahirisha na kusitasita inatuambia ngoja kwanza. Kwa kuisikiliza tunakuwa maadui wetu wenyewe, tena adui mbaya.

"Wakati ningali kijana sikulijua hili kwa namna aliyoongelea rafiki yetu Msiria. Mwanzo nilifikiri kwamba maamuzi yangu mabaya ndiyo yalisababisha nikose fursa nyingi zenye faida. Baadaye nikafikiri ni sababu ya ujeuri wangu. Mwisho ndipo nikagundua ni kitu gani hasa—tabia ya kusitasita na kuhairisha bila sababu za msingi badala ya kutenda, kutenda kwa haraka na kwa akili. Baada ya kuijua nimeichukia sana. Kwa hasira za punda wa porini aliyefungwa kwenye gari la farasi nilijichomoa kutoka kwa huyo adui wa mafanikio yangu."

"Asante! Ningependa kumuuliza mfanyabiashara swali," alisema Msiria.

"Wewe unavaa mavazi bora, si kama wavaavyo maskini. Na hata ongea yako ni kama ya mtu aliyefanikiwa. Hebu tuambie, hadi sasa bado unaisikia sauti ya kuhairisha mambo ikikunong'oneza masikioni?"

"Kama tu rafiki yetu mfanyabiashara ya mifugo, mimi pia ilinibidi kuishinda tabia ya kuahirisha mambo," alisema mfanyabiashara. "Kwangu ilikuwa ni adui ambaye alitazama mafanikio yangu ili ayayeyushe. Kisa nilichosimulia ni kimoja tu ila vipo vingi vinavyoonyesha jinsi nilivyopoteza fursa. Ukiijua tabia hii ni rahisi kuishinda. Hakuna mtu anaweza

kumruhusu mwizi aibe ghala yake ya nafaka kwa hiari. Wala hakuna mtu anaweza ruhusu adui akimbize wateja wake na faida yake kwa hiari. Nilipogundua kuwa adui yangu anafanya matendo kama hayo nilidhamiria kumshinda. Hivyo, kila mtu anapaswa kuishinda roho ya kusitasita na kuahirisha mambo kabla hajatarajia kushiriki utajiri wa Babiloni."

MUNGU WA BAHATI HUWAPENDELEA WATU WA VITENDO.

SHERIA TANO ZA DHAHABU

“Ukiambiwa uchague kati ya mfuko uliojaa dhahabu na mabamba ya vigae yaliyoandikwa maneno ya hekima na busara, utachagua nini?”

Wasikilizaji walikuwa wamekaa jangwani, wakiwa wamekusanyika kuzunguka moto. Walikuwa wakisikiliza kwa makini. Mwanga wa moto ulionyesha nyuso zao ambazo zilianza kuwa nyeusi sababu ya jua la jangwani.

“Dhahabu, dhahabu,” walijibu wote ishirini na saba kwa pamoja.

Mzee Kalabab alitabasamu kama vile kuna siri anaifahamu yeye peke yake.

“Sikilizeni niwaambie,” alisema huku akiinua mikono kuwanyamazisha. “Sikilizeni mbwa mwitu wanavyolia kwa kunung’unika sababu ya njaa. Ukisema uwapatie chakula ni nini kitatokea? Wataishia kupigana na wakisha kula watapigana zaidi na kuzurura, wala hawatafikiria kesho yao itakuwaje.

“Hivyo ndivyo walivyo binadamu. Waambie wachague kati ya hekima na dhahabu nao watafanya nini? Wataidharau hekima na kutapanya dhahabu. Kesho yake wanaanza kunung’unika sababu hawana dhahabu.

“Pesa ipo kwaajili ya wale wanaojua sheria zake na kuzifuata.”

Kalabab akatengeneza kanzu yake na kujifunika hadi miguuni sababu upepo wa baridi wa usiku ulikuwa umeanza kuvuma, kisha akaendelea.

“Mmekuwa waaminifu sana kwangu, na katika safari yetu yote mmetunza vizuri ngamia wangu. Mmefanya kazi kwenye joto kali la jangwani bila malalamiko. Mmepambana kishujaa na vikundi vya waporaji waliotaka kupora mali yangu. Kwa sababu ya hayo nitawasimulia kisa kihusucho sheria tano zinazoongoza pesa. Sijawahi msimulia mtu yeyote kisa hiki.

“Nisikilizeni kwa makini sana mambo nitakayowaeleza. Iwapo mtayaelewa vizuri na kuyafanyia kazi mtakuja kuwa matajiri wakubwa.”

“Kalabab mpaka sasa umetusimulia visa vingi sana,” aliongea msimamizi wa upakiaji. “Tunategemea hekima yako na busara zako zituongoze huko tuendako baada ya kesho kumaliza utumishi kwako.”

“Mambo yote niliyokuwa nawasimulia yalikuwa ni visa vilivyonitokea katika safari zangu za mbali. Lakini leo nitawasimulia kuhusu hekima ya Arkad, mtu mwenye busara na tajiri mkubwa.“

“Tumemsika sana huyo bwana,” alisema kiongozi wa upakiaji. “Inasemwa kuwa ndiye mtu tajiri zaidi kuwahi kuishi Babiloni.”

“Alikuwa tajiri mkubwa kwa sababu alikuwa anajua jinsi ya kushughulika na pesa. Alikuwa na ujuzi mkubwa wa pesa

kuliko mtu yeyote aliyepata kuishi kabla yake. Leo nitawasimulia kuhusu hekima yake kama nilivyosimuliwa na kijana wake Nomasir. Zamani nilipokuwa bado kijana huko Ninawi.

“Siku moja mimi na muajiri wangu tulikuwa kwenye jumba la Nomasir hadi usiku mwingi. Nilikuwa namsaidia bosi wangu kupeleka mazulia ili Nomasir ayakague na kuyajaribu kuona kama yanamfaa. Alipopata linalomfaa alitukaribisha kukaa na kunywa pamoja naye. Kilikuwa kinywaji bora na chenye harufu nzuri sana, sijawahi kunywa kinywaji kizuri namna ile.

“Tulipokuwa tunakunywa alitusimulia kisa cha baba yake, Arkad. Nitasimulia kama alivyosimulia.

“Kama mnavyojua, ni desturi ya Babiloni kwa wana wa matajiri kuishi na wazazi wao wakitegemea kurithi utajiri. Arkad hakukubaliana na desturi hii. Hivyo basi, Nomasir alipofika umri wa mtu mzima, alimwita na kumwambia:

'' ‘Mwanangu, ninatamani urithi na kuendeleza utajiri wangu, lakini ni lazima kwanza uthibitishe kuwa unauwezo wa kuusimamia. Kwa hiyo ningependa uonyeshe kwa vitendo iwapo una uwezo wa kupata pesa, na kuwa mtu wa kuheshimika kati ya watu.

'' ‘Kwa kuanzia nitakupatia vitu viwili ambavyo mimi mwenyewe sikuvipata nilipokuwa bado kijana maskini.

'' ‘Kwanza nakupatia mfuko huu wa dhahabu. Iwapo utazitumia kwa busara basi ndiyo utakuwa msingi wa utajiri wako.

'' 'Pili nakupatia hili bamba ambalo juu yake kumeandikwa sheria tano zihusuzo pesa. Iwapo utazitumia kwa vitendo zitakuletea ufanisi na usalama.

'' 'Baada ya miaka kumi kutoka leo rudi hapa nyumbani na unionyeshe mambo uliyotimiza. Iwapo utathibitika kuwa unafaa nitakufanya kuwa mrithi wa mali zangu. Kinyume na hilo, nitatoa mali zangu na kuwapa makuhani, pengine zitanisaidia kuingia peponi.

"Kwa hiyo Nomasir akaondoka na kwenda kujitegemea. Akabeba pochi ya dhahabu aliyopewa na kufunga lile bamba vizuri kwenye kitambaa cha hariri. Akamchukua mtumwa wake, wakapanda farasi na kwenda zao.

"Baada ya miaka kumi kupita Nomasir alirudi kwa baba yake kama walivyokubaliana. Baba yake akamwandalia karamu kubwa sana, na ndugu na marafiki wakaalikwa. Baada ya karamu, baba yake na mama yake wakaketi vitini kama vile ni mfalme na malkia. Nomasir akasimama mbele yao ili kueleza yale aliyotimiza kwa kipindi cha miaka kumi.

"Mke wa Nomasir, wana wake wawili, rafiki zake na ndugu zake wengine wa ukoo walikaa kwenye zulia nyuma yake, wakisubiri kwa hamu kumsikiliza.

'' 'Baba yangu,' alianza kusema, 'Ninainama kwa heshima ya busara zako. Miaka kumi iliyopita nilipoanza kuingia utu uzima, uliniagiza niende na nikapambane kuwa mwanaume kati ya wanaume badala ya kuwa mshirika na mrithi tu wa mali zako.

'' 'Ulinipatia dhahabu na hekima yako. Nikiri kuwa dhahabu uliyonipa sikuweza kuitumia vizuri, ilipukutika yote. Ilikimbia kama vile sungura hukimbia kutoka katika mikono ya mwindaji asiye na uzoefu.

"Baba yake akatabasamu na kusema,' endelea kusimulia, napenda kusikia kwa undani zaidi.'

'' 'Nilipotoka hapa nikaamua kwenda Ninawi. Kwa sababu ni mji uliokuwa unakua, nilitumaini kutakuwa na fursa nyingi. Nilijiunga na msafara wa wafanyabiashara waliokuwa wakielekea huko. Njiani nilipata rafiki wengi na kati yao walikuwapo mabwana wawili wachangamfu. Walikuwa na farasi mweupe mzuri sana.

'' 'Tulipokuwa safarini walinisimulia kuwa huko Ninawi kuna tajiri ambaye alikuwa na farasi, na farasi wake huyo hajawahi shindwa mashindanoni. Mmiliki wake alikuwa akijigamba kuwa hakuna farasi mwenye kasi kama wake. Alikuwa tayari kuweka kiasi chochote cha pesa dhidi ya farasi mwingine yoyote wa Babiloni. Rafiki zangu wale waliniambia kuwa, ukilinganisha na farasi waliyekuwa naye, farasi anayesifiwa ni kama punda tu, na anaweza kushindwa kirahisi sana.

'' 'Wakaniambia kuwa, kama nitapenda, niungane nao katika kuweka pesa juu ya farasi wao dhidi ya farasi wa yule tajiri. Nilivutiwa sana na mpango ule.

'' 'Farasi wetu alishindwa vibaya na nilipoteza dhahabu nyingi sana.'

Baba yake akacheka baada ya kusikia hivyo.

'' 'Baadaye nikaja kugundua kuwa ulikuwa ni mpango wa kitapeli. Wale watu walikuwa wakisafiri na misafara ya wafanyabiashara wakitafuta watu wa kuwatapeli. Yule aliyedaiwa kuwa ni tajiri wa Ninawi alikuwa ni mshirika wao, na waligawana pesa baada ya kushinda. Utapeli huu wa kijanja ulinifundisha somo la kuwa makini.

'' 'Baada ya muda mfupi nilipata funzo lingine lakini kwa uchungu vilevile. Kwenye ule msafara kulikuwa na kijana ambaye tulitokea kuwa marafiki wazuri sana. Alionekana kuwa ni mtoto wa kitajiri, alikuwa anaenda Ninawi kuangalia fursa, kama mimi tu. Muda mfupi baada ya kufika Ninawi akaniambia kuwa kuna mfanyabiashara amefariki na duka lake pamoja na bidhaa zake vinaweza kununuliwa kwa bei nafuu sana. Akaniambia tuwe washirika lakini kwanza inampasa kurudi Babiloni kuchukua pesa zake. Akanishawishi kununua biashara ile kwa pesa zangu. Alisema kuwa pesa zake zitatumika kuongezea mtaji hapo baadaye.

'' 'Siku zilikwenda lakini hakurudi Babiloni kufuata pesa zake, na mbaya zaidi alikuwa hajui biashara, na alikuwa ni mtu mwenye matumizi mabaya. Nilimfukuza kwenye biashara lakini tayari hali ya biashara ilikuwa mbaya sana. Bidhaa zilizobaki zilikuwa hazifai kuuzwa na sikuwa na pesa ya kununulia zingine. Niliamua kuuza ile biashara kwa Muisraeli mmoja kwa bei ya hasara.

'' 'Baada ya hapo maisha yalikuwa magumu sana. Nilitafuta kazi lakini sikupata kwa sababu sikuwa na ujuzi wowote. Nililazimika kumuuza mtumwa wangu, na baadhi ya

nguo zangu ili nipate kula na sehemu ya kulala. Siku zilivyosonga ndivyo maisha yalivyozidi kuwa magumu.

'' 'Katika siku hizo ngumu nilikumbuka jinsi ulivyo na imani nami. Ulinituma nikawe mtu wa maana na hilo ndilo nililopanga kutimiza.' Baada ya kusikia hayo mama yake alijiziba uso na kulia.

'' 'Muda huo ndipo nilipokumbuka kuhusu lile bamba ulilonipatia. Nikasoma maneno yake kwa umakini mkubwa. Nikatambua kuwa, iwapo ningepata busara iliyokuwemo mule kabla ya kuanza kuwekeza, basi nisingeweza kupoteza pesa zangu. Nilijifunza sheria zote na kuziweka akilini. Nikajiapisha kuwa iwapo Mungu wa bahati akinibariki tena, nitaongozwa na busara iliyojengwa kwa miaka mingi badala ya kufanya mambo bila uzoefu, kama ilivyo kawaida ya vijana.

'' 'Kwa faida ya nyote mliokusanyika hapa usiku wa leo, nitasoma hekima aliyonipa baba yangu, kama tu ilivyoandikwa kwenye bamba alilonipa miaka kumi iliyopita.

SHERIA TANO ZA DHAHABU

1. *Dhahabu huja kwa wingi kwa yule ambaye huweka akiba moja ya kumi ya kipato chake, na kuitumia akiba kuwekeza kwa ajili ya wakati ujao.*
2. *Dhahabu hufanya kazi kwa bidii na kwa uaminifu iwapo itampata mtu anayeipatia kazi yenye faida. Hapo itaongezeka kama wanyama wa kufungwa.*

3. *Dhahabu hung'ang'ania kukaa kwa mtu anayeilinda na mwenye tahadhari. Mtu anayeomba ushauri kutoka kwa watu wenye ujuzi na uzoefu wa kuitunza.*
4. *Dhahabu haikai, na hupotea kwa mtu ambaye anawekeza kwenye biashara, au mradi ambao haujui vizuri, au miradi ambayo haishauriwi na wale wenye uzoefu na ujuzi wa kuitunza.*
5. *Dhahabu haikai kwa mtu anayeiwekeza kwenye miradi inayodai kutoa faida kubwa kuliko kawaida, wala kwa wale wanaodanganywa na matapeli na watu wajanja—wajanja, na wale ambao wanawekeza bila kupata ushauri kutoka kwa wale wenye uzoefu, au wale wanaowekeza kwa sababu wanapenda tu miradi ya aina hiyo.*

'' 'Hizi ndizo sheria tano za dhahabu kama zilivyoandikwa na baba yangu. Ninaweza kusema kuwa zina thamani kuliko dhahabu yenyewe, kama tu mtakavyoona kwenye kisa changu.

"Hapo Nomasir alimuangalia tena baba yake. 'Nimekusimulia jinsi kutokuwa na uzoefu kulivyonitumbukiza kwenye umaskini na taabu.

'' 'Lakini hakuna magumu yasiyo na mwisho. Nilipata kazi ya kusimamia watumwa waliokuwa wakijenga ukuta wa jiji.

'' 'Kwa kufuata sheria ya kwanza ya pesa, nilitunza pesa kutoka kwenye pato langu. Niliendelea kutunza kadri nilivyopata hadi nilipofikisha kipande kimoja cha fedha. Nilipata shida kwa sababu kuna matumizi mengi ya maisha,

niliishi kibahili sana. Nilipanga kuwa kabla miaka kumi haijaisha niwe nimepata kiasi cha dhahabu kama kile ulichonipatia.

'' 'Siku moja mmiliki wa wale watumwa ambaye sasa alikuwa rafiki yangu aliniambia. "Wewe ni kijana bahili sana, hutumii kabisa pesa zako, inamaana pesa zako umetunza tu, hazizalishi?"

'' 'Ndiyo,' nilimjibu, 'mpango wangu ni kutunza hadi kifike kiasi kama kile alichonipatia baba yangu nami nikakipoteza,'

'' 'Ni mpango mzuri, lakini unafahamu kuwa pesa unayoitunza inaweza kukuzalishia pesa nyingi zaidi?"

'' 'Nafahamu lakini naogopa kupoteza pesa zangu kama nilivyopoteza zile alizonipatia baba yangu.'

'' 'Kama unaniamini basi ninaweza kukufundisha jinsi ya kuwekeza pesa kwa faida,' aliniambia. "Ndani ya mwaka mmoja ukuta huu utakuwa umemalizika kujengwa. Utahitaji shaba kwaajili ya kutengenezea milango. Kila lango litahitaji mlango ili kulinda jiji dhidi ya maadui. Huu ndiyo mpango wangu: tujikusanye na tuchange pesa, kisha tukanunue shaba na tini kutoka migodini na kuileta hapa Ninawi kwaajili ya milango. Mfalme atakaposema 'milango itengenezwe,' basi sisi pekee ndiyo tutakuwa na shaba na tini, na tutamuuzia kwa bei nzuri. Hata kama mfalme hatanunua kutoka kwetu tutaweza kuuza kwa watu wengine na kwa bei nzuri.

'' 'Kwa jinsi alivyonieleza nilikumbuka sheria ya tatu ya pesa. Sheria inayoshauri kuwekeza chini ya uongozi wa watu

wenye ujuzi na uzoefu. Sikujutia uamuzi wangu, uwekezaji wetu ulikuwa wa mafanikio makubwa na pesa zangu chache ziliongezeka sana.

'' 'Baada ya hapo nikakaribishwa kuwa mshirika rasmi wa lile kundi, toka hapo nilishiriki kwenye uwekezaji mwingine mwingi sana. Lilikuwa ni kundi la watu wanaojua jinsi ya kuwekeza pesa kwa faida. Kila mpango wa uwekezaji ulijadiliwa kwa kina kabla ya kuanza. Hawakuwekeza kwenye miradi ambayo kulikuwa na hatari ya kupoteza mtaji wala, hawakuwekeza kwenye miradi ambayo haileti faida au ambayo ni ngumu kurejesha mtaji.

'' 'Vitu vya kipumbavu kama mashindano ya farasi, au biashara yangu ya ushirika na yule tapeli hata visingefikiriwa na watu hawa. Mara moja wangejua ubaya wa miradi ile.

'' 'Kutokana na kushirikiana na watu hawa, nilijifunza jinsi ya kuwekeza pesa kwenye miradi yenye faida na salama. Miaka ilivyokwenda ndivyo hazina yangu ilivyozidi kuongezeka kwa kasi. Nilifikisha kile kiasi nilichopoteza mwanzo na kupata ziada.

'' 'Kutokana na magumu niliyopitia na hatimaye mafanikio, nilikuwa nimeona ukweli wa busara zilizokuwemo kwenye zile sheria tano za dhahabu, na ukweli wa busara za baba yangu. Zilifanya kazi kila nilipozitumia.

'' 'Kwa asiyefahamu sheria hizi tano, pesa kwake haiji kirahisi na huondoka haraka. Lakini kwa yule anayezifahamu, pesa huja kirahisi na kumfanyia kazi kama mtumwa muaminifu.

“Nomasir alisimama na kumuonyeshea ishara mtumwa aliyekuwa amesimama nyuma ya kile chumba. Mtumwa alileta mifuko mitatu mizito ya ngozi, akibeba mmoja mmoja. Nomasir aliuchukua mmoja na kuuweka mbele ya baba yake na kusema:

‘' ‘Ulinipatia mfuko mmoja wa dhahabu, dhahabu ya Babiloni. Tazama, narudisha kwako dhahabu ya Ninawi yenye uzito uleule. Wote watakubaliana nami kuwa ni mabadilishano sawa.

‘' ‘Pia ulinipatia bamba la kigae lililokuwa limeandikwa mambo ya busara juu yake. Tazama! Narudisha mifuko miwili ya dhahabu,’ baada ya kusema hayo, alichukua ile mifuko miwili na kuiweka mbele ya baba yake.

‘' ‘Nimefanya hivi ili kukuthibitishia ni jinsi gani nathamini hekima na busara zako kuliko dhahabu zako. Ni nani anaweza kupima thamani ya hekima? Bila hekima pesa hupotea haraka, lakini mtu mwenye hekima hata kama hana pesa anaweza kuzipata. Mifuko hii mitatu ya dhahabu ni ushahidi kuhusu hilo.

‘' ‘Ni jambo ninalojivunia sana kusimama hapa mbele yako na kusema kuwa hekima yako imeniwezesha kuwa tajiri na kuwa mtu katika watu.’

“Baba yake aliweka mikono yake juu ya kichwa cha Nomasir na kusema. ‘Umejifunza masomo yako vizuri, nami ni mtu mwenye bahati kwa kuwa na mwana ambaye ninaweza kumuamini juu ya mali yangu.’ ‘'

Kalabab alisimama kusimulia kisa chake na kuwaangalia wasikilizaji wake kwa makini.

‘‘Hadithi hii ya Nomasir ina maana gani kwenu?”Aliwauliza. Kisha akaendelea kusema.

“Nani kati yenu anaweza kwenda kwa baba yake, au kwa baba mkwe wake na kumueleza jinsi alivyoweza kusimamia pesa zake vizuri?

“Watu huwa na pesa nyingi kwa sababu wanazijua sheria tano za pesa na wanazifuata.

“Kwa sababu nilijifunza sheria hizo nilipokuwa kijana na nikazifuata, nimeweza kuwa mfanyabiashara tajiri. Utajiri wangu haujaja kimiujiza.

“Utajiri unaokuja haraka hupotea haraka pia.

“Utajiri unaodumu na kumfurahisha anayeumiliki huja polepole. Huo ni mtoto aliyezaliwa kutokana na maarifa na uvumilivu.

“Kwa mtu mwenye kufikiri kwa kina, kupata utajiri si kazi ngumu wala mzigo mzito. Siri ni kubeba mzigo huo mwaka hadi mwaka na mwisho lengo lake litatimia.

“Sheria tano za dhahabu huwapatia utajiri wale wanaozichunguza. Kila moja ya sheria hizi tano ni ya maana sana. Msizidharau kwa sababu nimezieleza kwa hadithi fupi tu. Nitarudia kuwaeleza tena. Nimeziweka zote akilini mwangu kwa sababu nilizijua ningali kijana na niliona thamani yake. Nilijifunza kwa bidii hadi nilipozijua vizuri na kuzikariri.

Sheria ya kwanza ya dhahabu

Dhahabu huja kirahisi na kwa wingi kwa mtu ambaye anatunza si chini ya moja ya kumi ya pato. Sehemu itakayojenga utajiri kwaajili ya wakati wake ujao na wa familia yake.

“Mtu yeyote anayeweka akiba moja ya kumi ya pato lake bila kukoma, na akiziwekeza pesa hizo kwa hekima, atapata utajiri ambao utampatia kipato kwa wakati wake ujao na wa familia yake iwapo Miungu ikimchukua. Mara zote sheria hii husema kuwa pesa humfuata mtu huyo. Mimi mwenyewe nimeliona hilo maishani mwangu. Kadri nilivyozidi kutunza pesa ndivyo ilivyozidi kuja kwa urahisi na kwa wingi. Pesa niliyotunza ilizalisha zaidi, yenu pia itafanya hivyo. Na kilichozalishwa kinatakiwa kizalishe pia. Hivyo ndivyo sheria ya kwanza inavyofanya kazi.

Sheria ya pili ya dhahabu

Dhahabu hufanya kazi kwa bidii na kwa uaminifu kwa muajiri anayeipatia kazi yenye faida. Hapo huongezeka kama wanyama wa kufugwa.

“Pesa ni mfanyakazi mwenye kujituma. Tamaa yake kubwa ni kuongezeka kila fursa ya kuongezeka inapopatikana.Mtu yeyote anayejiwekea akiba ya pesa ndiye hufuatwa na fursa zenye faida. Kila mwaka pesa itajizalisha kwa namna ya ajabu sana.

Sheria ya tatu ya dhahabu

Pesa hung'ang'ania kukaa kwa mtu mwenye kuitunza kwa tahadhari na anayeiwekeza baada ya kupata ushauri kutoka kwa wenye uzoefu wa masuala ya pesa.

"Ni kweli, pesa haiondoki kwa mtu mwenye kuchukua tahadhari na hukimbia kutoka kwa watu wasio makini. Mtu anayeomba ushauri kutoka kwa watu wenye ujuzi wa masuala ya pesa, hujifunza kutohatarisha hazina yake bali kuilinda na kuitunza. Huyo hukaa na kufurahia inavyoongezeka kila siku.

Sheria ya nne ya dhahabu

Pesa huondoka kwa mtu anayewekeza kwenye miradi ambayo hana uzoefu nayo au ambayo haishauriwi na wale wenye uzoefu na masuala ya pesa.

"Kwa mtu mwenye pesa na ambaye hana uzoefu, kila mradi utaonekana ni wenye faida. Lakini mingi yao huwa na hatari ya kuleta hasara. Na ikitokea watu wenye uzoefu wa kuwekeza wakaipitia miradi hiyo, basi huikuta inauwezekano mdogo wa kuleta faida. Mtu mwenye pesa ambaye hana uzoefu wa masuala ya pesa lakini akaamua kuwekeza mradi asioujua kwa kutegemea uelewaji wake mwenyewe, mara nyingi hukuta miradi hiyo haipo kama alivyotarajia na kuishia kupoteza hazina yake. Mtu mwenye busara ni yule anayewekeza hazina yake kwa kufuata ushauri kutoka kwa wenye ujuzi wa masuala ya pesa.

Sheria ya tano ya dhahabu

Dhahabu humkimbia mtu anayeilazimisha kuzalisha kiasi kikubwa kuliko inavyowezekana, anayefuata ushauri wa matapeli na wajanjawajanja, anayewekeza bila kupata ushauri wa wale wenye uzoefu wa masuala ya pesa na yule anayewekeza kwenye miradi kwa sababu tu anaipenda.

"Mara nyingi mtu akiwa na pesa mawazo mazuri ya jinsi ya kufanikiwa humjia. Anakuwa na mawazo ya kuwekeza na kupata faida kubwa kuliko kawaida. Mtu mwenye hekima anajua hatari ya kutaka kutengeneza pesa nyingi kwa haraka.

"Msiwasahau wale matajiri wa Ninawi ambao hawakuwekeza kwenye miradi iliyohatarisha mitaji yao, wala hawakuzika mitaji yao kwenye miradi isiyoleta faida.

"Huu ndiyo mwisho wa simulizi langu kuhusu sheria tano za dhahabu. Hiyo ndiyo siri ya mafanikio yangu.

"Kwa kweli hakuna siri ya utajiri bali ukweli ulio wazi. Ukweli ambao kila mtu anayetaka kufanikiwa inampasa kujifunza na kuufuata. Mtu anayetamani kutokuwa kama hao mbwa mwitu, viumbe ambao wanahangaika kupata chakula chao kila leo anatakiwa kufanya yale niliyowaeleza.

"Kesho tutaingia Babiloni, nadhani mnauona moto unaowaka daima juu ya hekalu la Beli? Kesho nitawalipa kila mmoja kwa kazi yake, mmekuwa waaminifu sana.

"Kila mmoja wenu yampasa kujiuliza, miaka kumi kutoka leo atazungumza nini juu ya pesa nitazomlipa?

"Kama kati yenu kuna watu kama Nomasir, basi watatumia sehemu ya kumi ya pesa zao kuwekeza, na

watatumia hekima ya Arkad katika uwekezaji huo. Kama watafanya kama alivyofanya kijana wa Arkad, basi miaka kumi kutoka sasa watakuwa matajiri wakubwa na watu wenye kuheshimika.

"Matendo ya hekima hutufuata maisha yetu yote. Hutuburudisha na kutusaidia. Hivyohivyo, matendo yasiyo na hekima hutufuata ili kutuumiza na kututesa. Sehemu kubwa ya mateso hayo huwa ni majuto juu ya mambo tuliyopaswa kufanya lakini hatukufanya. Majuto juu ya fursa zilizotutembelea lakini tukazipuuza.

"Babiloni ni mji tajiri kiasi kwamba hakuna mtu anayeweza kuhesabu dhahabu ulizonazo. Kila mwaka hazina yake inazidi kuongezeka. Kama hazina zingine, hii ni zawadi, zawadi nzuri kwaajili ya wale wenye malengo ya kuipata. Ndani ya nia zenu kuna nguvu kubwa. Chocheeni nia hizo kwa kutumia sheria tano za dhahabu nanyi mtashiriki utajiri wa Babiloni."

MKOPESHA PESA WA BABELI

Mtu mmoja anayeitwa Rodan, aliyekuwa ni mtengeneza mikuki alikuwa ameshikilia kiasi kikubwa sana cha pesa. Maishani mwake hajawahi kushika kiasi kikubwa kama hicho. Vipande hamsini vya dhahabu! Alikuwa anatembea kwa furaha akishuka kwenye barabara pana inayotoka kwenye ikulu ya mfalme. Dhahabu kwenye pochi yake ililia kila alipotembea. Hajawahi kusikia sauti nzuri kama hiyo.

Hakuamini kuwa vipande vile hamsini vya dhahabu ni vyake. Mawazo juu ya nguvu ya vipande vile yalimzonga, viliweza kununua chochote alichotaka; nyumba nzuri, ardhi, ng'ombe, ngamia, farasi na magari yake; chochote alichotamani.

Azifanyie nini? Jioni hii alipokuwa anakatisha kuelekea kwa dada yake mawazo yake yote yalikuwa kwenye pesa zake.

Jioni kadhaa mbele Rodan alikuwa dukani kwa Mathon. Mathon alikuwa ni mkopesha pesa, na muuza vito na vitambaa adimu. Bila kutizama pembeni, alipita moja kwa moja hadi nyuma ya duka, ilipo nyumba ya kuishi Mathon. Huko alimkuta Mathon akila chakula alichoandaliwa na mtumwa wake.

“Naomba unisaidie ushauri juu ya jambo moja maana sielewi cha kufanya.” alisema Rodan huku akiwa amesimama kizembe, miguu katanua na koti lake likiwa wazi na kuacha nywele za kifuani kuonekana.

Mathon alitabasamu kirafiki na kusema, “Umepatwa na nini hadi utake ushauri kutoka kwa mkopesha pesa? Umepoteza pesa kwenye kamari? Au kuna mwanamke amekuchanganya? Nimekufahamu siku nyingi lakini hata siku moja hujawahi omba msaada wangu.”

“Hapana! Hapana! Sijaja kukopa pesa, nimekuja tu kuomba ushauri wako,”

“Maajabu haya! Hakuna mtu anayeenda kwa mkopesha pesa kuomba ushauri. Au sijasikia vizuri?”

“Umesikia sahihi kabisa,” alisema Rodan.

“Inawezekanaje kuwa hivyo? Isijekuwa una jambo lako! Watu huja kwangu kukopa pesa kwaajili ya mambo yao lakini si kupata ushauri. Lakini kiukweli ni nani anayeweza kutoa ushauri mzuri zaidi ya mkopesha pesa? Mtu ambaye watu humtafuta wapatapo matatizo. Sasa niambie, kitu gani kinakusumbua. Kwanza karibu ule pamoja nami.” alikaribishwa Rodan, “Karibu uwe mgeni wangu usiku wa leo.”

“Andol” Mathon alimwita yule mtumwa mweusi, “Tandika zulia kwaajili ya rafiki yangu Rodan, amekuja kupata ushauri. Mletee chakula kizuri na mletee bilauri kubwa, pia chagua divai bora kabisa ndiyo umletee.”

“Ni zawadi niliyopewa na mfalme,” alianza kusema Rodan.

“Zawadi ya mfalme? Yaani mfalme amekupa zawadi mbayo imekuletea matatizo! Zawadi gani hiyo?”

“Nilipewa kazi ya kuunda mikuki, mfalme alipendezwa sana na kazi yangu hivyo akanipatia zawadi ya vipande 50 vya dhahabu, vipande hivyo ndivyo vinavyonichanganya.

“Haipiti saa lazima nitaombwa na mmoja wa jamaa zangu.”

“Hiyo ni kawaida. Watu hupenda kugawiwa pesa toka kwa mtu wanayefikiri amezipata kirahisi. Kwani huwezi kukataa? Inamaana huna roho ngumu kama mikono yako ilivyo migumu?”

“Wengi ninawakatalia lakini kuna wengine ni vigumu kuwakatalia. Mtu unawezaje kumnyima dada yako kipenzi?”

“Dada yako hawezi kukuzuia kufurahia zawadi yako.”

“Lakini ni kwaajili ya mume wake, Araman.” Alijibu Rodan. “Anasema kuwa mume wake hajawahi pata fursa ya kutajirika, hivyo ananibembeleza nimkopeshe ili afanye biashara na kutajirika, atanilipa kutokana na faida atakayopata.

“Sikiliza rafiki yangu,” akasema Mathon. Hili ni jambo la maana sana umelileta, inatupasa kulijadili. Pesa inampa yule aliyenayo wajibu mkubwa na pia inabadili nafasi yake katika jamii. Inamfanya awe muoga wa kuipoteza au kutapeliwa. Na inamfanya ajihisi ana nguvu, lakini pia inaweza sababisha nia zake njema zimuingize matatizoni.

“Umewahi kusikia kisa cha mkulima wa Ninawi aliyekuwa na uwezo wa kuelewa lugha za wanyama? Natumaini hujawahi maana hizi siyo hadithi watu husimuliana wanapokuwa wanaunda mikuki, au kuponda shaba. Nitakusimulia kisa hicho ili ujue kuwa kukopa ni zaidi ya kuhamisha fedha kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine.

“Mkulima aliyeweza kuelewa wanyama wanachosema alikuwa anakaa karibu na banda Kila jioni ili kusikiliza wakiongea.

“Jioni moja alimsikia ng’ombe dume akinung’unika na kumwambia punda kuwa anafanya kazi ngumu sana. ‘Ninavuta jembe la kulimia toka asubuhi hadi usiku unapoingia. Haijalishi kuna joto kiasi gani, miguu yangu imechoka namna gani au nira imenichubua shingo kiasi gani, lazima nifanye kazi. Lakini wewe unaraha sana, umefungwa matandiko mazuri na kazi yako ni kumbeba bwana na kumpeleka atakako. Kama hana safari basi unapumzika siku nzima ukila nyasi.

“Punda alikuwa ni mnyama mwenye dharau lakini alikuwa na roho nzuri hivyo alimuonea huruma yule ng’ombe. ‘Rafiki yangu,’ akaanza kusema punda yule, ‘unafanya kazi ngumu sana. Nitakusaidia kuipunguza. Nitakwambia jinsi unavyoweza kupata siku za mapumziko. Asubuhi mtumwa anapokuja kukuchukua kwenda kulima, lala chini na gugumia kwa sauti kumfanya afikirie kuwa unaumwa hivyo hataweza kukupeleka kazini.’

“Fahali yule alichukua ushauri wa punda. Kesho yake asubuhi mtumwa alienda kwa mwenye shamba, akamwambia kuwa ng’ombe wa kulimia anaumwa hivyo hataweza kufanya kazi.

“Mwenye shamba akasema. ‘‘‘Basi mfunge punda kwenye jembe la kulimia. Kazi ya kulima lazima iendelee.’

“Nia ya punda ilikuwa ni kumsaidia rafiki yake tu, lakini siku hiyo alijikuta akilima siku nzima. Usiku ulipofika aliachiliwa lakini alikuwa amekasirika sana, miguu ilimuuma na shingo ilimuuma sababu nira ilikuwa imemchubua.

“Yule mwenye shamba akajibanza karibu na banda la wanyama ili aendelee kusikiliza.

“Wewe ni rafiki yangu mzuri sana. Sababu ya ushauri wako nimepumzika siku nzima,’ alisema yule fahali.

‘' ‘Nimekuwa kama watu wengine wenye huruma, watu ambao wanawasaidia rafiki zao na mwisho hushia kuwafanyia kazi. Kuanzia leo utafanya kazi zako mwenyewe. Tena nimemsikia bwana akisema kuwa ukiumwa tena atakuchinja, na natamani akuchinje tu maana umekuwa mvivu,’ alisema punda kwa hasira.

“Kuanzia siku hiyo urafiki wao uliisha na hawakusemezana tena.

“Rodan unafikiri kisa hiki kinatufundisha nini?”

“Ni hadithi nzuri,” alijibu Rodan, “Lakini sijaelewa inachofundisha.”

“Sikufikiria kama utaelewa, lakini kuna somo zuri na ni rahisi kuliona, ni hili: kama unataka kumsaidia rafiki yako

basi msaidie, lakini hakikisha tatizo lake halihamii kwako.”

“Sikufikiria hilo. Ni somo zuri sana. Kwakweli sina mpango wa kubeba mzigo wa shemeji yangu.

“ Lakini wewe hukopesha pesa kwawatu wengi, si huwa wanakulipa?”

Mathon akatabasamu. Tabasamu la mtu mwenye utajiri wa maarifa. Kisha akasema:

“Je, mkopo unaweza kuwa mzuri iwapo aliyekopeshwa hawezi kulipa? Si ni lazima mkopesha pesa awe makini kujua iwapo mkopo wake utalipwa, au utatapanywa na kumuacha na hasara?

“Nitakuonyesha dhamana zilizopo kwenye sanduku langu la dhamana nazo zitakusimulia visa vyao.”

Mathon akaingia chumbani na kutoka na sanduku lenye kama urefu wa mkono mmoja. Lilikuwa limezungushwa kwa ngozi na kupambwa kwa shaba. Aliliweka sakafuni na kuchuchumaa kulifungua. Kwa kila mkopo ninaotoa huwa nataka kitu fulani toka kwa wateja wangu. Wanapomaliza kulipa huwa nawarudishia, lakini wakishindwa kulipa mimi huviacha humu kama kumbukumbu ya kukosa kwao uaminifu.

“Sanduku langu linaniambia kuwa; mikopo salama ni ile ambayo wakopaji wanaweka vitu vya thamani kama dhamana. Wenye ardhi, vito, ngamia nk. Muda mwingine dhamana huwa na thamani kubwa kuliko mkopo niliotoa. Zingine huwa ni ahadi, tunakubaliana kuwa wakishindwa kulipa basi watanipatia sehemu fulani ya mali zao. Kwa mikopo kama

hiyo huwa nahakikisha mali hizo zinathamani ya juu kidogo kuliko mkopo ninaotoa.

“Wengine ni wafanyakazi kama ulivyo wewe. Hawa wana kipato cha uhakika, wasipopatwa na matatizo yoyote ninakuwa na uhakika wa kulipwa pesa zangu pamoja na riba. Mikopo hiyo hutegemea jitihada za watu.

“Wengine ni wale ambao hawana mali wala kazi ya kuwaingizia kipato. Maisha ni magumu lakini kuna watu wengi wasioweza kubadilika kulingana na nyakati.”

Mathon alifungua sanduku lake na Rodan akasogea na kuinama karibu kwa shauku. Alipofungua kulikuwa na kidani cha shaba kikiwa juu ya kitambaa chenye rangi nyekundu-angavu.

“Mathon alikichukua kile kidani na kukisugua taratibu. Hiki kitabaki kwenye sanduku langu siku zote, mwenye nacho alikwishafariki. Hiki ni kumbukumbu ya rafiki yangu mpendwa. Tulifanya biashara pamoja na kupata mafanikio makubwa. Alikutana na mwanamke mmoja mzuri kutoka mashariki na wakaoana, alikuwa ni mwanamke mnjanja—mjanja sana. Rafiki yangu alitumia pesa zake nyingi ili kutimiza tamaa za mwanamke yule. Alipofilisika alinifuata kuomba msaada, nilimshauri na kumwambia kuwa nitamsaidia kuweka mambo yake sawa. Alinihakikishia kuwa hataniangusha lakini haikuwa hivyo. Kuna siku waligombana na mkewe akaishia kuchomwa kisu na mkewe na kufariki.”

“Nini kilimpata mke wake?” Akauliza Rodan.

“Hicho kipande cha kitambaa chekundu-angavu ni chake. Alijutia alichokifanya hivyo akajiua kwa kujitumbukiza kwenye mto Efrati. Mkopo huu hautakuja kulipwa kamwe. Sanduku hili linatufundisha kuwa mtu aliye kwenye msongo wa mawazo hafai kukopeshwa.

“Hapa kuna kitu kingine, hiki kisa chake ni tofauti.” Alisema Mathon na kuchukua pete iliyokuwa imetengenezwa kwa mifupa ya ng’ombe dume.

“Hii ilikuwa mali ya mkulima. Nilikuwa nanunua mazulia kutoka kwa wake zake. kuna kipindi baa la nzige lilitokea na hawakuwa na chakula. Nilimkopesha kwa makubaliano kuwa atanilipa atakapovuna msimu unaofuata. Lakini baada ya muda akaja na kuniomba kuwa kwenye nchi ya mbali kulikuwa na mbuzi bora sana. Aliniambia kuwa walikuwa ni wenye manyoya mengi na laini, manyoya ambayo yangeweza kutengeneza mazulia bora kabisa.

“ Nilimkopesha pesa ili akanunue mbuzi hao na kuwaleta hapa Babeli. Mwaka ujao tutavuna manyoya na kuwashangaza matajiri wa Babeli kwa mazulia bora kabisa, nao watanunua kwa pesa nyingi. Hapo ndipo nitamrudishia pete yake. Anasisitiza kuwa atanilipa haraka sana.

“He! Kuna wakopaji wanaosisitiza kulipa madeni yao haraka na kwa mkupuo?” alihoji Rodan.

“Kwa wale wanaokopa kwa malengo ya kuwekeza mara nyingi huwa hivyo, lakini wale wanaokopa kwa matumizi tu nakuonya dhidi yao iwapo unataka pesa yako irudi mikononi mwako.”

“Vipi kuhusu hiki,” alisemaRodan huku akishika bangili ya dhahabu iliyokuwa imepambwa na vito adimu, ikiwa na muundo wa pekee.

“Bado unatamani wanawake? " Alisema Mathon kwa utani.

“Mimi bado ni kijana kuliko wewe,” alijibu Rodan.

“Ni kweli lakini bangili hiyo isikufanye ufikirie mapenzi, mwenye nayo ni mwanamke mnene na mzee. Ni mwenye maneno mengi hadi huniudhi. Mume wake alikuwa ni tajiri na walikuwa wateja wangu wazuri. Lakini baadaye hali yao haikuwa nzuri na wakafilisika. Akataka mwanawe awe mfanyabiashara hivyo alikuja na kukopa dhahabu. Akampatia mwanawe ili aungane na wafanyabiashara wanaosafiri.

“Mfanyabiashara aliyeungana naye hakuwa mtu mzuri. Walipokuwa mji wa mbali alimtoroka kijana wakati wa asubuhi sana. Kijana hakuachwa na chochote. Labda kijana huyu akiwa mtu mzima ataweza kunilipa, lakini mpaka sasa sijalipwa chochote zaidi ya maneno tu. Hata hivyo bangili hii ni dhamana nzuri kwa ule mkopo.

“Huyu mama alikuomba ushauri wa juu cha kufanya na ule mkopo?”

“Hata kidogo. Alikuwa ana ndoto akimuona kijana wake akiwa tajiri na mtu mkubwa hapa Babiloni. Kumshauri vinginevyo ilikuwa ni kumkasirisha tu. Toka mwanzo nilikuwa na shaka na ile biashara kwa sababu kijana wake hakuwa na uzoefu wowote, lakini sababu aliweka dhamana sikuona sababu ya kumkatalia.

“Hiki hapa,” aliendelea kusema Mathon huku akifungua kamba moja, ‘Hii ni mali ya Nebaturi, mfanyabiashara ya ngamia. Kila atakapo kununua ngamia wengi kuliko pesa alizonazo huniletea kamba hii, nami humkopesha kulingana na mahitaji yake. Ni mtu ninayemuamini sana. Ni mfanyabiashara mzuri na muaminifu hivyo hata bila dhamana mimi humkopesha. Ninawaamini wafanyabiashara wengi hapa Babiloni sababu ya uaminifu wao. Huweka mali zao kama dhamana na kuzikomboa mara tu wakamilishapo biashara.Wafanyabiashara wazuri ni hazina ya mji wetu, pia ni faida kwangu kuwasaidia kuendelea kufanya biashara na kuzidi kuneemesha mji wetu.”

Mathon alichukua kito cha rangi ya ubluu na ukijani kisha akakitupa chini kwa dharau. “Mdudu kutoka Misri. Aliyekuwa anamiliki hiki kito hajali kabisa kunilipa. Nikimfuata kumdai anajibu, ‘Nitakulipaje nami nimeandamwa na majanga kila leo? Hata hivyo wewe unapesa za kutosha! Unafikiri nitafanya nini?’

“Dhamana ni ya baba yake. Baba yake si mtu tajiri lakini alijinyima na kuweka shamba na mifugo yake kama dhamana ili mwanae afanye biashara. Kijana wake alianza vizuri biashara zake na alikuwa akipata faida, lakini baadaye akaingiwa na tamaa ya kutaka utajiri wa haraka. Kwa kuwa hakuwa na ujuzi mwingi, biashara yake ikafa.

“Vijana wana malengo makubwa sana. Mara zote wanatafuta njia ya mkato ya kuwa matajiri. Ili kupata utajiri haraka mara nyingi hukopa bila kufikiri. Kwa kukosa kwao

uzoefu hawatambui kuwa deni baya ni shimo refu ambalo unaweza kutumbukia kirahisi, lakini ukahangaika kwa siku nyingi ili kutoka. Ni shimo la majuto na huzuni. Ni shimo ambalo jua la mchana huzibwa na mawingu na usiku hufanywa mchungu kwa usingizi wa mang'amung'amu.

"Si kwamba nashauri watu wasikope, hapana! Nasisitiza watu wakope lakini iwe kwa jambo la maana. Mimi mwenyewe nilianza kufanya biashara kwa pesa za mkopo.

"Lakini mkopeshaji anapaswa kufanya nini kwa jambo kama la huyu kijana? Kijana mwenyewe amekata tamaa, hafanyi chochote wala hafanyi bidii yoyote kulipa deni. Moyo wangu unakuwa mzito kuchukua shamba na mifugo ya baba yake."

"Umeniambia habari nyingi na nimezifurahia," alisema Rodan. "Lakini hujajibu swali langu, je nimkopeshe vipande vyangu hamsini vya dhahabu mume wa dada yangu? Kumbuka hawa ni ndugu zangu wa karibu sana.

"Dada yako ni mtu anayejitambua nami namheshimu kwa hilo. Lakini kama mume wake angekuja kwangu kuomba nimkopeshe vipande hamsini vya dhahabu lazima ningemuuliza anataka kufanyia nini?

"Kama akisema anataka kuwa mfanyabiashara kama mimi, anataka kuuza vito na samani za gharama nitamuuliza. Una ujuzi gani kuhusiana na biashara? Unajua unakoweza kununua kwa bei rahisi ? Unajua unakoweza kuuza kwa bei nzuri?

"Je, shemeji yako anafahamu vitu hivyo?

“Kwakweli hafahamu,” akajibu Rodan. “Alikuwa msaidizi wangu kwenye kutengeneza mikuki na amewahi kuwa msaidizi wa dukani.”

“Kama ni hivyo nitamwambia kuwa hajachagua kazi yake kwa busara. Mfanyabiashara anatakiwa kuwa na ujuzi wa kazi hiyo. Ana malengo mazuri lakini hayatimiziki, nisingeweza mkopesha pesa zangu.

“Tuseme angejibu kuwa, ‘Nafahamu sababu nimekuwa msaidizi wa wafanyabiashara kwa muda mrefu. Ninajua jinsi ya kufika Smyrna na kununua mazulia yaliyoshonwa na wakinamama kwa bei ya chini. Pia nawajua matajiri wengi wa Babiloni ninaoweza kuwauzia kwa faida kubwa,’ Hapo ningemwambia kuwa ‘Lengo lako ni zuri na mpango wako unatekelezeka. Kwa hiyo ningekuwa tayari kumkopesha vipande hamsini vya dhahabu iwapo atakuwa na dhamana.”

“Iwapo angesema ‘Nina dhamana yoyote lakini mimi ni muaminifu, nitalipa pesa yako vizuri,’ ningemwambia; ‘Ninathamini kila kipande cha dhahabu nilichonacho. Inaweza tokea wanyang’anyi wakakupora pesa unapoenda Smyrna au kukupora mazulia unaporudi. Si unakuwa huna jinsi ya kunilipa na pesa yangu inakuwa imepotea?’

“Sikiliza Rodan, pesa ndiyo bidhaa ya mkopesha pesa. Ni rahisi kuikopesha lakini ukikopesha bila busara itakuwa vigumu sana kuirudisha. Mkopeshaji mwenye busara anahitaji kujihakikishia ulipwaji wa pesa yake.

‘‘Ni vizuri kuwasaidia wale walio kwenye matatizo, ni vizuri kuwasaidia wale wanaoanza ili baadaye waje kuwa

watu wa maana. Lakini msaada unatakiwa kutolewa kwa hekima, isiwe kama yule punda wa mkulima, kumsaidia mtu na badala yake tuishie kubeba mzigo wake.

“Sasa bwana Rodan, kuhusiana na swali lako, hili ndilo jibu langu: baki na pesa zako, hakuna mtu atasema ana haki ya kupata sehemu ya pesa hiyo labda utake mwenyewe kumpa. Kama unataka kukopesha ili upate faida basi kopesha kwa tahadhari, na kopesha watu wengi. Sipendi pesa ikae tu lakini hata zaidi, sipendi hatari ya kupoteza pesa.

“Umefanya kazi kama mtengeneza mikuki kwa miaka mingapi?”

“Miaka mitatu kamili,’ alijibu Rodan.

“Mbali na zawadi uliyopewa na mfalme, ni kiasi gani kingine umeweka kama akiba?”

“Vipande vitatu vya dhahabu.”

“Kwahiyo kwa kila mwaka uliofanya kazi ulijinyima na kutunza kipande kimoja cha dhahabu?”

‘‘Inaonekana hivyo.”

“Hivyo inamaana utahitaji kufanya kazi na kujinyima kwa miaka hamsini ili uweze kutunza vipande hamsini vya dhahabu. Kufanya kazi maisha yako yote!

“Fikiria hili, unaweza kumruhusu dada yako ahatarishe akiba yako uliyoifanyia kazi kwa miaka hamsini? Ukiungua kwenye tanuri la kuyeyusha shaba halafu mume wake aende kuitumia kujaribu kuwa mfanyabiashara?”

“Siwezi kwakweli.” Alijibu Rodan kwa msisitizo.

“Basi nenda na kamwambie kuwa: ‘Nimefanya kazi kwa miaka mitatu mfululizo isipokuwa siku za mfungo tu. Toka asubuhi hadi usiku nimefanya kazi, nimejinyima vitu vingi nilivyotamani ili niweze kutunza kipande kimoja cha dhahabu kwa mwaka. Wewe ni dada yangu mpendwa, na ningependa mume wako aanze kufanya biashara na kufanikiwa. Sasa naomba uniletee mpango wake wa biashara yake ili rafiki yangu Mathon auchunguze kama ni mzuri na unatekelezeka. Kama upo sawa nitamkopesha akiba yangu ya mwaka mmoja na kumpa nafasi ya kuonyesha kama anaweza biashara.’ Fanya hivyo, kama kweli ana nia ya kufanikiwa atafanikiwa. Hata akishindwa, kiasi utakachokuwa umempatia ni kile ambacho anaweza kumudu kukulipa.

“Mimi nakopesha pesa kwasababu ninazo nyingi kuliko ninavyoweza kuzitumia katika biashara yangu. Nimeonelea pesa ya ziada ikafanyie kazi wengine na hivyo kuniletea faida. Sitaki kabisa kupoteza pesa yangu kwa sababu nimeifanyia kazi kwa bidii, na nimejinyima vitu vingi kuipata. Siwezi kumkopesha mtu ambaye sina uhakika kama ni salama na itarudi. Pia sikopeshi watu ambao najua watachelewa kunilipa.

“Nimekuambia siri za sanduku langu la dhamana. Umejifunza udhaifu wa binadamu na tamaa ya kukopa huku wakijua hawana njia ya kulipia. Kutokana na hilo umeona jinsi watu wanavyokuwa na matumaini ya kuwekeza na kupata kipato kikubwa iwapo wakipata pesa, lakini mara

nyingi huwa ni matarajio hewa tu. Hii ni kwa sababu wengi wao hawana uzoefu wala ujuzi wa kufikia malengo hayo.

“Wewe sasa una pesa, unatakiwa kuzifanyisha kazi ili zikuzalishie zaidi. Unaweza hata kuwa mkopesha pesa kama mimi. Ukitumia pesa yako vizuri itakuzalishia na kukufanya uishi maisha ya furaha na kuridhika siku zako zote. Lakini ukiiacha ipotee itakuwa ni chanzo cha uchungu na majuto maisha yako yote.

“Kitu gani unatamani kuhusiana na dhahabu yako?”

“Natamani kuitunza isipotee,” akajibu Rodan.

“Umejibu vyema,” akasema Mathon. “Jambo la kwanza ni usalama wa pesa yako. Fikiria ikiwa mikononi mwa shemeji yako, itakuwa salama kama unavyotaka?”

“Nadhani haiwezi maana shemeji yangu si mwenye hekima katika utunzaji wa pesa.”

“Basi usiyumbishwe na huruma za kijinga kuwa una wajibu wa kuwasaidia wengine, na hivyo ukagawa hazina yako. Kama unataka kuwasaidia jamaa zako, au watu wa ukoo wako tafuta njia nyingine lakini si kuhatarisha hazina yako. Kumbuka kuwa pesa hupotea kwa njia isiyotegemewa kutoka kwa wale wasio na uzoefu wa kuitunza. Ni bora kupoteza pesa kwenye anasa na starehe kuliko kuwapa wengine waipoteze.

“Baada ya kuhakikisha usalama wa pesa zako, nini kinafuata?”

“Kuifanya izalishe,” akajibu Rodan.

“Umejibu vyema pia. Inatakiwa izalishe na kukua. Pesa ikikopeshwa kwa hekima inaweza kukua na kuwa mara mbili

hata kabla ya kuwa mzee. Ukiiweka katika hatari ya kupotea unakuwa unahatarisha si tu pesa hiyo, bali hata kile ambacho ingezalisha.

“Kwa hiyo Rodan, usidanganywe na mipango kabambe isiyotimizika, mipango inayotolewa na watu ambao wanafikiri wana ujuzi wa kuifanya pesa izalishe kiasi kikubwa sana. Hiyo ni mipango ya waota ndoto ambao hawajui kanuni za biashara. Usitarajie kupata faida kubwa kuliko kawaida. Kukopesha au kuwekeza kwa matarajio makubwa kupita kiasi ni kukaribisha hasara. Kuwapa watu pesa yako na kutegemea faida kubwa kupita kawaida ni kukaribisha hasara.

“Shirikiana na watu wenye uzoefu na waliofanikiwa. Acha pesa yako ilindwe na hekima na uzoefu wao. Pia wekeza kwenye miradi iliyojithibitisha kuwa ina faida.

“Kwa mtindo huo utaepuka hasara ambazo huwapata vijana wengi wapatapo pesa.”

Rodan alipoanza kumshukuru kwa ushauri wake, Mathon ni kama hakusikiliza, aliendelea kusema:

“Zawadi uliyopewa na mfalme inatakiwa kukufundisha hekima. Ukitaka kubaki na vipande vyako hamsini vya dhahabu, unatakiwa kuwa makini. Utavutiwa na vitu vingi na utapata ushauri mwingi sana. Utaambiwa fursa nyingi zinazodaiwa kutoa faida kubwa. Habari na hadithi kutoka kwenye sanduku langu la dhamanazinatakiwa kuwa onyo kwako. Kabla hujaruhusu pesa yako kutoka kwenye pochi

hakikisha utaweza kuirudisha. Kama utahitaji ushauri zaidi unaweza kurudi nami nitafurahi kukupatia.

‘‘‘Mwisho naomba usome nilichoandika. Chini ya mfuniko wa sanduku la dhamana. Maneno haya yana faida kwa mkopeshaji na mkopaji pia.

BORA TAHADHARI KIDOGO KULIKO MAJUTO MAKUBWA.

KUTA ZA BABELI

Mzee Banzar, shujaa mkongwe na shupavu wa enzi zake. Leo alikuwa amesimama akilinda njia ya kuelekea sehemu ya juu ya ukuta wa Babiloni. Huko juu, wanajeshi shupavu walikuwa wakipambana kulinda ukuta. Wakati ujao wa jiji hili kubwa na ule wa malaki ya wakazi wake ulikuwa mikononi mwao.

Nje ya ukuta kelele za majeshi ya wavamizi zilisikika, kelele za watu wengi sana. Vishindo vya maelfu ya farasi, na kelele zenye kutia uziwi za magogo ya kubomolea milango zilisikika zikipiga milango ya shaba.

Ndani ya milango walisimama wanajeshi waliotumia mikuki, walijiandaa wakiwa tayari kulinda lango iwapo milango ingebomolewa. Walikuwa ni wachache tu. Jeshi kubwa la Babiloni lilikuwa pamoja na mfalme wao, sehemu za mbali huko mashariki likipigana vita dhidi ya waelami. Hawakutarajia jiji lao kuvamiwa kipindi hiki hivyo waliacha kikosi kidogo kulinda jiji. Ghafla jeshi kubwa la waashuru lilishuka kutoka kaskazini. Kuta za jiji zilitakiwa kusimama au sivyo jiji la Babiloni lingeangamizwa.

Pembeni ya Banzar kulikuwa na umati mkubwa wa raia. Walikuwa na nyuso zilizopauka na zenye kujawa na uoga. Kwa shauku walikuwa wakiuliza habari za mwenendo wa vita.

Walikuwa kimya kwa mshangao huku wakiangalia msururu wa majeruhi na maiti wakitolewa njiani. Siku hiyo ndiyo ilikuwa siku ya pambano. Baada ya kuzingira jiji kwa siku tatu, ghafla adui akawa ameelekeza nguvu zake zote kwenye hili eneo na kwenye lango hili.

Walinzi waliokuwa juu ya ukuta Walipambana na maadui waliokuwa kwenye minara ya kupandia kuta, na wale waliopanda kwa ngazi. Walitumia mishale, mafuta yanayowaka na mikuki kwa wale maadui waliofika juu ya ukuta. Maelfu ya adui walirusha mishale mingi sana dhidi ya walinzi hao. Banzar alikuwa amekaa eneo ambalo alikuwa ni wa kwanza kupata habari kuhusu vita inayoendelea.

Mfanyabiashara mmoja mzee alimkaribia huku akitetemeka. "Niambie! Niambie!" Alimsihi Banzar,"Hawataweza kuingia. Wana wangu wako pamoja na mfalme. Hakuna wa kumlinda mke wangu mzee. Mali zangu watapora zote. Chakula changu pia, hawatatuacha na kitu chochote. Sisi ni wazee, hatuwezi kujilinda wala kuwa watumwa. Tutapatwa na njaa na kufa. Niambie kuwa hawataweza kuingia."

"Tulia ndugu yangu," akajibu Banzar. "Kuta za Babiloni ni imara. Rudi sokoni, na mwambie mke wako kuwa kuta zitamlinda na mali zenu zipo salama kama inavyolindwa hazina ya mfalme. Tembea pembeni ya kuta ili mishale inayorushwa isije kukupata."

Baada yam zee Yule kuondoka, mwanamke mmoja akiwa amebeba mtoto akamfuata.

“Sajenti, kuna habari gani toka huko juu ya ukuta? Niambie ukweli ili nikamwambie mume wangu. Yuko kitandani kwa homa iliyotokana na majeraha lakini anasisitiza kuvaa mavazi ya vita na kubeba mkuki ili anilinde, mimi ni mjamzito. Anasema maadui wakifanikiwa kuingia watalipa kisasi kwa ukatili wa kutisha.”

“Uwe na amani moyoni mama. Kuta za Babiloni zitakulinda wewe na wanao. Ni ndefu na imara. Husikii kelele za mashujaa wetu wanapokuwa wanamimina mafuta yanayowaka adui wanaopanda kuta kwa ngazi?”

“Nasikia hilo lakini pia nasikia sauti ya gogo likipiga lango la jiji.”

“Nenda kwa mumeo, mwambie milango ni imara na haitaweza kuvunjwa. Hata hao maadui wanaopanda ukutani hukutana na mikuki ikiwasubiri. Nenda kwa uangalifu. Na tembea pembeni ya majengo.”

Banzar alisogea pembeni ili kuruhusu kikosi cha jeshi kilichokuwa na silaha nzito kupita. Walipokuwa wakipita binti mmoja mdogo alimvuta mkanda na kusema.

“Askari naomba uniambie, tupo salama?” Aliuliza. “Nimesikia sauti za kuogopesha na naona watu wakivuja damu. Ninaogopa sana. Nini kitaipata familia yangu, mama yangu na wadogo zangu?”

Banzar akainama na kumsogelea yule ntoto.

“Usiogope mtoto mzuri,” alimhakikishia. “Kuta za Babiloni zitakulinda wewe na mama yako na wadogo zako. Malkia Semiramisi alizijenga hizi kuta miaka mia moja

iliyopita kwa ajili ya usalama wa watu kama wewe. Hakuna aliyewahi kuzipenya. Nenda na mwambie mama na wadogo zako kuwa kuta za Babeli zitawalinda na hawana sababu za kuwa na wasiwasi."

Siku baada ya siku, Banzar alisimama kwenye kituo chake akisalimia vikosi vikipanda juu ukutani. Walishuka walipokuwa wamejuruhiwa au wamekufa tu. Banzar alikuwa amezungukwa na raia wengi waliokuwa wamejawa na woga huku wakitaka kujua iwapo kuta zitahimili.

Kwa heshima aliwajibu wote kuwa,

"Kuta za Babiloni zitawalinda."

Kwa wiki tatu na siku tano mashambulizi yaliendelea bila kukoma. Sehemu aliyokuwa amekaa Banzar iligeuka matope kutokana na damu na wanajeshi kupita walipokuwa wanaenda juu ya ukuta, au walipokuwa wanajikokota kushuka. Kila siku maiti za wavamizi zilijazana nje ya ukuta. Usiku, wenzao walizitoa na kwenda kuzizika. Kwenye siku ya tano ya wiki ya nne vita iliendelea usiku kucha bila kukoma. Kulipopambazuka vumbi lililotimuliwa na adui aliyekuwa anaondoka lilionekana.

Walinzi wa kuta za jiji walipiga kelele kwa shangwe. Wanajeshi waliokuwa ndani nao wakapiga kelele, na raia vilevile. Jiji zima likashangilia. Watu walitoka majumbani mwao na mitaa ikajaa umati wa watu. Wasiwasi uliowajaa kwa wiki kadhaa ukageuka nyimbo za furaha. Kutoka kwenye mnara wa hekalu la Beli moto wa ushindi uliwashwa. Moshi ulipanda juu kupeleka taarifa hadi sehemu za mbali.

Kwa mara nyingine kuta za Babiloni zilikuwa zimemzuia adui mwenye nguvu. Adui aliyepanga kupora hazina yake, kutesa na kufanya watu wake kuwa watumwa.

Jiji la Babaliloni lilidumu karne na karne kwa sababu lilikuwa na ulinzi thabiti. Gharama ya kutojilinda ilikuwa ni kubwa sana kwake.

Kuta za Babiloni zilikuwa ni mfano bora juu ya tamaa ya kujilinda ya mwanadamu. Hii ni tamaa ya asili ya mwanadamu. Tamaa hiyo ina nguvu leo kama ilivyokuwa enzi za kale. Tofauti ni kuwa leo tuna njia bora za kuitimiza.

Leo tuna kuta zisizopenywa za bima, akaunti za akiba na miradi mingi salama tunayoweza kuwekeza. Leo tunaweza kujilinda dhidi ya majanga yasiyotarajiwa, yanayoweza kuingia katika nyumba zetu na kuweka makazi.

HATUWEZI KUIMUDU GHARAMA YA KUTOKUWA NA ULINZI WA KUTOSHA.

MUUZA NGAMIA WA BABELI

kadri mtu anavyopatwa na njaa ndivyo akili yake inavyofanya kazi zaidi. Pia ndivyo uwezo wake wa kunusa harufu ya chakula unavyoongezeka.

Hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa Tarkad mwana wa Azure. Kwa siku mbili alikuwa hajatia kitu chochote mdomoni zaidi ya tini mbili ndogo alizokuwa ameiba bustanini. Lakini kabla hajachuma tini nyingi zaidi, alitokea mwanamke mwenye hasira na kumfukuza hadi mtaani. Sauti yake kali bado ilikuwa inasikika masikioni mwa Tarkad alipokuwa anatembea sokoni. Ndiyo iliyomzuia kudokoa matunda yaliyokuwa yanauzwa kwenye vikapu sokoni.

Kabla ya leo alikuwa hajawahi kufikiria ni chakula kiasi gani huletwa kwenye masoko ya Babiloni, na jinsi kilivyo na harufu nzuri. Kutoka sokoni akaingia hotelini na kuanza kutembea tembea karibu na ukumbi wa kulia chakula. Aliwaza kuwa pengine hapa anaweza kuonana na mtu anayemfahamu ili akope pesa kidogo. Alijua kuwa hatakiwi pale kama hana pesa.

Akiwa bado amezama kwenye mawazo akajikuta anagongana uso kwa uso na mtu ambaye hakupenda kabisa kukutana naye, alikutana na mtu mrefu na mkakamavu,

Dabasir, muuza ngamia. Katika jamaa zake wote ambao amewahi kukopa pesa ndogondogo, Dabasir ndiye alimfanya ajihisi vibaya sana baada ya kushindwa kulipa.

Dabasir alipomuona Tarkad uso wake ukakunjuka kwa furaha. “Ha! Ni wewe Tarkad! Nimekuwa nakutafuta unilipe zile sarafu mbili nilizokukopesha mwezi uliopita, na kile kipande cha pesa nilichokukopesha kabla ya hapo. Bora tumekutana, nina shida nazo leo, unasemaje?”

Tarkad akapatwa na kigugumizi na uso ukamuumuka. Kwa njaa yake hakuwa na ujasiri wa kubishana na Dabasir. Dabasir alikuwa ni mtu wa kuongea bila kumung’unya maneno.

“Samahani, samahani sana,” alisema Tarkad kwa kubabaika na kinyonge. Hapa sina pesa ya kukulipa.’

“Basi kazitafute,” akasema Dabasir kwa msisitizo.

“Ina maana huwezi pata sarafu chache na kipande cha fedha ili kumlipa rafiki wa baba yako aliyekutendea wema ulipokuwa na shida?”

‘’ ’Nimeandamwa na bahati mbaya ndiyo maana nimeshindwa kukulipa.”

" ‘Bahati mbaya! Unawezaje kuilaumu Miungu kwa uzembe wako mwenyewe? Bahati mbaya huwapata wale wanaofikiria kukopa kuliko kulipa. Hebu nifuate maana nina njaa. Nataka kukusimulia kisa kimoja.”

Tarkad alifadhaishwa na jinsi Dabasir alivyokuwa anaongea bila kumung’unya maneno, lakini alimfuata na kufurahi kupata nafasi ya kuingia kwenye ukumbi wa

chakula. Walienda kwenye kona moja na kukaa kwenye zulia. Mmiliki wa hoteli ile, bwana Kauskori alipokuja huku akitabasamu Dabasir akamwambia. “We kenge mnene wa jangwani hebu niletee mguu mmoja wa mbuzi ulioiva vizuri, na pia mkate pamoja na mbogamboga zote ulizonazo, nina njaa sana. Pia usimsahau huyu rafiki yangu, mletee jagi la maji baridi maana joto ni kali sana leo.

Moyo wa Tarkad ukanyong’onyea. Yaani akae pale akinywa maji huku akimuangalia Dabasir akila mguu mzima wa mbuzi! Lakini hakusema kitu.

Dabasir hakuwa mtu wa kukaa kimya, alitabasamu na kuwapungia wateja wengine mikono. Karibu wote waliokuwemo mule alikuwa anajuana nao.

“Nimesikia habari fulani kutoka kwa msafiri mmoja aliyetoka Urfa hivi karibuni. Kanisimulia habari za tajiri mmoja ambaye alijenga nyumba, na kisha akakata mawe yaliyokuwa yanaangaza kama kioo na kuyaweka madirishani. Lakini mawe yale yalikuwa ya manjano, na ukiangalia nje kupitia dirishani unaona dunia ikiwa na rangi tofauti kabisa.

“Unasemaje kuhusu hili Tarkad, yaani dunia yote ionekane kwa rangi tofauti na ile ya asili?

“Sina la kusema,” akajibu Tarkad huku mawazo yake yakiwa kwenye ule mguu wa mbuzi ulionona mbele ya Dabasir.

“Mimi nimeamini. Sababu mi mwenyewe nimewahi kuiona dunia ikiwa na rangi tofauti. Kisa nitakachokusimulia

kinahusu jinsi nilivyoweza kuiona dunia kwa rangi yake halisi tena."

"Dabasir ana kisa anataka kusimulia." Alisema mtu mmoja aliyekuwa anakula pembeni yao akiwaambia wengine mule mgahawani. Alisema huku akisogeza zulia lake. Wale wengine nao wakasogea na kutengeneza nusu duara. Walisogea na vyakula vyao, ni Tarkad pekee ndiye ambaye alikuwa hana chakula. Alitamani sana lakini Dabasir hakumkaribisha.

"Kisa ninachotaka kusimulia." Alianza kusema Dabasir huku akiendelea kula mguu wa mbuzi. "Kinahusiana na nilivyoanza maisha na jinsi nilivyokuja kuwa mfanyabiashara wa ngamia. Kuna mtu anajua kuwa zamani nilikuwa mtumwa huko Siria?"

Kusikia hivyo watu wote wakaanza kunong'ona kwa mshangao.

"Nilipokuwa kijana," akaendelea Dabasir baada ya kukata kipande kikubwa cha nyama."Nilijifunza kazi ya baba yangu, kutengeneza matandiko ya wanyama. Nilifanya kazi kwenye karakana yake na baada ya muda nikaoa. Sababu nilikuwa kijana na sikuwa na ujuzi mkubwa kipato changu kilikuwa kidogo, lakini kilitosha kumtunza mke wangu. Nilitamani vitu vizuri lakini sikuwa na jinsi ya kuvipata. Nikagundua kuwa wafanyabiashara walikuwa tayari kunikopesha nami niwalipe baadaye.

"Kutokana na kukosa uzoefu, sikujua kuwa yule anayetumia kuliko pato lake anakuwa anapanda mbegu ya

upepo wa matumizi yasiyo na lazima. Upepo ambao mavuno yake ni kimbunga cha matatizo na aibu. Nilizama kwenye matumizi kwa kukopa nguo nzuri na kumnunulia mke wangu vitu vya anasa. Nyumba yetu tukajaza vitu vya anasa. Tulikopa na kutumia kuliko uwezo wetu.

"Mwanzo niliweza kulipa bila tatizo lolote, lakini siku zilivyoenda nikaona kuwa pato langu halitoshi kuishi na kulipa madeni. Wakopeshaji wakaanza kunifuatilia nilipe madeni na maisha yangu yakaanza kuwa machungu. Nilikopa kwa rafiki zangu lakini nao sikuweza kuwalipa. Maisha yakawa mabaya kabisa. Mke wangu akarudi kwao na mimi nikaamua kutoroka Babiloni na kwenda kuishi mji mwingine.

"Nikapata kazi kwenye msafara wa wafanyabiashara, nikafanya kazi kwa miaka miwili. Maisha yalikuwa magumu na ya kutangatanga. Baaadaye nikaacha kazi na kujiunga na kundi la waporaji waliokuwa wakitangatanga jangwani kuvamia misafara isiyo na ulinzi. Kwa jinsi baba yangu alivyonilea sikupaswa kufanya matendo yale lakini sikuona aibu. Nilikuwa naiona dunia kupitia kioo chenye rangi, sikutambua jinsi nilivyokuwa nimepotea.

"Kwenye kazi yetu ya kwanza tulipata mafanikio. Tulipora dhahabu nyingi, hariri na vitu vingine vya thamani. Tulienda Ginir na kutapanya mali yetu yote.

"Mara ya pili bahati haikuwa upande wetu. Tulipokuwa tumemaliza kupora, ghafla tukaanza kushambuliwa na mikuki kutoka kwa watu wa chifu wa eneo lile. Misafara ilikuwa inamlipa chifu yule kwaajili ya ulinzi. Viongozi wetu

wawili waliuwawa na tuliobaki tulichukuliwa hadi Damasko. Huko tulivuliwa nguo zetu na kuuzwa kama watumwa.

“Mimi nilinunuliwa na chifu mmoja wa jangwani kwa vipande viwili vya fedha. Nilinyolewa nywele na kupewa nguo ya kuziba uchi tu kama watumwa wengine. Kwasababu nilikuwa kijana nisiyejali niliona kama mchezo tu. Lakini hilo lilibadilika ghafla pale yule chifu alipo nipeleka kwa wake zake na kuwauliza iwapo wanahitaji towashi. Hapo ndipo nikagundua nipo kwenye hali mbaya.

“Kwa uoga mkubwa nilisimama huku wale wanawake wakinichunguza. Kichwani nikiwaza iwapo watanionea huruma. Aliyeanza kunikagua alikuwa ni mke mkubwa, Sira. Alinikagua bila kusema lolote, sikujua ameamua nini.

“Wa pili kunikagua alikuwa mwanamke mzuri sana ambaye aliniangalia kwa dharau kama vile nilikuwa mnyoo tu. Wake zake wadogo wawili walinikagua kama vile nilikuwa kichekesho tu.

“Nilikaa nikisubiri hukumu yangu, ulionekana kama ni muda mrefu sana. Ilionekana kama wanawake wale wanategeana kutoa majibu. Mwishowe Sira alisema.

" ‘Matowashi tunao wengi wa kutosha, lakini hatuna watunza ngamia wa kutosha. Wachache tulionao hawaijui kazi yao vizuri. Hata leo ningependa kumtembelea mama yangu ambaye ni mgonjwa lakini sioni mtumwa wa kuongoza ngamia vizuri. Muulize huyu kama anaweza kuongoza ngamia.’

“Bwana wangu akaniuliza, ‘Unajua nini kuhusiana na ngamia?’

“Nilijikaza nisionyeshe furaha yangu, nikajibu. Naweza wafanya wapige magoti, naweza kuwapakia na naweza kuwaongoza kwenye safari ndefu bila kuchoka. Pia ikihitajika, naweza kurekebisha matandiko yao na kamba za kuwafunga.

" ‘Huyu mtumwa anaonekana anauelewa. Kama unaona anafaa mchukue awe mtunza ngamia wako.’

“Hivyo nikawa mtumwa wa Sira, na siku hiyohiyo niliongoza ngamia wake kwenda kumuona mama yake. Nilitumia muda huo kumshukuru kwa kuniokoa dhidi ya kuhasiwa. Nikamueleza kuwa mimi sikuzaliwa mtumwa bali ni mtoto wa mtu-huru, mtengeneza matandiko huko Babiloni. Pia nikamsimulia hadithi ya maisha yangu. Majibu yake hayakuwa ya kufariji na yaliniacha na maswali mengi.

'' ‘Unawezaje kujiita mtu huru iwapo udhaifu wako umekutumbukiza kwenye hali kama hii? Mtu kama akiwa na roho ya utumwa atakuwa mtumwa tu hata akizaliwa wapi na nani. Maji si hufuata mkondo? Kama mtu ana roho ya mtu-huru, je hataheshimiwa katika jiji lake hata kama hana utajiri?

“Nilikuwa mtumwa kwa mwaka mmoja na niliishi na watumwa wengine lakini sikuweza kuwa mmoja wao. Siku moja Sira aliniuliza, ‘watumwa wengine wanachangamana pamoja na kufurahi, kwanini wewe hukaa peke yako hemani?’

“Nafikiria ulichoniambia. Nafikiria iwapo nina roho ya utumwa. Siwezi kuchangamana nao hivyo nimeamua kukaa peke yangu.’

‘' ‘Hata mimi muda mwingi hukaa peke yangu,’ aliniambia. Mahari yangu ilikuwa kubwa sana. Na bwana wangu alinioa sababu ya thamani yangu, lakini hanitamani tena. Takwa kubwa la mwanamke ni kutamaniwa. Lakini sababu ya hilo na sababu ya kutopata mtoto imenibidi kujitenga. Ningekuwa mwanaume ningekubali kufa kuliko kuwa mtumwa, lakini desturi yetu kwa mwanamke kuwa mtumwa ni jambo la kawaida.

‘' ‘Wewe kwani unanionaje’ nilimuuliza. ‘Je, nina roho ya mtu-huru au roho ya mtumwa?’

‘' ‘Una mpango wa kulipa madeni unayodaiwa huko Babeli?’ alinihoji.

‘' ‘Nina nia ya kulipa madeni yangu lakini sina jinsi,’

‘' ‘Kama miaka imepita na ulikuwa ukizurura tu, bila kufanya jitihada yoyote kulipa madeni yako wewe ni mtumwa wa hali ya chini kabisa. Mtu anayejiheshimu lazima atalipa madeni yake.

‘' ‘Nitafanya nini kulipa madeni yangu na mimi ni mtumwa huku Siria?’

‘' ‘Endelea kuwa mtumwa ewe mtu dhaifu!’

‘' ‘Mimi siyo mtu dhaifu,’ nilipinga vikali.

‘' ‘Thibitisha kama kweli wewe siyo dhaifu,’

‘' ‘Nitathibitishaje sasa?’

" ‘Je, mfalme wako wa Babeli hapigani na maadui kutoka kila upande akitumia kila njia na jeshi lake lote? Madeni yako ndiyo adui zako. Ndiyo yaliyokukimbiza kutoka Babiloni. Uliyaacha na yamekuwa na nguvu kukuzidi. Kama ungepambana nayo kiume ungeyashinda na ungekuwa mtu wa kuheshimika. Lakini hukuwa na moyo wa kupambana, na tazama umekuwa mtu wa chini hadi kuwa mtumwa hapa Siria.

“Nilitafakari maneno yake makali. Nilifikiria maneno ya kumjibu kumuonyesha kwamba mimi sina roho ya utumwa, lakini sikuweza kusema chochote. Siku tatu baadaye kijakazi wake alinifuata na kuniambia kuwa ninaitwa na Sira.

‘' ‘Mama yangu ni mgonjwa tena,’ aliniambia Sira. ‘Andaa ngamia wawili wenye afya bora. Wapakie maji na mahitaji mengine kwaajili ya safari ya siku nyingi. Kijakazi wangu atakuandalia mahitaji yote kwaajili ya safari.’

“Nilipakia vitu kwenye ngamia nikistaajabu jinsi vilivyokuwa vingi. Mama yake Sira aliishi umbali wa siku moja tu lakini kijakazi aliandaa vitu vingi sana. Wakati wa safari kijakazi alipanda ngamia wa nyuma nami nilikuwa mbele nikiongoza ngamia wa Sira. Tulipofika nyumbani kwa mama yake tayari usiku ulikuwa umeingia. Baada ya kumuondoa kijakazi wake Sira aliniambia.

‘' ‘Dabasir wewe una roho ya mtu-huru au roho ya mtumwa?”

‘' ‘Nina roho ya mtu huru,’ nilijibu kwa msisitizo.

'' 'Sasa ndiyo nafasi yako ya kuthibitisha hilo. Bwana wako amelewa na machifu wake hawajitambui. Chukua hawa ngamia na utoroke. Chukua na hizi nguo za bwana wako ili usijulikane. Nitasema kuwa uliiba ngamia na kutoroka nilipoenda kumuona mama,'

'' 'Hakika wewe una roho ya malkia,' nilimwambia. Natumaini utapata furaha maishani mwako.

" 'Furaha! Alijibu, 'Furaha haimsubiri mke mtoro anayeitafuta kwenye nchi ya mbali katikati ya watu wageni. Nenda zako na Miungu ya jangwani ikulinde. Safari yako ni ndefu na huko utakopita hakuna chakula wala maji.'

"Sikuhitaji kuhimizwa zaidi. Nilimshukuru sana na nikatokomea gizani. Sikuijua vizuri hii nchi hivyo nilikisia tu upande ambao mji wa Babiloni ulikuwako. Nilisonga kwa kujiamini nikikatiza jangwani kuelekea kwenye vilima vya mbali. Nilipanda ngamia mmoja na mwingine nilimfunga akifuata nyuma. Nilisafiri usiku kucha na kesho yake yote bila kusimama. Hofu ya juu ya kinachowapata watumwa wanaoiba mali za mabwana wao na kutoroka ilinisukuma mbele.

"Mchana wa siku ya pili nilifika kwenye nchi ya mawe mengi na kame sana. Mawe yale makali yaliwaumiza ngamia miguu hivyo walianza kutembea polepole na kwa taabu. Sikukutana na watu wala wanyama, lilikuwa ni eneo pweke sana.

"Ilikuwa safari ngumu sana, ni watu wachache wanaoweza kupona safari kama ile. Siku baada ya siku tulisonga mbele. Chakula na maji vilituishia na jua katili

lilitupiga. Katika siku ya tisa ya safari, nilidondoka kutoka juu ya ngamia na sikuwa na nguvu ya kupanda tena. Nilijua kuwa mwisho wangu unefika, kifo katika nchi ya ukiwa.

"Nilijinyoosha na kulala mpaka kulipopambazuka, ngamia wangu walikuwa wamekaa mbali kidogo, wakionekana kama wenye huzuni sana. Eneo lililonizunguka lilikuwa ni miamba na jangwa tupu. Vichaka vya miiba vilionekana hapa na pale lakini hakukuwa na kitu cha kula wala maji ya kunywa. Hakuna cha kufaa binadamu wala ngamia.

"Inamaana huu ndiyo mwisho wangu? Kifo cha bila kelele na cha amani!" Niliwaza.

"Niliangalia lile jangwa katili lililokuwa mbele yangu kisha nikajiuliza tena, 'Nina moyo wa mtumwa au moyo wa mtu-huru?' Hapo nikagundua kuwa; iwapo nina moyo wa mtumwa basi nitakata tamaa, nitajilaza na kufa. Kifo kimfaacho mtumwa mtoro.

"Lakini iwapo nina moyo wa mtu-huru natakiwa kufanya nini? Hakika nitapambana kurudi Babiloni. Nitalipa wote wanaonidai, nitarudisha furaha ya mke wangu anayenipenda kwa dhati. Pia nitafanya wazazi wangu wajivune kuwa na mtoto kama mimi. Sira alisema, 'Madeni yako ndiyo adui zako waliokufanya ukimbie Babiloni,' maneno yake yalikuwa kweli tupu. Kwanini sikubaki na kupambana kiume na adui huyo? Kwanini niliruhusu mke wangu kurudi kwao?

"Ghafla kitu cha ajabu kikanitokea, dunia yote ilionekana kama ina rangi tofauti kabisa. Ni kama siku zote nilikuwa

naiangalia kupitia kioo chenye rangi na sasa kimeondolewa. Niliona thamani halisi ya maisha.

" ‘Nife jangwani! Hapana hata kidogo,’ nikapata mwanga mpya, nikatambua ninalotakiwa kufanya. Kwanza natakiwa kurudi Babiloni na kuonana na kila anayenidai. Nitawaambia kuwa nimerudi kuwalipa baada ya miaka mingi ya kutangatanga na taabu. Nitawalipa haraka kadri Miungu itakavyonijalia. Baada ya hapo nitatafuta nyumba kwaajili yangu na mke wangu, nitakuwa raia mwema ambaye wazazi wangu watajivunia.

“Madeni yangu ndiyo yalikuwa adui zangu’ lakini wale walionikopesha walikuwa ni rafiki zangu. Waliniamini na walikuwa hawana shaka nami.

“Nilijikaza na kusimama. Sikujali njaa wala kiu, hayo yalikuwa ni mapito tu katika safari ya kurudi Babiloni. Roho ya mtu-huru ikanijaa, mtu anayeenda kushinda adui zake na kurudisha furaha ya rafiki zake. Nilipandwa na mori mkubwa sana.

“Baada ya ngamia wangu kujitahidi kwa mara kadhaa waliweza kusimama. Kwa uvumilivu wakaanza kusonga polepole kuelekea kaskazini, nilikuwa nina hisia huo ndiyo uelekeo wa Babiloni.

“Baada ya kusafiri kwa muda tukafika nchi tuliyopata maji, nyasi na matunda. Mwishowe tukaikuta barabara inayoelekea Babiloni. Moyo wa mtu-huru huona maisha ni kama msururu wa changamoto zinatakiwa kutatuliwa, lakini

moyo wa mtumwa huishia kunung'unika, 'sina la kufanya mimi ni mtumwa tu!"

"Vipi kuhusu wewe Tarkad, njaa yako haifanyi kichwa chako kifanye kazi zaidi? Je, upo tayari kuanza safari ya kurudi kwenye maisha ya kujiheshimu? Unaweza kuiona dunia kwa rangi yake halisi? Je una nia ya dhati ya kulipa madeni yako hata kama ni makubwa kiasi gani? Unataka kuwa mtu unayeheshimika tena?

Machozi yakamlengalenga Tarkad. Akapiga magoti na kusema. "Umenionyesha mwanga mpya, tayari nahisi roho ya mtu-huru ikiwa ndani yangu."

"Uliporudi Babiloni maisha yalikuwaje?" Aliuliza msikilizaji mmoja.

"Penye nia pana njia," alijibu Dabasir. "Nilikuwa na nia hivyo nikaanza kutafuta njia. Kwanza nilimtafuta kila aliyekuwa akinidai na kumuomba anivumilie mpaka nitakapoweza kumlipa. Wengi wao walinipokea kwa furaha sana na wachache walinishutumu. Lakini pia kati yao walitokea waliokuwa tayari kunisaidia.

"Mtu mmoja alinipa msaada niliouhitaji sana, alikuwa ni Mathon mkopesha pesa. Alipofahamu kuwa nilipokuwa Siria nilifanya kazi ya kutunza Ngamia, akaniagiza kwenda kwa mfanyabiashara wa ngamia aliyeitwa Nebaturi. Nebaturi alikuwa amepewa kazi na mfalme ya kununua ngamia bora kwa ajili ya safari za uvumbuzi. Nilitumia ujuzi wangu kumsaidia kupata ngamia bora. Polepole nikaanza kulipa

madeni yangu. Mwishowe nikaweza kuinua kichwa na kujiona mtu kati ya watu.

Baada ya kusema hayo Dabasir akageukia chakula chake na kuita kwa sauti kubwa ambayo ilisikika hadi jikoni. “Kauskori! Konokono mkubwa wewe! Chakula kimepoa, niletee nyama nyingine ya moto. Pia mletee na Tarkad kipande kikubwa cha nyama. Huyu ni mwana wa rafiki yangu, nitakula naye”

Hivyo ndivyo hadithi ya Dabasir ilivyoisha, hadithi ya mfanyabiashara wa ngamia wa Babeli. Alijitambua mara alipoona ukweli wa mambo. Ukweli ambao watu wenye hekima waliujua zamani za kale kabla yake. Ukweli huo uliwaongoza watu wa vizazi vyote kutoka kwenye taabu hadi kwenye mafanikio, na utaendelea kufanya hivyo kwa wale wenye hekima ya kutambua nguvu zake za ajabu. Mtu yeyote anayesoma maneno yafuatayo anaweza kuyatumia.

PENYE NIA PANA NJIA.

MABAMBA YA VIGAE KUTOKA BABELI

CHUO CHA MTAKATIFU SWITHIN
Chuo kikuu cha Nottingham.
Newark-on-Trent,
Nottingham.

Profesa Franklin Caldwell,
Msimamizi wa tafiti za kisayansi za Uingereza,
Hillah, Mesopotamia,
Oktoba 21, 1934.

Mpendwa Profesa:

Mabamba matano ya vigae uliyoyachimbua kwenye magofu ya Babiloni hivi karibuni yamewasili pamoja na barua yako. Nimevutiwa nayo na nimetumia muda mwingi nikitafsiri maandishi yake. Ningejibu barua yako mapema lakini nilitaka nimalize kuyatafsiri kwanza. Nimeambatanisha tafsiri hizo.

Mabamba yalifika bila kuharibika. Nashukuru kwa kuyafunga kwa uangalifu, na kwa kuweka dawa ya kuyahifadhi.

Utashangazwa kama tu sisi tulivyoshangazwa na habari zilizoandikwa humo. Mtu anaweza kutegemea habari za kale kuzugumzia mambo ya mapenzi, na hadithi za safari za mbali za kufikirika, hadithi kama "Alfu lela ulela" na kadhalika. Badala yake yanazungumzia matatizo ya mtu aliyeitwa Dabasir. Matatizo yanayohusiana na kulipa madeni yake. Mtu akisoma atagundua kuwa kwa kipindi cha miaka elfu tano dunia haijabadilika kama mtu anavyoweza kutarajia. Ni jambo la ajabu lakini limenipa hasira sana. Kwa kuwa mimi ni profesa wa chuo kikuu, natarajiwa kuwa na uelewa juu ya vitu karibu vyote. Nashangaa mtu kutoka kwenye mavumbi ya magofu ya Babiloni anaanza kunishauri jinsi ya kulipa madeni, na namna ya kujiongezea kipato! Maarifa mageni kabisa kwangu.

Lakini nikiri kuwa ushauri wake unavutia na unafaa kujaribiwa, inahitajika kuona iwapo unafanya kazi leo kama ilivyokuwa katika Babiloni ya kale. Mimi na mke wangu tumepanga kujaribu kutumia yale yaliyoandikwa humo kwenye maisha yetu. Tunatarajia maisha yetu yataboreka.

Nakutakia baraka nyingi kwenye kazi yako ya maana unayoifanya na ninasubiri kwa hamu na nitafurahi kuwa msaada kwa wakati mwingine.

Wako mtiifu,

Alfred H. Shewrbury.

Idara ya akiolojia.

BAMBA NAMBA MOJA

Mimi Dabasir, niliyerudi hivi karibuni toka utumwani Siria. Nikiwa na nia ya kulipa madeni yangu yote na kuwa mtu wa maana katika Babiloni. Kwenye bamba hili la kigae ninaandika kumbukumbu la maisha yangu, nataka kumbukumbu hili liniongoze na kunisaidia katika kufikia malengo yangu.

Chini ya ushauri wa rafiki yangu Mathon mkopesha pesa. Nimedhamiria kufuata mbinu aliyoniambia, mbinu ya kumtoa mtu mwenye nia kutoka kwenye madeni, na kumfanya awe mtu wa maana. Mbinu hiyo inahusisha malengo makuu matatu, malengo ambayo natamani sana kuyatimiza na ndiyo tumaini langu. Malengo yenyewe ni haya yafuatayo.

Kwanza; kuwa na kipato na kwaajili ya wakati ujao:

Hivyo basi, moja ya kumi ya pato langu nitaitunza kama yangu mwenyewe. Mathon alisema maneno haya ya hekima:

"Mtu anayetunza dhahabu na fedha kwenye pochi yake ni mtu mwema kwa familia yake, na kwa mfalme wake pia.

"Mtu ambaye hana kitu kwenye pochi yake zaidi ya senti chache tu, hudharaulika na familia yake na hudharaulika na mfalme pia.

"Mtu ambaye hana kitu chochote kwenye pochi yake ni asiyejali familia yake, na aliyekosa uaminifu kwa mfalme wake. Huyo ni mtu katili.

"Kwa hiyo, mtu anayetamani kufanikiwa ni lazima awe na pesa mfukoni mwake. Huyo ndiye anayeipenda familia yake na ni muaminifu kwa mfalme wake."

Mbili; mbinu hiyo ilinitaka lazima kutimiza mahitaji ya mke wangu ambaye kwa sababu ya kunipenda amerudi kutoka kwao.

Mathon anasema kuwa, kumtunza mke wako vizuri ni jambo litakalokuletea heshima, na linalokupa nguvu za kutimiza malengo yako.

Kwahiyo, saba ya kumi ya pato langu inatakiwa kutumika kwa matumizi ya nyumbani. Matumizi ya nguo, chakula na starehe kidogo sababu ni muhimu kufurahia maisha. Lakini alinionya kutotumia zaidi ya sehemu ya saba ya pato langu kwa matumizi ya nyumbani.

Mpango huo nimepanga kuutimiza kama ifuatavyo: Lazima niishi kwa kutumia saba ya kumi ya pato langu na si zaidi, na wala sitakiwi kununua kitu ambacho kitanifanya nitumie zaidi.

BAMBA NAMBA MBILI

Tatu; mbinu hiyo inanitaka kulipa madeni yangu kutokana na kipato changu.

Kwa hiyo, kila mwisho wa mwezi nilitenga mbili ya kumi ya pato langu kwaajili ya kuwalipa wale waliokuwa wananidai. Baada ya muda fulani nitakuwa nimelipa madeni yangu yote. Kwahiyo ninaandika kwenye bamba hili majina ya watu wote wanaonidai na kiasi wanachonidai.

Fahrul, mshona nguo, vipande 2 vya fedha na vipande 6 vya shaba.

Sinjar, mtengeneza makochi, kipande kimoja cha fedha.

Ahmari, Rafiki yangu, vipande 3 vya fedha na kipande 1 cha shaba.

Zankari, rafiki yangu, vipande 4 vya fedha na vipande 7 vya shaba.

Askamir, rafiki yangu, kipande kimoja cha fedha na vipande 3 vya shaba.

Harinsir, sonara, vipande 6 vya fedha na vipande 2 vya shaba.

Diabeka, rafiki wa baba yangu, vipande 4 vya fedha na kipande 1 cha shaba.

Alkahadi, baba mwenye nyumba, vipande 14 vya fedha

Mathon, mkopesha pesa, vipande 9 vya fedha

Birejiki, mkulima, kipande kimoja cha fedha na vipande 7 vya shaba

(Kwa bahati mbaya kufika hapa bamba lilikuwa limeharibika na sikuweza kutafsiri zaidi.)

BAMBA NAMBA TATU

Kwa ujumla watu hao wananidai vipande miamoja na kumi na tisa vya fedha, na vipande miamoja na arobaini na moja vya shaba. Kwa sababu ya deni hilo na baada ya kuwa sina namna ya kulilipa, nikaamua kumruhusu mke wangu arudi kwao na mimi nikakimbia mji. Huko nilitumbukia kwenye matatizo na kuishia kwenye aibu ya kuuzwa utumwani.

Sasa baada ya Mathon kunionyesha namna ninavyoweza kulipa madeni yangu, ndipo nimegundua kosa langu la kukimbia madeni yaliyotokana na anasa zangu. Kwa hiyo, nimewatembelea watu wote wanaonidai na kuwaeleza kuwa sina pesa ya kuwalipa kwa sasa lakini nitafanya kazi na kuwalipa.Nimewaambia kuwa nitatumia mbili ya kumi ya pato langu kulipa madeni yao, hicho ndicho kiasi ninachoweza

kutenga. Hivyo, naomba uvumilivu wao na baada ya muda nitakuwa nimelipa madeni yote.

Ahmari ambaye nilifikiri alikuwa rafiki yangu wa karibu alinisema vibaya. Birejiki, yule mkulima alisema nianze kumlipa yeye kwanza sababu alikuwa na shida sana.

Alkahadi, baba mwenye nyumba wangu alikataa katakata. Alisema kuwa atanichukulia hatua iwapo sitamlipa deni lake lote.

Wengine wote walinikubalia. Sasa nina dhamira kabisa ya kulipa madeni yangu, nimegundua ni rahisi kulipa madeni kuliko kuyakimbia. Japo siwezi kutimiza matakwa ya wote wanaonidai, lakini nimepanga kwenda nao taratibu na kwa uvumilivu.

BAMBA NAMBA NNE

Ni mwezi mmoja umepita. Nimefanya kazi kwa bidii sana. Mke wangu amenitia moyo kutimiza lengo langu la kulipa madeni yangu. Nimefanikiwa kumuuzia Nebaturi ngamia bora kabisa, nimepata vipande kumi na tisa vya fedha.

Hivi nimetumia pesa hizo kama nilivyopanga. Moja ya kumi nimeweka akiba. Saba ya kumi tumeitumia mimi na mke wangu kwa matumizi ya nyumbani. Mbili ya kumi nimeigawanya na kuwalipa wanaonidai kidogokidogo, kila mmoja kulingana na kiwango anachonidai.

Sikumkuta Ahmari lakini nilimuachia mke wake pesa yake. Birejiki alifurahi sana hadi akataka kunibusu mikono. Ni Alkahadi tu ndiye aliyenuna na kusema kuwa natakiwa kumlipa

haraka. Nikamwambia kuwa iwapo nitaachwa nilipe kwa amani na kubaki na kiasi kwaajili ya chakula nitaweza kulipa haraka. Wengine wote walinishukuru na kunipongeza kwa jitihada zangu.

Kwa hiyo ndani ya mwezi mmoja nimepunguza deni langu kwa kiasi cha vipande vinne vya fedha. Pia nimeweza kuweka akiba karibia vipande viwili vya fedha. Ninahisi moyo wangu ukiwa mwepesi, sijahisi namna hii kwa muda mrefu sana.

Mwezi mwingine umepita tena. Nimefanya kazi kwa bidii lakini sikufanikiwa sana. Niliweza kununua ngamia wachache tu. Nikifanikiwa kupata vipande kumi na moja tu vya fedha. Pamoja na hilo, mimi na mke wangu tumefanya kama tulivyopanga. Japo hatukuweza kununua mavazi mapya na tulikula mboga za majani tu.

Tulijilipa moja ya kumi ya vile vipande kumi na moja vya fedha. Nilishangaa sana baada ya Ahmari kufurahi na kunipongeza japo nilimlipa pesa kidogo tu. Birejeki naye alifurahi na kunipongeza.

Alkahadi alikasirika sana, lakini nilipomwambia kama hajaridhika anirudishie ile pesa niliyomlipa akawa mpole. Wengine waliridhika kama ilivyokuwa pale mwanzo. Mwezi mwingine ukawa umeisha na nafsi yangu ikawa na furaha sana.

Mwezi uliofuata nilifanikiwa kupata ngamia bora sana, nilipata vipande arobaini na mbili vya fedha. Mwezi huu mimi na mke wangu tulinunua viatu maana tulivyokuwa navyo viliisha, tulinunua nguo na tuliweza kula nyama na kuku.

Zaidi ya vipande nane vya fedha tulitumia kulipa madeni. Safari hii hata Alkahadi hakukasirika. Hii ni mbinu bora sana kwani inatutoa kwenye madeni na wakati huohuo inatusaidia kujenga utajiri.

Ni miezi mitatu imepita tokea niamue kuandika kwenye bamba hili. Kwa muda wote nimekuwa nikijilipa moja ya kumi ya ninachopata. Mimi na mke wangu tumetumia saba ya kumi ya pato hilo kwa mahitaji yetu, pia nimetumia mbili ya kumi kuwalipa wale wanaonidai. Kwenye pochi yangu nimefanikiwa kutunza vipande ishirini na moja vya fedha. Ninajivunia sana jambo hilo. Mke wangu anatunza nyumba yetu vizuri, inapendeza nasi tunafurahi kuishi pamoja.

Thamani ya mbinu hii haielezeki. Je, haijamfanya mtu aliyekuwa mtumwa kuwa mtu wa maana na kuheshimika?

BAMBA NAMBA TANO

Ni miezi kumi na miwili imepita toka niandike kwa mara ya mwisho. kulikuwa na mambo mengi lakini sijutii, mpaka sasa nimeweza kulipa madeni yangu yote. Leo ni siku ambayo mimi na mke wangu tunasherekea mafanikio yetu kwa karamu kubwa.

Mambo mengi yalitokea siku niliyoenda kulipa madeni yangu kwa mara ya mwisho. Ahmari aliniomba msamaha kwa maneno makali aliyokuwa amenitolea. Aliniambia kuwa mimi ni mmoja kati ya watu anaopenda sana kufanya nao urafiki.

Mzee Alkahadi hakuwa mtu mbaya kama nilivyofikiria. Aliniambia, "Hapo mwanzo ulikuwa kipande cha udongo mbichi

wa mfinyanzi. Mtu yeyote angeweza kukufanya atakavyo. Lakini sasa umekuwa kipande cha shaba, mtu wa maana. Kama ukihitaji kukopa pesa muda wowote usisite kuniona." Hakuwa peke yake aliyekuwa ameanza kuniheshimu. Wengine pia walianza kunizungumzia kwa namna tofauti. Mke wangu pia alianza kuniheshimu.

Mbinu ya Mathon ndiyo iliyoniletea mafanikio yale. Iliniwezesha kulipa madeni yangu na kuweka akiba. Wote wanaotaka kufanikiwa nawashauri kutumia mbinu hiyo. Kama iliweza kumfanya mtu aliyekuwa mtumwa kulipa madeni yake na kuanza kuweka akiba, basi si inaweza kumsaidia mtu yeyote kuwa huru?

Na mimi si kwamba nimemaliza kuitumia, la hasha! Ninatumaini kuwa iwapo nitaendelea kuitumia itanifanya kuwa tajiri.

Chuo cha mtakatifu Swithin
Chuo kikuu cha Nottingham
Newark-on-Trent
Nottingham.
Novemba 7, 1936.

Profesa Franklin Caldwell,
Msimamizi wa tafiti za kisayansi za Uingereza
Hillah, Mesopotamia,

Mpendwa profesa:

Iwapo katika uchimbuzi wako unaoendelea kwenye magofu ya Babiloni ukabahatika kukutana na mzimu wa raia wake mmoja wa kale. Mzimu wa Dabasir, mfanyabiashara ya ngamia, nakuomba kitu kimoja. Mwambie kuwa maandishi yake aliyoandika kwenye mabamba ya vigae miaka mingi iliyopita, yamewafikia wanazuoni wawili huku Uingereza. Umwambie kuwa wanazuoni hao wanashukuru sana kwa yale aliyoandika.

Pengine unakumbuka ahadi yangu niliyotoa nilipokuandikia mwaka mmoja uliopita. Nilikuambia kuwa mimi na mke wangu tumepanga kujaribu kutumia mbinu yake ya kujitoa kwenye madeni na kutunza pesa. Utakuwa ilihisi hali hali mbaya tuliyokuwa nayo, japokuwa tulijitahidi kuificha rafiki zetu wasijue.

Kwa miaka mingi tumekuwa kwenye aibu ya madeni mengi, na tumekuwa na wasiwasi kuwa pengine baadhi ya wafanyabiashara wanaweza sambaza habari zetu na kufanya nikimbie chuo kwa aibu. Tulijitahidi kulipa madeni yetu kadri ya kipato chetu lakini ilikuwa ni kazi ngumu sana. Pia tulilazimika kununua sehemu ambazo tungeweza kopeshwa hata kama bei ya vitu ilikuwa juu.

Maisha yetu yakawa kama ule mzunguko ambao kadri muda unavyoenda mambo yanazidi kuwa mabaya badala ya kuboreka. Tulikata tamaa. Hatukuweza kuhamia nyumba ya bei rahisi kwa sababu tuliyoishi tulikuwa na deni. Ilionekana kuwa hakuna kitu tunaweza kufanya ili kuboresha hali yetu.

Lakini tazama, akatokea mtu wako, mfanyabiashara wa ngamia kutoka Babiloni! Kaja na mbinu ya jinsi ya Kufanya na kutimiza kile tulichotamani kutimiza. Alitushawishi kutumia mbinu yake.

Tuliorodhesha madeni yetu yote kisha nikaenda kuyaonyesha kwa wote wanaotudai. Niliwaeleza ni jinsi gani itakuwa ngumu kuwalipa iwapo mambo yakiendelea kuwa kama yalivyo. Walijionea wenyewe ukubwa wa deni letu. Niliwawambia kuwa njia pekee ya mimi kuweza kuwalipa ni kutenga asilimia ishirini ya mshahara wangu kila mwezi, na kuwalipa kulingana na ukubwa wa deni la kila mmoja.

Kwa mtindo huo nitakuwa nimewalipa wote baada ya miaka miwili na kidogo. Niliwaambia kuwa kuanzia sasa tutanunua vitu kwa pesa taslimu, kwa njia hiyo nao kwa namna fulani watafaidika na ununuzi wetu.

Walikuwa watu waungwana sana. Mzee mmoja ambaye hutuuzia mbogamboga na matunda aliongea maneno ambavyo yaliwashawishi na wengine. “Kama mtanunua vitu kwa pesa taslimu na kuendelea kupunguza deni polepole ni jambo bora sana. Ni bora kuliko sasa ambapo hamjalipa deni kwa miaka mitatu.” Baada ya hapo nikakubaliana nao wote kuwa hawatatubugudhi iwapo tutakuwa tunatumia asilimia ishirini ya pato letu kulipa madeni. Baada ya hapo tukaanza kupanga mipango ya jinsi ya kuishi kwa kutumia ile asilimia sabini, huku tukiweka asilimia kumi kama akiba.

Kufanya mabadiliko lilikuwa zoezi la kuburudisha sana. Tulifurahia kupanga mambo kwa namna hii na ile ili

kuhakikisha tunaishi kwa kutumia asilimia sabini ya pato letu bila kutaabika. Tulianza na kodi ya nyumba, tukafanikiwa kupunguza kiasi fulani. Baadaye tukaangalia aina ya chai tunayokunywa , tukashangaa kugundua kuwa tunaweza kupata chai bora zaidi, tena kwa bei nafuu.

Ni habari ndefu, siwezi andika yote kwenye barua lakini zoezi lilikuwa jepesi kuliko tulivyofikiria. Tulifanikiwa kupanga bajeti yetu na tukawa na furaha sana. Kutoka hapo tulifanya matumizi yetu bila kuwa na madeni yoyote.

Kuhusu kuweka akiba kutoka kwenye asilimia kumi ya pato letu; tulifanikiwa kuweka.

Ni jambo la kufurahisha sana kuanza kutunza pesa bila kuhitaji kuzitumia. Kuna furaha kwenye kutunza pesa kuliko ilivyo kwenye kuzitumia.

Baada ya kutunza na kuridhika na kiwango tulichofikia tulipata wazo la mradi wenye faida. Tulipata mradi ambao tuliweza kuwekeza asilimia kumi ya pato letu la kila mwezi. Toka tumeanza kubadili mtindo wa maisha kuwekeza ndilo jambo lililotuburudisha sana. Ni jambo pekee ambalo tulilipia kwa kutumia pesa zetu taslimu.

Ni jambo la kufurahisha kuona uwekezaji wetu unakua kila siku. Nikistaafu kazi yangu ya kufundisha, uwekezaji huo utakuwa umekuwa pesa nyingi sana. Kiasi cha kutosha maisha yetu baada ya kustaafu.

Nimefanya yote hayo kwa kutumia pato lile lile nililokuwa napata toka zamani. Huwezi amini ila ndiyo ukweli. Tunalipa madeni yetu polepole na wakati huohuo uwekezaji wetu

unaongezeka, jambo la kushangaza, hali yetu ya kifedha ni nzuri kuliko hapo mwanzo. Nani anaweza kuamini kuwa tofauti kubwa hutokea kati ya mtu anayeishi kwa kufuata bajeti na yule anayeishi bora liende.

Mwishoni mwa mwaka ujao tutamaliza madeni yetu yote na tutakuwa na fedha zaidi kwaajili ya kuwekeza, na nyingine kwaajili ya kusafiri na kutalii.

Tumedhamiria kutoruhusu tena matumizi yetu kuzidi asilimia sabini ya pato letu.

Sasa utakuwa umeelewa kwanini tunahitaji kumshukuru huyo bwana. Mbinu yake imetutoa toka kuzimu ya duniani. Alijua kuwa mbinu yake inafanya kazi kwa sababu yeye mwenyewe aliitumia. Alitaka na wengine wafaidike na somo alilojifunza kwa uchungu. Hicho ndicho kilimfanya afanye kazi ngumu ya kuandika ujumbe wake kwenye mabamba haya. Ujumbe wake ni muhimu sana kwa watu walio kwenye matatizo ya kifedha, ni muhimu kiasi kwamba bado unafanya kazi miaka elfu tano tokea uandikwe.

Wako muaminifu,

Alfred H. Shrewsbury,

Idara ya akiolojia.

MTU MWENYE BAHATI KULIKO WOTE KATIKA BABELI

Mbele ya msafara alikuwepo Sharru Nada. Alikuwa ni mfanyabiashara mkubwa sana katika jiji la Babiloni. Alipenda kuvalia mavazi mazuri na ya kisasa. Pia alipendelea wanyama wazuri, na hata farasi aliyempanda alikuwa ni wa aina bora kabisa katika Arabia. Kwa kumuangalia mtu asingeweza kujua kuwa umri wake ulikuwa umesonga. Pia ilikuwa ni vigumu zaidi kugundua kuwa hakuwa na amani moyoni mwake.

Safari ya kutoka Damasko hadi Babiloni ilikuwa ni ndefu na yenye magumu mengi sana. Lakini hili silo jambo lililomhangaisha. Pia njiani kulikuwa na makabila katili ya waarabu wa jangwani. Hawa muda wote walikuwa wanatamani kupora misafara ya wafanyabiashara matajiri. Lakini hawa pia hakuwaogopa sababu alikuwa na walinzi wa kutosha.

Kilichomhangaisha ni kijana aliyekuwa kapanda farasi pembeni yake. Kijana huyu alikuwa ametoka naye Damasko, jina lake Hadan Gula. Hadan Gula alikuwa ni mjukuu wa mshirika wake wa siku nyingi katika biashara, Arad Gula. Moyoni alikuwa akihisi ana deni kwa Arad Gula, deni ambalo

alihisi asingeweza kulilipa kamwe. Alitamani kufanya kitu kumsaidia mjukuu wake lakini hakujua cha kufanya, na hasa ni kutokana na kijana mwenyewe.

Kila akiangalia hereni na pete alizoavaa yule kijana aliwaza, “Inakuwaje huyu anafikiri vito huvaliwa na wanaume lakini ni mkakamavu kama babu yake? babu yake hakuvaa na kujipamba namna hii.”

Pamoja na hayo bado akawa ameamua kumchukua na kumsaidia kujenga maisha yake. Baba yake alikuwa ametapanya mali zote zilizoachwa na babu yake.

Hadan Gula alimkatisha mawazo yake kwa kusema. “Kwanini unafanya kazi kwa kujitesa. Kwanini mara zote unasafiri na msafara wako wa biashara? Kwanini hupumziki na kufurahia maisha?”

Sharru Nada akatabasamu na kusema. “Kufurahia maisha? Ungekuwa wewe ndiyo mimi, ungefanya nini ili kufurahia maisha?”

“Ningekuwa tajiri kama wewe ningeishi kama mwana mfalme. Nisingejitaabisha kusafiri jangwani kwenye joto. Kila shekeli inayoingia ningeitumia kufurahia maisha. Ningevaa nguo za gharama na kujipamba kwa vito adimu. Hayo ndiyo yangekuwa maisha yangu, maisha matamu.”

Baada ya kusema na kusikia hayo wote wakacheka.

“Babu yako hakuvaa vito.” Alisema Sharru Nada kwa kushutumu lakini akaona si sawa, akabadili na kusema kwa utani. “Inamaana hautakuwa na muda wa kufanya kazi?”

“Kazi ni kwaajili ya watumwa,” alijibu Hadan Gula. Sharru Nada aliuma meno kwa hasira lakini hakusema neno. Waliendelea kusafiri kimyakimya hadi walipofika kwenye mteremko unaoelekea kwenye bonde pana sana. Hapa Sharru Nada alisimamisha farasi wake na kumuonyesha Hadan Gula bonde la kijani lililokuwa linaonekana kwa mbali. “Unaona lile bonde? Angalia kwa mbali utaona ukuta wa Babiloni, ule mnara ni mnara wa hekalu la Beli. Kama macho yako ni mazuri utaona moshi kutoka kwenye moto unaowaka daima juu ya mnara huo.

“Kwa hiyo pale ndiyo Babiloni? Siku zote nilitamani kuona mji tajiri zaidi duniani,” alisema Hadan Gula . Huu ni mji ambao babu yangu alianza kujenga utajiri wake. Kama angekuwa hai tusingekuwa tunahangaika.”

“Kwanini unataka roho yake ikae duniani kuliko muda uliopangwa? Wewe na baba yako mnaweza kuendeleza kazi yake nzuri.”

“Bahati mbaya sisi hatuna kipaji kama chake. Baba yangu na mimi hatujui siri ya utajiri wake.”

Sharru Nada hakujibu kitu bali alianza kuongoza farasi wake kwa uangalifu kushuka bondeni. Nyuma yao ulifuata msafara mkubwa uliokuwa ukitimua vumbi jekundu. Baada ya mwendo wakafika kwenye barabara ya kwenda Babiloni, wakaishika kuelekea kusini kupitia kwenye mashamba ya umwagiliaji.

Kulikuwa kuna wanaume watatu wakilima shambani. Sharru Nada aliwaangalia na kuhisi kama amewahi kuwaona

sehemu, jambo la ajabu kabisa! Yaani mtu apite shambani baada ya miaka arobaini na awaone watu walewale wakilima! Lakini kuna kitu kilikuwa kinamwambia ndiyo wale aliowaona miaka arobaini iliyopita. Mmoja kwa mikono isiyo na nguvu alikuwa ameshikilia jembe la kulimia, na wengine walisimama pembeni ya ng'ombe wakiwachapa kuwaongoza. Miaka arobaini iliyopita aliwaonea wivu watu hawa. Wakati huo alitamani angekuwa wakulima wale, na ingetokea wangesema wabadilishane kazi angekubali kwa mikono miwili! Lakini sasa hali ilikuwa tofauti. Kwa kujivuna akaangalia msafara wake wa biashara, ngamia na punda walikuwa wamejaa mizigo ya thamani kutoka Damasko. Pamoja na wingi wa mali ile lakini ilikuwa ni sehemu tu ya mali zake.

Alimuonyesha Hadan Gula wale wakulima na kusema, "Bado wanalima shamba lile lile walilokuwa wanalima miaka arobaini iliyopita!"

"Kwanini unafikiri ni wakulima walewale?"

"Niliwaona palepale," akasema Sharru Nada huku kumbukumbu zikimjia, hakujua kwanini kumbukumbu za zamani hazimwachi, ghafla akaona sura yenye tabasamu ya Arad Gula ikimjia. Hapo akaona kikwazo cha kufikia akili ya yule kijana mbinafsi na asiyejali kikiondoka.

Aliwaza jinsi ya kumsaidia kijana yule mwenye kujikweza, na mwenye mawazo ya kutumia na kununua vito tu. Ana kazi nyingi ambazo angeweza kumpa mtu aliyetayari kufanya kazi, lakini si yule anayeona kufanya kazi ni kujishusha. Hata

hivyo bado alihisi ana deni kwa Arad Gula. Hivyo anatakiwa kumsaidia yule kijana kwa uwezo wake wote na si kumsaidia kishingo upande. Yeye na Arad Gula hawakuwa watu wa kufanya mambo kishingo upande.

"Unataka kufahamu jinsi mimi na babu yako tulivyoanza ushirika, ushirika uliotuletea faida kubwa?" Alimuuliza Hadan Gula.

"Kwanini usiniambie jinsi unavyopata shekeli za dhahabu? Hilo ndilo ninalotaka kusikia," alisema Hadan Gula.

Sharru Nada hakujali jibu hilo, akaendelea kusema. "Mara ya kwanza kuonana na wale watu wanaolima nilikuwa na umri kama wako tu. Msafara wetu ulipita karibu na shamba lao. Mzee mmoja aliyeitwa Megiddo ambaye tulikuwa tumefungwa pamoja alisema kwa kejeli kuhusu ulimaji wa wale watu, alisema. 'Ona wale wavivu wanavyolima. Mshika jembe hakandamizi jembe lifike chini, na muongoza ng'ombe hafuati njia vizuri. Watapataje mavuno mazuri kama wanalima hovyo hovyo namna hiyo?'

"Unasema Meggido alikuwa kafungwa pamoja na wewe?" Aliuliza Hadan Gula kwa mshangao.

"Ndiyo, tulifungwa ringi za shaba shingoni na mnyororo mrefu ulituunganisha. Baada ya Megiddo alifuata Zabado, mwizi wa kondoo. Huyu nilimfahamu toka nipo Haroun. Mwisho alikuwa mtu tuliyemwita Haramia sababu hakutuambia jina lake. Tulidhani atakuwa ni baharia kwa sababu alikuwa amejichora tatuu ya nyoka aliyejikunja

kifuani mwake, kama ambavyo mabaharia hujichora. Tulikuwa tunatembea watu wane-wannne tukiwa tumeunganishwa pamoja kwa minyororo.

"Ulikuwa mtumwa?" Aliuliza Hadan Gula akiwa haamini.

"Babu yako hajawahi kukuambia kuwa nimewahi kuwa mtumwa?"

"Alikuwa anakuongelea mara nyingi, lakini hajawahi kugusia hili."

"Babu yako alikuwa ni mtu unayeweza kumuamini kutunza siri hata iwe nzito kiasi gani. Bila shaka na wewe ni mtu ninayeweza kukuamini, sivyo?" Sharru Nada aliongea hayo huku akimkazia macho Hadan Gula.

"Usiwe na shaka, sitasema chochote, lakini hili jambo limenishangaza sana. Ilikuwaje hadi ukawa mtumwa?"

Sharru Nada akabinua mabega na kusema, "Mtu yeyote anaweza kuwa mtumwa. Kamari na pombe ndivyo vilivyonitia matatizoni. Nilikuwa mhanga wa matendo ya hovyo ya kaka yangu. Kaka yangu alimuua rafiki yake katika ugomvi. Baba yangu aliniweka kama dhamana kwa yule mjane ili kumlinda kaka yangu dhidi ya mkono wa sheria. Aliposhindwa kupata pesa ya kunikomboa, yule mama kwa hasira akaniuza kwa mfanyabiashara ya watumwa."

"Hiyi siyo haki kabisa!" Akasema Hadan Gula. "Sasa uliwezaje kuwa huru?"

"Hilo tutalizungumza baadaye kidogo. Acha tuendelee na hadithi yangu.

“Tulipokuwa tunapita wale wakulima walituzomea. Mmoja wao akavua kofia yake na kuinama kwa dhihaka na kusema, “Karibuni Babiloni wageni wa mfalme. Mfalme anawasubiria kwenye kuta za jiji na amewaandalia karamu. Tofali za udongo na supu ya vitunguu. Hapo wakulima wote walicheka kwa sauti kubwa sana.

“Haramia alipandwa na hasira na kuwatukana. ‘Yule mtu anamaanisha nini kusema mfalme anatusubiri kwenye kuta za jiji?’ nilimuuliza Haramia.

“Anamaanisha kwenda kufanya kazi ya kubeba tofali kwenye ujenzi wa kuta za jiji hadi mgongo uvunjike. Kabla ya kuvunjika mgongo, unaweza pigwa hadi kufa. Mimi siwezi pigwa, nitawaua. “

“Haniingii akilini kuongelea kuhusu bwana kumpiga hadi kumuua mtumwa wake anayefanya kazi kwa bidii na kwa kujituma. Mabwana hupenda watumwa watiifu na huwatunza vizuri,” alisema Megiddo.

‘’ ‘Nani anataka kufanya kazi kwa bidii?’ alihoji Zabado. ‘Wale wakulima ni watu wenye akili. Hawafanyi kazi kujichosha, wanategea ila wanajifanya wanafanya kazi kwa bidii.’

‘' ‘Huwezi fika popote kwa kutegea kazi,’ alipinga Megiddo. Ukilima hekari moja kwa siku, ni kazi ya kutosha na bwana anajua hilo. Lakini ukilima nusu hekari tu, huo ni utegezi. Mimi si mtegezi, napenda kufanya kazi kwa ufanisi. Sijutii kuwa na rafiki mzuri kama kazi. Kazi imeniletea vitu

vyote vizuri nilivyowahi kumiliki, shamba, ng'ombe, mazao na vingine vyote.'

'' 'Sasa viko wapi vitu hivyo?' aliuliza Zabado kwa kejeli. 'Mi naonelea ni jambo la akili kutegea kazi. Kama tukiuzwa kwenda kufanya kazi kwenye ujenzi wa ukuta, mimi nitakuwa mbeba maji au kazi zingine rahisi, wewe unaependa kazi utakuwa ukivunja mgongo kwa kubeba tofali,' alimaliza kusema Zabado na kuachia kicheko cha dharau.

"Usiku ule sikuweza kulala, nilikuwa na uoga mkubwa sana. Nilikuwa nimelala karibu na sehemu walipokuwa walinzi. Watu wote walipokuwa wamelala, nikamsogelea mlinzi wa zamu ya kwanza aliyeitwa Godoso. Godoso alikuwa ni aina ya wale waarabu katili sana. Hakujali kitu wala hakuwa na huruma. Kama akikupora pesa atataka akuchinje pia.

'' 'Godoso naomba uniambie kitu kimoja,' nilinong'ona. 'Tukifika Babiloni tutauzwa kwaajili ya kazi ya kujenga ukuta?'

'' 'Kwanini unataka kujua?' aliuliza Godoso kwa udadisi.

'' 'Ina maana huelewi?' nilimwambia kinyonge, mimi bado ni kijana, nataka kuishi. Sitaki kufanya kazi au kupigwa hadi kufa huko kwenye kuta. Kuna uwezekano nikapata bwana mwema?'

'' 'Nitakwambia kitu,' alisema Godoso kwa kunong'ona. Wewe ni mtu mzuri, hujanisumbua kwa lolote. Mara nyingi tunaenda kuuza watumwa kwenye soko la watumwa. Sasa nisikilize kwa makini, wanunuzi wakija waambie wewe ni

mfanyakazi mwenye bidii na unapenda kufanya kazi kwa bwana mwema. Wafanye watake kukununua. Usipofanya hivyo kesho yake utajikuta kwenye kazi ya kubeba tofali, kazi ngumu sana.'

"Baada ya Godoso kuondoka nilijilaza mchangani huku nikiangalia nyota na kufikiria kuhusu kazi. Niliwaza iwapo nitaweza kuifanya kazi kuwa rafiki yangu kama Megiddo alivyosema kuwa rafiki yake mkubwa ni kazi. Niliona ili niepukane na kwenda kutumikishwa kwenye kuta lazima niifanye kazi kuwa rafiki yangu.

"Megiddo alipoamka nikamueleza ile habari. Hilo ndilo lilikuwa tumaini letu pekee la kuepuka mateso ya kufanya kazi kwenye ujenzi wa ukuta. Mchana wa siku hiyo tulikaribia kuta za jiji la Babiloni. Tuliona watu wengi wako kwenye mistari, wengi kama siafu. Walikuwa wakipanda na kushuka kwenye mteremko mkali kupitia njia zilizopindapinda. Tulivyokaribia zaidi tulishangaa kuona maelfu ya watu wakifanya kazi. Kuna waliokuwa wakichimba bwawa kuzunguka ukuta, na wengine wakifyatua tofali. Wengi wao walikuwa wakibeba tofali kwenye vikapu wakiwapelekea wajenzi.

"Wasimamizi waliwatukana walioonekana kutegea, na waliwachapa kwa mijeledi wale ambao hawakufuata mistari. Watumwa wengine walionekana kutembea kidhaifu na wengine wakianguka wasiweze kuinuka tena. Hawa walipigwa mijeledi ili kuwaamsha, na kama walishindwa kuamka walisogezwa pembeni ya njia ambako waliendelea

kuugulia. Baada ya muda waliburuzwa mpaka kwenye rundo la miili mingine iliyokuwa inasubiria maziko yasiyo na heshima. Moyo ulininyong'onyea, nikatetemeka kwa uoga nilipoona mambo hayo. Niliwaza kuwa hali hiyo ndiyo inayonisubiri iwapo nitashindwa kununuliwa kwenye soko la watumwa.

"Ilikuwa kama Godoso alivyosema. Tulichukuliwa mpaka ndani ya jiji na kufungwa kwenye jela ya watumwa. Asubuhi ilipofika tulipelekwa na kufungiwa kwenye mahabusu za soko la watumwa. Hapo watumwa wengi walijikusanya pamoja kwa woga na ni mijeledi ya walinzi ndiyo iliyoweza kuwatenganisha. Mimi na Megiddo tuliongea na kila mnunuzi aliyeweza kutusikiliza.

"Yule mchuuzi wa watumwa alileta wanajeshi kutoka kikosi cha ulinzi wa mfalme. Hawa walimfunga Haramia na kumpiga kikatili alipokuwa akikataa. Nilimuonea huruma walipokuwa wakiondoka naye.

"Megiddo alihisi kwamba naye ataondoka muda si mrefu, hivyo wanunuzi walipokuwa mbali akanisisitiza jinsi ya kufanya kazi kwa bidii kutakavyonipa manufaa hapo baadaye. 'Wengine wanachukia kazi, wanaifanya kuwa adui yao. Ni vyema uifanye kuwa rafiki yako. Jitahidi uipende, usijali hata kama ni ngumu kiasi gani. Mtu anayetaka kujenga nyumba nzuri hatawaza sana juu ya uzito wa nguzo, au umbali wa kufuata maji ya kujengea. Niahidi kuwa iwapo utapata mnunuzi mzuri basi utafanya kazi kwa bidii yako yote. Hata kama hatathamini kazi yako wewe usijali. Kumbuka kuwa

kazi ikifanywa vizuri inamnufaisha anayeifanya. Inamfanya kuwa mtu bora.'

Aliacha kuzungumza pale mkulima mmoja aliposimama karibu yetu na kuanza kutuchunguza.

"Megiddo alimuuliza kuhusu shamba lake na mazao yake. Haikuchukua muda yule mkulima akaona kuwa Megiddo atamfaa. Baada ya mabishano makali kuhusu bei, mkulima yule alitoa pochi kubwa kutoka mfukoni, alilipa na kuondoka na Megiddo.

"Watu wengine wachache waliuzwa asubuhi ile. Ilipofika mchana, Godoso akaniambia kuwa mchuuzi wa watumwa alikuwa kachoka na hakutaka kukaa usiku mwingine pale. Amepanga ikifika jioni atawachukua watumwa waliobaki na kwenda kuwauza kwa mnunuzi wa mfalme. Nilikata tamaa nilipoona mtu mmoja mnene, aliyevalia nadhifu akija na kuuliza iwapo kati yetu kuna mtu ana ujuzi wa kuoka mikate.

"Nilimsogelea na kumwambia, 'Kwanini muoka mikate bora kama wewe unatafuta mwingine ambaye hatakuwa na ujuzi wa juu kama wewe? Huoni kuwa ni rahisi kumfundisha mtu ambaye yuko tayari ili aweze kutengeneza kwa kiwango kama chako? Niangalie vizuri mimi, mimi ni kijana, nina nguvu na nina bidii ya kazi. Nipe nafasi nami nitafanya kila niwezalo kukuzalishia fedha na dhahabu."

"Mtu yule alivutiwa na maelezo yangu na akaanza kubishana na yule mchuuzi. Hapo mwanzo yule mchuuzi alikuwa hana hata habari na mimi, lakini aliposikia nataka kununuliwa akaanza kunipamba kwa sifa. 'Huyu ana afya

njema na tabia njema pia.' Nilijihisi kama ng'ombe aliyenona anayetaka kuuzwa kwa mchinjaji. Baada ya muda walikubaliana bei, nilifurahi sana. Nilimfuata bwana wangu huku nikiwaza kuwa nina bahati kuliko watu wote katika Babiloni.

"Makazi yangu mapya niliyapenda. Bwana wangu, Nana-Naid alinifundisha jinsi ya kusaga shayiri kwenye jiwe, jinsi ya kuwasha moto kwenye jiko la kuokea na jinsi ya kusaga unga laini wa ufuta kwaajili ya keki za asali. Makazi yangu yalikuwa kwenye ghala la nafaka. Kulikuwa pia na mtumwa mwingine, mwanamke mzee aliyekuwa akitunza nyumba, aliitwa Swasti. Swasti alinipenda sana. Alinipatia chakula cha kutosha na alifurahi nilipokuwa nikimsaidia kazi ngumu.

"Hapa nilipata fursa niliyokuwa nimeitafuta sana, fursa ya kumpendeza bwana wangu huku nikiwa na matumaini ya kupata njia ya kuwa huru tena.

"Nilimuomba Nana-Naid anifundishe jinsi ya kukanda na kuoka mikate. Alinifundisha na alifurahi jinsi nilivyokuwa najituma. Nilipoelewa hili kikamilifu nikamuomba anifundishe jinsi ya kutengeneza keki za asali. Baada ya muda mfupi nikawa ndiye muokaji mkuu. Mmiliki wangu alifurahia kukaa na kupumzika siku nzima, lakini hili suala halikumpendeza Swasti, alikuwa akitingisha kichwa na kusema, 'Binadamu kukaa bila kazi si jambo jema kwa afya yake.'

"Kutoka hapo nikaanza kufikiria namna ya kujipatia kipato ili niweze kununua uhuru wangu. Kazi ya kuoka

ilikuwa inaisha mchana, nikawaza iwapo Nana-Naid atanikubalia kwenda kutafuta kazi ya kufanya baada ya hapo, na kisha tugawane malipo yangu. Lakini wazo lingine likanijia, 'Kwanini usitengeneze keki nyingi za asali na uzitembeze kwa watu wenye njaa katika mitaa ya jiji?"

"Nikamueleza Nana-Naid mpango wangu, nikisema: 'Iwapo ningeweza kutumia muda wa baada ya kumaliza kazi kukuzalishia pesa, utakubali tugawane pesa nitakayopata ili niweze kujinunulia mahitaji madogomadogo?

"Hilo halina shida,' alinijibu. Nilipomwambia mpango wa kutembeza keki za asali alifurahi sana.

"Hivi ndivyo itakavyokuwa,' aliniambia. 'Ukiuza keki mbili kwa senti moja mimi nitachukua nusu senti kwaajili ya kulipia unga, asali na kuni za kuokea. Nusu itakayobaki, mimi nitachukua robo na wewe robo.'

"Nilifurahi sana kwa ukarimu wake wa kuniruhusu kubaki na robo ya mauzo yangu. Usiku ule nilifanya kazi kwa bidii kutengeneza sinia kwaajili ya kuuzia. Nana-Naid alinipatia moja ya nguo zake kuukuu ili nionekane nadhifu, Swasti alinisaidia kuishona na kuifua.

"Kesho yake nilioka keki za asali za ziada. Zilivutia na kutamanisha sana ndani ya sinia. Nilipokuwa natembea nilipaza sauti nikitangaza biashara yangu. Mwanzoni hakuna mtu aliyeonekana anazitaka na nikaanza kukata tamaa kuendelea kutembeza. Muda ulivyokwenda watu njaa zikawashika, ndani ya muda mfupi nikawa nimeuza kila kitu.

“Nana- Naid alifurahishwa sana na mafanikio yangu na akanilipa robo yangu. Nilifurahi sana kuanza kuingiza kipato. Megiddo alikuwa sahihi aliposema kuwa mabwana huthamini kazi nzuri za watumwa wao. Usiku ule sikulala kwasababu ya furaha. Nilikuwa nikiwaza ni kiasi gani nitapata kwa mwaka, na nitahitaji miaka mingapi kuweza kununua uhuru wangu.

“Baada ya kuuza kila siku kwa muda fulani nikapata wateja wa kudumu. Mmoja wao alikuwa si mwingine bali babu yako, Arad Gula. Alikuwa akizunguka mji wote, nyumba kwa nyumba akiuza mazulia. Alikuwa akiongozana na punda wa mizigo pamoja na mtumwa wake mweusi. Alikuwa akinunua keki nne, mbili za kwake na mbili za mtumwa wake. Mara zote walisimama na tulizungumza hadi walipomaliza kula.

“Siku moja babu yako aliniambia kitu ambacho sitakuja kukisahau. ‘Kijana napenda keki zako lakini zaidi napenda jinsi unavyofanya biashara yako. Moyo kama huo utakufikisha mbali sana kwenye mafanikio.’

“Lakini wewe Hadan Gula sidhani kama unaelewa umuhimu wa maneno hayo ya kufariji kwa kijana mtumwa. Kijana aliye mpweke ndani ya jiji kubwa, akijitahidi kwa kila hali kujitoa katika aibu ya utumwa”

“Niliendelea kuweka zile senti kwa muda wa miezi mingi. Nilianza kuhisi uzito wake kwenye pochi niliyofunga kwenye mkanda kiunoni. Kama Megiddo alivyokuwa amesema, kazi ilijithibitisha kuwa rafiki yangu wa karibu zaidi. Nilikuwa na furaha sana lakini Swasti alianza kuwa mtu mwenye wasiwasi

mwingi. “Ninapatwa na wasiwasi kwa sababu bwana wetu anatumia muda mwingi sana kwenye nyumba ya kuchezea kamari,’ alisema.

“Siku moja nilikutana na Megiddo mtaani, nilifurahi sana. Alikuwa anawaongoza punda watatu waliobeba mboga kuelekea sokoni. ‘Naendelea vizuri sana,’ aliniambia. ‘Mmiliki wangu anafurahishwa na kazi yangu, na sasa kaniweka kuwa msimamizi. Si unaona hadi ananiamini kwenda sokoni kuuza? Pia ana mpango wa kuniletea familia yangu. Kufanya kazi kwa bidii kumenisaidia kutoka ndani ya matatizo. Siku moja kutanisaidia kujinunulia uhuru wangu mwenyewe, na kuniwezesha kumiliki shamba langu mwenyewe tena.’

“Siku zilivyokwenda biashara ilizidi kushamiri. Nana-Zaid alikuwa kila siku akinisubiria nirudi kwa hamu. Nikifika alihesabu pesa na kuzigawa. Pia alinihimiza kutafuta masoko zaidi ili kuongeza mauzo.

“Mara nyingi nilikwenda nje ya jiji kuwauzia wasimamizi wa watumwa waliokuwa wakijenga ukuta. Sikupenda hali ya kule lakini wasimamizi walikuwa wateja wazuri sana. Siku moja nilishangaa kumuona Zabado akiwa amesimama kwenye mstari akisubiri kikapu chake kiwekwe tofali. Alikuwa amechoka na mgongo wake ulipinda ukiwa na makovu na vidonda vya mijeledi ya wasimamizi. Nilimuonea huruma na kumpatia keki ambayo aliila kwa pupa kama mnyama mwenye njaa kali. Kwa jinsi alivyoziangalia kwa

uchu keki kwenye sinia, niliondoka haraka kabla hajanipora sinia langu.

“Siku moja babu yako, Arad Gula aliniuliza, ‘Kwanini unafanya kazi kwa bidii sana?’ Ni kama tu swali ulilonuliza leo, unakumbuka? Nilimwambia ambacho Megiddo aliniambia kuhusu kazi, na jinsi ambavyo kazi imekuwa rafiki yangu mzuri. Nilimuonyesha pochi yangu yenye pesa kwa kujivuna na kumwambia kuhusu mpango wangu wa kununua uhuru wangu.

‘' ‘Utakapokuja kuwa huru utatafanya kazi gani?’ aliniuliza.

‘' ‘Nina mpango wa kuwa mfanyabiashara,’ nilimjibu.

‘' ‘Hapo Arad Gula aliniambia jambo ambalo sikuamini masikio yangu. ‘Unafahamu kuwa na mimi ni mtumwa? Hii biashara nipo kwenye ushirika na bwana wangu.’

“Ishia hapohapo!” Aling’aka Hadan Gula. “Siwezi endelea kusikiliza ukimvunjia heshima babu yangu. Babu yangu hakuwa mtumwa,” alisema Hadan Gula huku macho yamemuiva wa hasira.

Sharru Nada alikuwa mtulivu na kuendelea kusema. “Namheshimu babu yako kwasababu aliweza kujitoa kwenye matatizo na kuwa raia wa maana sana katika Damasko. Si wewe mjukuu wake ni wa aina hiyo? Je, ni mwanaume unayeweza kuukabili ukweli mchungu, au ni mtu anayependezwa na uongo wa kufurahisha?”

Hadan Gula alikaa vizuri juu ya farasi wake na kwa sauti ya chini na huzuni akasema. “Babu yangu alipendwa na watu

wote. Amefanya mema yasiyo na idadi. Njaa ilipoingia si ni yeye aliyetumia pesa zake kununua nafaka Misri? Si ni yeye aliyetuma msafara wake kuzisafirisha hadi Damasko, na kuwagawia watu ili wasife njaa? Sasa leo unaniambia alikuwa mtumwa wa kudharaulika huko Babiloni!"

"Sharru Nada alijibu, "Kama angeendelea kuwa mtumwa, angekuwa mtu wa kudharaulika. Lakini alipotumia jitihada zake kujitoa na kuwa mtu mashuhuri katika Damasko, Miungu ilifuta aibu yake na kumpa heshima yao."

"Baada ya kuniambia kuwa naye ni mtumwa, akanieleza jinsi ambavyo kwa siku nyingi amekuwa na hamu ya kununua uhuru wake. Sasa amepata pesa za kutosha kununua uhuru wake lakini anawaza kuhusu kazi ya kufanya. Hivi karibuni biashara yake ilikuwa imeyumba, hilo lilimfanyakuogopa kuondoka kwa bwana wake na kujitegemea.

"Nilipinga vikali kusitasita kwake na nikamwambia, 'Huna sababu nzuri ya kuendelea kuwa chini ya bwana wako. Hebu onja tena hali ya kuwa mtu huru. Kuishi kama mtu huru na kufanikiwa ukiwa huru. Amua kile unachotaka kufanya na ukikifanya kwa bidii utakifanikiwa. Kazi itakusaidia kufikia malengo yako.' Aliondoka huku akinishukuru kwa kumsuta juu ya kusita kwa moyo wake."

"Siku moja nilitoka nje ya jiji tena, nilishangaa nilipokuta umati mkubwa wa watu umekusanyika. Nilipomuuliza mtu mmoja kuna nini alinijibu, 'Hujasikia? Kuna mtumwa amemuua mlinzi lakini amekamatwa, atachapwa hadi afe

kwa uhalifu wake. Hata mfalme mwenyewe atakuwepo hapa leo!'

"Watu walikuwa wengi sana wakiwa wamezunguka nguzo ya kumfunga mtuhumiwa anayechapwa. Niliogopa kusogea karibu nisije mwaga sinia langu la keki. Nilipanda juu ya ukuta uliokuwa unajengwa na kuangalia kutoka juu. Siku hiyo ndiyo nilipata bahati ya kumuona Nebkadneza akiwa amepanda gari la kuendeshwa kwa farasi, gari la dhahabu. Sijawahi ona mtu aliyekuwa kapambwa kifahari kiasi kile. Kwenye nguo zake kulikuwa na dhahabu na hariri.

"Sikuweza kuona anayechapwa lakini niliweza kusikia kilio chake. Niliwaza, 'Inakuwaje mfalme wetu mwema anaruhusu ukatili kama ule?' Na cha kushangaza alikuwa anacheka na kutaniana na watu wengine mashuhuri. Hapo nilifahamu kuwa alikuwa ni katili sana, na pia nikaelewa ni kwanini wale watu hufanyishwa kazi ya kujenga ukuta kama wanyama.

"Baada ya mfungwa yule kufa, mwili wake ulitundikwa kwenye nguzo kichwa chini miguu juu ili kila mtu aone. Watu walipopungua nilisogea kuona mwili ule. Kwenye kifua chake niliona tatuu ya nyoka aliyejikunja. Alikuwa ni Haramia!

"Siku niliyokutana tena na Arad Gula alikuwa amebadilika sana. Alikuwa mchangamfu na alinisalimia. 'Tazama mtumwa aliyekuwa unamjua sasa ni mtu huru. Tayari biashara yangu inakua na mke wangu ana furaha. Yeye ni mtu huru pia, ni mpwa wa bwana wangu. Amenishauri tuhamie mji ambao hakuna mtu anayejua kuwa nimewahi kuwa

mtumwa. Anataka watoto wetu wasikue na aibu kuwa baba yao alikuwa mtumwa. Kazi imekuwa msaidizi wangu mkubwa, imenirudishia kujiamini na kuongeza uwezo wangu wa kufanya biashara.'

"Nilifurahi kuwa ushauri wangu ulikuwa umemsaidia.

"Siku moja jioni Swasti alinifuata akiwa mwenye wasiwasi sana: 'Bwana wetu ana tatizo, nina wasiwasi juu yake. Miezi kadhaa iliyopita alipoteza pesa nyingi kwenye mchezo wa kamari. Mkulima ambaye humletea nafaka na asali hajamlipa. Pia alikopa pesa sehemu na hajalipa. Watu hao wana hasira juu yake na wameanza kumtishia.'''

" 'Kwa nini tunajihangaisha na matatizo yake. Sisi si walezi wake,' nilisema bila kufikiri.

'' 'Kijana mpumbavu! Huelewi chochote. Amekuweka wewe kama dhamana kwa mkopesha pesa. Chini ya sheria, mkopeshaji anaweza kukuchukua na kukuuza. Mimi sielewi cha kufanya, Nana-Naid ni bwana mzuri, hata sielewi kwanini amejiingiza kwenye matata haya?'

"Swasti alikuwa sahihi kabisa kuwa na wasiwasi. Asubuhi moja nilipokuwa naoka mikate, mkopesha pesa alifika akiwa na mtu mwingine aliyeitwa Sasi. Yule mtu aliniangalia na kusema kuwa nitafaa.

"Yule mkopesha pesa hakusubiri bwana wangu arudi bali alimwambia Swasti amjulishe kuwa amenichukua. Nilichukuliwa nikiwa na nguo nilizovaa tu na pochi yangu ya pesa kwenye mkanda.

“Nilichukuliwa kama vile mti unaong’olewa toka msituni na kimbunga na kutupwa baharini. Matumaini yangu yalipotea. Kwa mara nyingine kamari na bia zilinileta matatizo.

“Sasi alikuwa ni mkatili na mtu asiye na mzaha. Alipokuwa ananiongoza kupita jijini nilimueleza kuhusu kazi nzuri niliizomfanyia Nana-Naid, na nikamwambia kuwa natumaini kumfanyia kazi nzuri pia. Majibu yake yalikuwa ya kukatisha tamaa kabisa. Alijibu:

‘’ ‘Siipendi hii kazi na bosi wangu haipendi hata kidogo. Mfalme amemuagiza anitume nikajenge sehemu ya mfereji. Ameniambia ninunue watumwa wengi na wafanye kazi kwa bidii ili iishe haraka. Boh! Mtu anawezaje kumaliza haraka kazi kubwa namna ile?”

“Piga picha ya jangwa lisilo na miti bali vichaka vidogovidogo vya hapa na pale. Jua linawaka hadi maji kwenye mapipa yanakuwa ya moto na hayanyweki. Tena piga picha msururu wa watu wakishuka chini unakochimbwa mfereji na kutoka wamebeba vikapu vizito vya udongo toka asubuhi hadi usiku unapoingia. Vuta picha chakula kimewekwa ndani ya karai refu na tumejipanga tukila kama nguruwe. Kulikuwa hakuna hema wala kitanda cha nyasi. Hayo ndiyo maisha niliyoishi. Pochi yangu ya fedha niliichimbia sehemu nilipoweka alama lakini sikuwa na matumaini iwapo nitakuja kuichimbua.

“Mwanzoni nilifanya kazi kwa bidii lakini kadri miezi ilivyozidi kwenda nilianza kukata tamaa. Nilipatwa na homa

kutokana na joto kali na nikapoteza hamu ya kula. Usiku nilikuwa nikijigeuza geuza tu kwa kukosa usingizi.

“Katika taabu ile nilikumbuka maneno ya Zabado, ‘Kutojivunja mgongo kwa kutegea kazi’. Hapo nikakumbuka hali niliyomuona nayo kwa mara ya mwisho. Nikaona kuwa mbinu yake haisaidii kitu.

“Nikamkumbuka Haramia na ujeuri wake. Nikawaza iwapo nipambane na kuua. Lakini kumbukumbu ya mwili wake uliojaa damu ikaniambia kuwa mbinu yake haisaidii kitu.

“Mwishowe nikakumbuka mara ya mwisho niliyoonana na Megiddo. Mikono yake ilikuwa imekomaa kwa kufanya kazi kwa bidii, lakini uso wake ulikuwa ni wenye furaha sana. Mbinu yake ndiyo ilikuwa bora zaidi.

“Lakini nilikuwa nimefanya kazi kadri ya uwezo wangu. Hata Megiddo mwenyewe asingeweza fanya zaidi ya pale. Sasa kwa nini kazi hiyo haijaniletea mafanikio? Je, kweli ni kazi ndiyo iliyompatia Megiddo mafanikio, au ni baraka za Miungu? Inamaana nitafanya kazi maisha yangu yote bila kufikia malengo yangu, furaha na mafanikio? Maswali haya yote yalizunguka kichwani mwangu lakini sikuwa na majibu. Kwa kweli nilikuwa nimechanganyikiwa.

“Siku kadhaa mbele niliona kama uvumilivu wangu umefika mwisho na maswali yangu bado kupata majibu, ghafla niliitwa kwa Sasi. Tarishi alikuwa ametumwa kunipeleka kwa bwana wangu ndani ya Babiloni. Nilichimbua

pochi yangu na kuifunga kwenye nguo zangu zilizochanikachanika na kuondoka.

"Tulipokuwa njiani nilihisi kama kimbunga kinanichukua na kunipeleka huku na huku. Ilikuwa kama naishi kwenye maneno ya ajabu yaliyopendwa kuimbwa nyumbani kwetu Haroun.

Linamuangukia mtu kama kimbunga,
Linampeleka kama tufani,
Hakuna anayejua anakoelekea,
Hakuna ajuaye mwisho wake.

"Inamaana mimi nimeandikiwa kuadhibiwa maisha yangu yote? Ni magumu gani mapya yananisubiri?

"Fikiria jinsi nilivyoshangaa kumkuta Arad Gula kwenye ua wa nyumba ya bwana wangu akinisubiri. Alinisaidia kushuka na kunikumbatia kama vile nilikuwa ndugu yake tuliyepotezana siku nyingi.

"Tulipokuwa tunaondoka nilikuwa namfuata kama vile mtumwa amfuatavyo bwana wake, hakuruhusu hilo. Alizungusha mikono yake kwenye mabega yangu na kusema. 'Nimekutafuta kila sehemu. Nilipokuwa karibu kukata tamaa nikakutana na Swasti ambaye alinisimulia habari ya mkopesha pesa, naye alinionyesha kwa aliyekuwa akikumiliki sasa. Tulibishana sana kuhusu bei na imenigharimu pesa nyingi kukununua lakini sijutii lolote.

Falsafa yako na biashara yangu vimeniwezesha kupata mafanikio haya.

'' 'Ni falsafa ya Megiddo si yangu,' nilimkatiza.

'' 'Ni yako na Megiddo, asanteni nyote. Tunaelekea Damasko na ningependa uwe mshirika kwenye biashara yangu, utakuwa mshirika ukiwa mtu-huru.' Alisema hayo kwa furaha huku akitoa bamba lililoandikwa hati ya kununuliwa kwangu. Aliinua bamba lile juu na kulitupa chini ambapo lilivunjika vipandevipande. Hapo alivikanyagakanyaga vile vipande hadi vikawa vumbi tupu.

"Machozi ya furaha yalinitiririka. Nilitambua kuwa nilikuwa mtu mwenye bahati kuliko watu wote katika jiji la Babiloni.

"Kama ulivyoona, katika nyakati za taabu kazi ilithibitika kuwa ndiye rafiki yangu wa kweli. Utayari wangu wa kufanya kazi kwa bidii uliniokoa nisifanye kazi ngumu ya kujenga ukuta. Pia ulimvutia babu yako hadi akanifanya kuwa mshirika wake."

"Je, pia ni kazi ndiyo ilikuwa ufunguo wa siri ya mafanikio na utajiri wa babu yangu?" Aliuliza Hadan Gula.

"Ndiyo ufunguo pekee aliokuwa nao nilipokutana naye kwa mara ya kwanza." Alijibu Sharru Nada. "Babu yako alipenda kufanya kazi. Kutokana na hilo Miungu ilipendezwa naye na ikambariki.'

"Sasa nimeona," akasema Hadan Gula. "Kazi ilivutia rafiki zake wengi ambao walistaajabia kazi zake na mafanikio iliyoyaleta. Kazi ilimletea heshima aliyofurahia katika

Damasko. Kazi ilimletea yote hayo. Ajabu nilifikiri kazi ni kwaajili ya watumwa!"

"Maisha yana vitu vingi ambavyo binadamu anaweza kufurahia," alisema Sharru Nada. "Kila kitu kina mahala wake. Nafurahi kuwa kazi si kitu cha watumwa tu, ingekuwa hivyo ningekuwa nimenyimwa kitu kizuri sana maishani mwangu. Ninafurahia vitu vingi lakini hakuna ninachofurahia kama kazi."

Sharru Nada na Hadan Gula waliongoza farasi wao hadi kwenye ukuta mrefu wa jiji la Babiloni. Hapo waliingia ndani ya jiji kupitia lango kubwa. Walivyokuwa wanaingia walinzi wa lango walisimama kikakamavu na kumsalimia Sharru Nada kwa saluti..... Kwa kujiamini Sharru Nada aliongoza msafara wake kupita lango la jiji hadi ndani.

"Siku zote nimetamani kuwa kama babu yangu," alisema Hadan Gula. "Lakini sikuwahi jua kuwa alikuwa ni mtu wa aina gani hasa. Kwa kuwa umenieleza sasa natambua. Hilo limenifanya nimheshimu zaidi na kutaka kuwa kama yeye hata zaidi. Nina wasiwasi siwezi kukulipa kwa kuniambia siri ya mafanikio yake. Kuanzia leo nitaitumia siri hiyo. Nitaanza kidogokidogo kama alivyoanza. Hilo ni jambo la manufaa kuliko mapambo ya vito na nguo nzuri.

Baada ya kusema hayo Hadan Gula alitoa hereni toka masikioni mwake, na akavua pete toka vidoleni. Hapo akaongoza farasi wake na kugeuza. Kwa heshima kubwa akaanza kumuendesha farasi wake akiwa nyuma ya Sharru Nada.